Nipashe
Jumatano Septemba 25, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580032
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



## WB yamwaga mamilioni ya Dola miradi maji vijiji 65

UKURASA 3



Ukurasa 18

Chuki kwa wageni zaathiri heshima ya Afrika Kusini

Kura ya mapema kisheria, mitazamo tofauti Zanzibar

Ukurasa 14

Kimataifa

Dunia yatathmini kuondoka Ikulu ya Trump kwa 'mwenye mustachi'

Ukurasa 20

siasa

JUMATANO SEPTEMBA 25, 2019 Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

Chadema: Upinzani kurejesha wabunge wengi uchaguzi ujao- 2

- Ubabe unaoendelea ni sehemu ya siasa
- Sifa mgombea Chadema serikali za mitaa ni uadilifu
- Kesi ya Lissu imeonyesha Mahakama haziko huru nchini

Na Enock Charles

TANZANIA inatarajiwa kufanya uchaguzi wake wa Serikali za Mitaa, Novemba mwaka huu na uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani mwaka ujao.

Kwa hivi sasa vyama vya siasa viko katika maandalizi kwa ajili ya kuibuka na ushindi kwenye ngazi mbalimbali za chaguzi hizo.

Nipashe kupitia kwa mwandishi wake ilifanya mahojiano na Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vicent Mashinji kuhusiana na mambo mbalimbali lakini zaidi chaguzi zijazo nchini. Wiki iliyopita tuliwaletea sehemu ya kwanza ya mahojiano hayo.

Tuliishia kwenye swali la uamuzi wa Mahakama kuhusu umbali wa mita 100 kutoka kwenye kituo cha kupigia kura ambapo Dk. Mashinji aliliweka vizuri. Sasa endelea na sehemu hii ya pili na ya mwisho ya mahojiano hayo:

**SWALI:** Kwa sasa Chadema ina wanachama wangapi?

**JIBU:** Bado hatujafanya tathmini ya nchi nzima, lakini si chini ya milioni sita na tumerecruit (sajili) wapya na sasa hivi tunamalizia ku-compile (kukusanya), au unataka kusema ile ya Polepole ya wanachama milioni 15? Ha ha ha, hizo ni hadithi za Alinacha.

**SWALI:** Ni lini umejiunga na Chadema?

**JIBU:** Mwaka 2011, lakini mimi nimekuwa ni mfuasi wa Chadema ila sikuwa mwanachama rasmi kutoka mwaka 1998.

**SWALI:** Ni changamoto zipi kubwa umekutana nazo toka ushike nafasi ya Ukatibu Mkuu wa Chadema?

Endelea 16

Nyerere mrithi wa Marx mtangulizi kufikia Ujamaa

Ukurasa 15

Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vicent Mashinji. PICHA: MTANDAO

Sakaya: Sina diwani Kaliua, lakini kazi inakwenda sawa Ukurasa 19

UKURASA 13

# IGP Sirro atema cheche



- **Awananga** makamanda wanaosema 'hatoshi', akemea Ma-RPC kuwahukumu watuhumiwa, amtaja Mwangosi... *Endelea ukurasa 2*

## Wakili wa Dk. Tenga atoa ya moyoni

UKURASA 3



## Mtoto wa CDF aliyefariki ajalini aliandaliwa kuwa rubani Bombardier

UKURASA 2

MICHEZO YANGA NI USHINDI TU, ZESCO YAONYA UK.32

MAONI, KATUNI UK.6

# IGP Sirro atema cheche

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Jeshi la Polisi (IGP), Simon Sirro, amekemea kile alichokiita ubinafsi miongoni mwa watendaji wake, akiweka wazi kuwa wapo wasiopendezwa kumwona katika nafasi hiyo.

Vilevile, amekiri jeshi hilo kufanya makosa katika kushughulikia vurugu zilizojitokeza Septemba 2, mwaka 2012 na kusababisha kuuawa kwa mwandishi wa habari, Daudi Mwangosi kwa kupigwa bomu katika Kijiji cha Nyololo, Mufindi mkoani Iringa.

IGP Sirro aliyasema hayo jijini Dar es Salaam jana alipofungua kikao kazi cha siku tatu cha maofisa waandamizi wa Jeshi la Polisi Makao Makuu na makamanda wa mikoa kilicholenga kufanya tathmini ya miaka miwili na miezi saba ya uongozi wake.

Kikao hicho pia kimelenga kupanga mikakati ya kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajia kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

IGP Sirro aliwaeleza maofisa na makamanda hao kuwa kinachosumbua ndani ya jeshi hilo ni ubinafsi, akisisitiza kuwa haiwezekani wote wawe na cheo cha IGP.

"Wakati mwingine wapo wanaona kama sitoshi, wakati nikiwa ninazungumza, mwingine anaona hatoshi huyu, ninatosha mimi, kama unajiona kama unatosha na Mungu hakukupa, sasa si ukubali sasa, mimi nitafanyaje?

"Hakuna njia nikasema sasa, atajuaje kama mimi sitoshi, Kamanda wa Kinondoni unanipata vizuri, umenisikia? Sasa naenda mwaka wa tatu bado unafikiria, kubali yaishe, itafika mahali Mungu akiona unatosha atakupa.

"Sasa, kwa sababu wakati huu mwenyezi Mungu kasema Sirro shikilia hata kama uwezo wako ni mdogo, utavumilia, sasa utafanyaje maana sikujichagua mwenyewe, imekuja nikaambiwa wakati wako ndiyo huu, imekuja na nitaiacha, ninamwomba Mwenyezi Mungu niliache jeshi likiwa na heshima yake," alisema.

IGP Sirro alisema hatakubali kuona historia nzuri ya miaka 100 ya Jeshi la Polisi inaharibika mikononi mwake.

"Jeshi haliharibiki mikononi mwetu, siyo kwangu tu, unafikiri likaharibika jeshi ni Sirro peke yake, hapana! Historia itawarudia wote.

'Sina tabia ya kumchukia mtu, unapomchukia mtu, wewe mwenyewe unajipa matatizo, unaanza kumchukia Shilogile, chuki utaendelea nayo, sitakuwa na amani. Maisha yenyewe mafupi hapa duniani, kwa nini nifanye hivyo?

"Kinyongo niweke, hicho kinyongo nikiendelea nacho kitaendelea kuwa kinyongo ndani ya nafsi yangu, sasa raha nitaipataje? Labda niseme mimi siyo wa namna hiyo, hii ni ajira, leo nipo kesho sipo, ninawaomba sana tushirikiane, ushirikiano ndiyo nguzo ya kutusaidia," alisema.

**MA-RC KUHUKUMU WATUHUMIWA**

IGP Sirro pia alieleza kushangazwa na baadhi ya makamanda wa polisi kuwasimamisha kwenye vyombo vya habari watuhumiwa na kuwahoji hadharani kwa nia ya kutafuta sifa.

"Huyu ni mtuhumiwa, leo unamtangaza kaiba, unasahau kesho na keshokutwa, kesho ukiwa kwenu Musoma anakushtaki, wakati huo hata nauli ya kukuleta huna.

"Wakati mwingine unampa mtu nafasi anaona yeye ndiyo yeye, anaweza kufanya kila kitu, angalieni nchi nyingine ni nadra kukuta mtuhumiwa anaonyeshwa, labda tukio kubwa, siyo mtu kaiba televisheni," alisema.

Katika kikao hicho, IGP Sirro pia alitishia kutengua uteuzi wa kamanda ambaye angeshindwa kujieleza kwanini nyumba za makazi ya polisi kwenye mkoa wake hazijakamilika.

INAENDELEA UK. 8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitia saini kitabu cha maombolezo ya kifo cha Nelson Mabeyo, ambaye ni mtoto wa Mkuu wa Majeshi nchini, Jenerali Venance Mabeyo, nyumbani Msasani, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OWM**

# Mtoto wa CDF aliyefariki ajalini aliandaliwa kurusha Bombardier

**Na Elizabeth Zaya**

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), Ladislaus Matindi, amesema Nelson Mabeyo, aliyefariki katika ajali ya ndege juzi, alikuwa mwajiriwa mtarajiwa wa shirika hilo.

Aidha, amesema Nelson alikuwa ameandaliwa kwa mafunzo ya kurusha ndege ya shirika hilo aina ya Bombardier.

Akizungumza na Nipashe, Matindi alisema tayari Nelson ambaye ni mtoto wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Jenerali Venance Mabeyo, alikuwa amefanya usaili katika shirika hilo.

"Nelson alikuwa ni rubani mzuri na alishika nafasi ya pili katika usaili wetu, na marubani 16 waliajiriwa na ATCL hivi karibuni," alisema Matindi na kuongeza:

"Alikuwa aondoke mapema kwenda Canada kwa ajili ya mafunzo ya kurusha Bombardier, ila aliomba amalize mkataba wake na mwajiri wake."

Nelson alikuwa rubani katika ndege ya Kampuni ya Auric Air na alifariki juzi baada ya ndege hiyo kuanguka katika uwanja mdogo wa ndege wa Seronera uliopo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

Ajali hiyo ilitokea saa 1:30 asubuhi wakati ikipaa katika uwanja huo kwa ajili ya kuelekea mkoani Arusha.

Nelson alikuwa na rubani mwanafunzi, Nelson Orutu ambaye alifariki dunia.

# Neema yawaangukia mapacha walioungana

**Na Mary Geofrey**

MWAKA mmoja tangu watoto pacha waliokuwa wameungana maeneo ya tumboni na maini, wakafanyiwe upasuaji wa kutenganishwa, wamekabidhiwa nyumba ya kisasa ya kuishi.

Watoto hao Gracious na Precious, walifanyiwa upasuaji Septemba 23 mwaka jana, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) kwa mafanikio baada ya kuzaliwa wakiwa wameungana.

Nyumba hiyo ilijengwa na Benki ya UBA kwa gharama ya Sh. milioni 18, ilikabidhiwa kwa wazazi wa watoto hao jana na Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo.

Jokate alisema ujenzi wa nyumba hiyo umekamilika kwa siku 28, baada ya maandalizi ya muda mrefu ya kutafuta eneo lililopo karibu na huduma za kijamii kama shule na kituo cha afya kupatikana.

Alisema eneo hilo lilinunuliwa na Balozi wa Visiwa vya Shelisheli, Maryvonne Pool na Benki ya UBA waligharamia ujenzi wa nyumba hiyo na kuweka umeme.

"Leo ninayofuraha kubwa kukabidhi nyumba ya watoto hawa mapacha waliokuwa wameungana, MNH kwa kushirikiana na ofisi yangu, tulijitahidi kuhakikisha mama huyu anapata huduma za malazi salama kwa ajili ya kuangalia afya za watoto hawa," Jokate alisema.

Aidha, aliagiza Ofisa Tarafa ya Mzenga Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, kuhakikisha hati ya nyumba inapatikana na kuwekwa majina ya watoto hao ili kuepuka migogoro ya familia.

Awali Daktari Bingwa wa Watoto wa MNH, aliyewafanyia upasuaji Dk. Zaituni Bokhari, alisema mwaka mmoja tangu wawafanyie upasuaji watoto hao, wamewakuta wakiwa wenye afya njema.

Alisema waliwafanyia upasuaji wa kuwatenganisha maini na kuwatengeneza kitovu na kwamba hali zao zinaendelea vizuri.

"Tuna furaha kubwa kabisa kuona hali za watoto hawa zinaendelea vizuri, wamepona vizuri, ngozi imeunga vizuri na wanaenda haja bila shida yoyote," Dk. Zaituni alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa UBA, Usman Isiaka, alisema UBA ilivutiwa na huduma zilizotolewa na MNH za kuwatenganisha na kugharamia matibabu yao yote ya Sh. milioni 34 hivyo wakaona ni muhimu wakawasaidia nyumba ya kuishi.

Alisema mbali na nyumba hiyo, wamewakatia bima ya matibabu ya miaka 10 na kuwafungulia akaunti na kuweka akiba ya Sh. milioni mbili.

"Tumefurahi kuona nyumba hii imejengwa eneo zuri karibu na huduma za jamii kama shule na kituo cha afya. UBA pia tunaendelea kuwasaidia watoto hawa kwa kuwapa bima ya matibabu ya miaka 10 kuanzia mwaka jana," Isiaka alisema.

Naye mama mzazi wa watoto hao, Ester Simon, mbali na kuishukuru UBA, MHN na Balozi wa Visiwa vya Shelisheli, aliomba kuwekewa uzio wa nyumba ili kudhibiti watoto hao wasiweze kucheza barabarani.

Balozi Shelisheli nchini, Maryvonne, aliahidi kuwajengea uzio na kuwapa kitanda na godoro la kulalia watoto hao.

## HABARI KITAIFA

## Kairuki aipa TIC siku 7 kwenda Ruvuma

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Uwekezaji, Angellah Kairuki, ameutaka uongozi wa Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) kutembelea na kugakua mazingira ya wafanyabiashara na wawekezaji wazawa waliopo mkoa wa Ruvuma ndani ya siku saba.

Alitoa agizo hilo alipotembelea na kukagua viwanda vya kutengeneza kahawa vya Wilaya ya Mbinga, MCCCO na DAE, kwa ajili ya kukagua mazingira na utendaji wa viwanda hivyo mkoani humo.

Katika ziara hiyo aliambatana na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Christina Mdeme pamoja na watendaji kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Wizara ya Viwanda, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Nishati, Wizara ya Madini, Wizara ya Ardhi, pamoja na baadhi ya taasisi za serikali na TIC.

Waziri Kairuki alitoa maelekezo hayo baada ya kubaini kuwa taasisi hiyo haijawafikia wawekezaji wazawa kikamilifu hususani waliopo mikoani ili kuwatambua na kuwaelimisha kuhusu fursa zinazotolewa na taasisi hiyo.

"Ninawaagiza TIC mfike katika viwanda hivi ndani ya siku saba kuanzia sasa ili kuwatembelea na kuwaeleza huduma zinazotolewa na taasisi yenu ikiwamo fursa zilizopo na endapo wataona inafaa wajisajiri kwa kuwa ni suala la hiari," alisisitiza Waziri Kairuki.

Alisema kuwa ipo tija ya kuwatambua wawekezaji wazawa waliopo nchini kwa kuzingatia mchango wao katika uchumi wa viwanda kwa kuzingatia mwaka huu ni wa uwekezaji.

INAENDELEA UK. 8

# Wakili wa Dk. Tenga aomba kuzungumza na wateja wake

**Na Hellen Mwango**

UPANDE wa utetezi katika kesi ya uhujumu uchumi na kutakatisha fedha inayowakabili vigogo wa Kampuni ya Mawasiliano ya Six Telecoms Limited, akiwamo Wakili maarufu Dk. Ringo Tenga, umeiomba mahakama kuwapa muda kuzungumza na wateja wao kuhusu kesi hiyo.

Awali upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Constantine Kakula ulidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba kuwa shauri hilo limefika mahakamani hapo kwa ajili ya kutajwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Kakula alidai upande wa utetezi wana jambo ambalo wanataka kuiambia mahakama hiyo.

Wakili wa utetezi, Alex Mgongolwa, aliomba mahakama kuitisha kesi hiyo Septemba 27, mwaka huu, kwa sababu ya mazingira ya kesi yenyewe wanaomba wazungumze na wateja wao.

Hakimu Simba aliahirisha kesi hiyo hadi Septemba 27, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa na washtakiwa wote wamerudishwa rumande kwa sababu mashtaka yanayowakabili hayana dhamana.

Julai 26, mwaka huu, upande wa utetezi uliowakilishwa na Wakili Bryson Shayo uliomba mahakama kuipangia kesi hiyo wiki mbili ili apate muda wa kushauriana na wateja wao.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Hafidhi Shamte au Rashidi Shamte ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, mfanyabiashara na mkurugenzi wa kampuni hiyo, Peter Noni, Mkuu wa Fedha Noel Chacha na Kampuni ya Six Telecoms.

Dk. Tenga na wenzake wanadai kuwa kati ya Januari 1, 2014 na Januari 14, 2016 Dar es Salaam, walitoza malipo ya mawasiliano ya simu za kimataifa chini ya kiwango cha Dola za Marekani 0.25 kwa dakika kwa lengo la kujipatia faida.

Katika kipindi hicho wanadaiwa kuhujumu miundombinu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kutoza gharama chini ya kiwango na kushindwa kulipa Dola za Marekani 3,282,741.12 kwa TCRA kama malipo ya mapato.

Pia wanadaiwa katika kipindi hicho walishindwa kulipa ada za udhibiti za Dola za Marekani 466,010.07 kwa TCRA.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa waliisababishia TCRA hasara ya Dola za Marekani 3,748,751.22 (sawa na Sh. bilioni nane ).




Wafanyabiashara wadogo maarufu kama Machinga, wakiendelea na shughuli zao, katika barabara ya mabasi ya mwendokasi, jirani na kituo cha Msimbazi Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wao. **PICHA: JOHN BADI**

# WB yamwaga mabilioni ya maji vijiji 65

**Na Salome Kitomari**

VIJIJI 65 katika mikoa minane nchini vinatarajiwa kunufaika na upatikanaji wa maji safi na salama kutokana na maboresho ya pampu za maji zinazokuwa zinatumia mafuta ya diseli kutumia umeme wa jua.

Mafanikio hayo yanatokana na makubaliano yaliyoingiwa baina ya serikali na Benki ya Dunia (WB), kutoa Dola milioni 4.5 kutoka mpango 'Global Partnership for Results-Based Approaches (GPRBA)'.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na WB, ushiriki wake katika sekta ya maji nchini unakuja na mradi mkubwa wa majaribio wa kutumia pampu zinazoendeshwa kwa umeme wa jua ambao ni ubunifu wa kuisaidia serikali kusonga mbele kutoka kwenye matumizi ya pampu za mafuta ya dizeli hadi kutumia pampu za umeme wa jua ambazo zinatunza mazingira.

Taarifa hiyo ilisema mfumo huo mpya utawezesha vijiji vingi kupata maji safi na salama na kupunguza gharama za maji kwa kunufaisha watu 500,000

"Mradi huu unafungua rasilimali mpya za uwekezaji kwenye maeneo ya vijiji kwa kuondoa tofauti iliyopo kati ya upatikanaji wa maji vijijini na mijini, pia kuhamisha uhamasishaji wa sekta binafsi kutekeleza mradi husika na kujihusisha na mpango wa WB wa fedha kwa maendeleo ya watu," alisema Kaimu Mkuu wa GPRBA, Zaruhi Tokhmakhian.

Alisema ni mara ya kwanza kwa benki hiyo kuelekeza kiwango kikubwa cha fedha kwa sekta binafsi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye sekta ya maji vijijini.

Utoaji wa ruzuku za GPRBA na kusambaza vyanzo, alisema kunaongeza mzunguko wa fedha na kuimarisha huduma mbalimbali za kijamii.

Kwa mujibu wa Tokhmakhian, WB itatoa asilimia 60 ya zuruku kwa ajili ya mikopo kwa kamati za maji za kijamii kuachana na matumizi ya genereta za diseli na kutumia umeme wa jua itakaweza kusukuma maji.

Alisema asilimia 40 ya fedha hizo za mkopo zitawekezwa kwenye kamati za maji ambazo zitawajibika kurejesha mkopo huo kwa kipindi cha miaka minne.

Mkuu huyo pia alisema malipo ya maji yatafanyika kwa kutumia simu za mkononi kwa lengo la kutambua makusanyo ya mauzo ya maji kutoka kwenye kamati na kupeleka kwenye benki za maeneo husika.

Alisema fedha hizo zitakazotolewa kwenye kamati hizo zitajumuisha na utoaji wa mafunzo kwa watendaji ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ubora unaotakiwa ikiwamo kuweza kukopa zaidi kwa ajili ya miradi ijayo.

Taarifa hiyo ilibainisha kuwa pamoja na kurahisisha upatikanaji wa maji kwa wananchi kwa karibu na uhakika, pia watakwenda hadi kwenye ukarabati wa miradi ya umwagiliaji, kupunguza gharama za uendeshaji na matengenezo huku ushiriki wa sekta binafsi ukiwa mkubwa kwa miaka mitano ijayo.

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

NAFASI ZA KAZI

MWANDISHI WA HABARI WA KUJITEGEMEA

Gazeti la Nipashe linatangaza nafasi kwa Mwandishi wa habari wa kujitegemea kutoka mikoa yote nchini.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

1. Awe amefanyakazi angalau miaka mitatu (3) kwenye chombo cha habari
2. Ajue misingi, miiko na maadili ya uandishi wa habari
3. Awe mwenye kujituma na mbunifu katika kutafuta habari

Mwombaji awasilishe maombi yake kupitia barua pepe **nipashe.gazeti@nipashe.co.tz**

*Mwisho wa kutuma maombi ni Septemba 30*

615421902

# Serikali yaridhia kufuta mapori tengefu 12

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeridhia kufuta mapori tengefu 12 yenye ukubwa wa ekari 707,659.94 ambayo yamepoteza sifa na imeamua yagawiwe kwa wananchi kwa ajili ya shughuli za makazi, kilimo na mifugo.

Uamuzi huo umefikiwa juzi kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri kilichoongozwa na Rais John Magufuli, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Akitoa taarifa baada ya kikao hicho, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema mawaziri wa kisekta wakiongozwa na Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, walichambua na kuandaa taarifa ya mapendekezo ya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi nchini iliyowasilishwa katika kikao cha Baraza la Mawaziri juzi.

"Mawaziri walichambua na kubaini kuwa vijiji vyenye migogoro ni 975 na siyo 366 kama ilivyotangazwa awali, Baraza limeamua kwamba vijiji 920 vitabaki ndani ya hifadhi, mipaka irejewe upya, vipatiwe vyeti vya ardhi vya kijiji pamoja na kupangiwa mipango ya matumizi bora ya ardhi," alisema na kuongeza kuwa orodha ya vijiji hivyo itatangazwa baadaye.

Waziri Mkuu alisema serikali imeridhia misitu ya hifadhi saba yenye ukubwa wa ekari 46,715 iliyopoteza sifa itolewe kwa wananchi kwa ajili

INAENDELEA UK.8

# Waziri atumbua mameneja maji

**Na Dege Masoli,** PANGANI

NAIBU Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, amewatumbua vigogo wawili wa maji wa Wilaya ya Pangani kutokana na tuhuma mbalimbali ikiwamo kushindwa kusimamia miradi ipasavyo na kuisababishia serikali hasara ya mamilioni ya shilingi.

Aidha, Aweso amevunja jumuiya ya watumia maji ya kijiji cha Msalaza wilayani hapa na kuagiza vyombo vya usalama kuuhoji uongozi wa jumuiya hiyo kutokana na kile alichodai kuwapo harufu ya ubadhilifu wa mamilioni ya fedha zinazotokana na mauzo ya maji.

Waliotumbuliwa kwenye mkutano wa wadau wa Maji Mkoa wa Tanga uliofanyika wilayani ni Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RUWASA) wa Wilaya ya Pangani, Injinia Ladislaus Modestus na Meneja wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Pangani (Pawasa), Adam Sadick.

Kwa mujibu wa Aweso, changamoto nyingi za miradi ya maji nchini zinatokana na usimamizi mbovu wa wataalamu na kwamba hatua zinazochukuliwa zina lengo la kuwataka wabadilike.

Alisema kasumba za wataalamu kutegemea taarifa za watu wa chini ni kikwazo katika juhudi za serikali za kumtua mama ndoo kichwani na kuwataka sasa wabadilike na wajenge utaratibu wa kujiridhisha kwa kwenda kwenye miradi kujionea hali halisi badala ya kuridhika na taarifa za kupelekewa ofisini.


Katika kikao hicho ambacho alikutumia kupokea malalamiko ya makandarasi wanaotekeleza miradi mbalimbali ya maji mkoani Tanga, Aweso aliiagiza Ruwasa kutekeleza mambo matatu kwenye jumuiya zote za watumia maji nchi nzima ambayo alidai ndio mwarobaini wa changamoto za maji.

Mbali na kuwatimua wataalamu hao, maagizo mengine ni kuundwa tume ya kuchunguza miradi yote ya maji mibovu wilayani humo na Ruwasa kuzisaidia jumuiya za watumia maji zinazofanya

INAENDELEA UK.8



Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo (wa nne kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya UBA, Usman Isiaka, (wa tatu kushoto), wakizindua nyumba ya vyumba viwili, sebule na jiko iliyojengwa na benki hiyo, wilayani Kisarawe, Mkoa Pwani jana, kwa ajili ya watoto mapacha waliokuwa wameungana eneo la tumbo na maini na kufanikiwa kutengenishwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), mwaka mmoja uliopita. **PICHA: MARY GEOFREY**




# Mahakama Kisutu leo kuamua Mashinji, Matiko kusafiri au la

**Na Hellen Mwango**

HATIMA ya kuruhusiwa au la kwa Katibu Mkuu Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vicent Mashinji na Mbunge wa Tarime mjini, Esther Matiko kwenda nje ya nchi itajulikana leo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Mashinji na vigogo wengine saba wa Chadema akiwamo Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe wanakabiliwa na mashtaka 13 ya uchochezi.

Wakili wa Serikali Mkuu, Faraja Nchimbi, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kusikiliza ushahidi wa utetezi, lakini mshtakiwa Mashinji hayupo mahakamani.

Wakili wa utetezi Profesa Abdallah Safari, alidai mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, kwamba wana maombi mawili ya kuyawasilisha.

Ombi la kwanza ni kuitaarifu mahakama kwamba Dk. Mashinji ameshindwa kuhudhuria kesi hiyo kwa sababu ana kesi nyingine iliyopangwa Septemba 23, mwaka huu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Songea.

Ombi la pili, Matiko anakwenda kuwakilisha Bunge Kigali, nchini Rwanda na Ubelgiji.

Alidai kuwa Dk. Mashinji anatarajia kusafiri Septemba 29 mpaka Oktoba 6, mwaka huu na Matiko mkutano utaanza Septemba 25 mpaka 28, mwaka huu na mwingine utaanza nchini Ubelgiji Oktoba 7 na 8, mwaka huu.

Nchimbi alidai kuwa wamepokea hati ya Dk. Mashinji kuitwa Mahakama ya Songea kwa hilo hatuna pingamizi.

Alidai kuwa kuhusu ruhusa washtakiwa hao wanafahamu kwamba tarehe wanazosafiri kesi yao inasikilizwa hivyo upande wa Jamhuri unapinga wasiruhusiwe.

Hakimu Simba alisema atatoa uamuzi huo leo asubuhi.

Mbali ya Mbowe, Dk. Mashinji, Matiko, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni, Katibu Mkuu Taifa, Dk. Mashinji , Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, mbunge wa Tarime vijijini, John Heche, Mbunge wa Iringa mjini, Peter Msigwa na Mbunge wa Kawe Halima Mdee.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Mjini, Matiko na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kula njama.

Wanadaiwa kuwa, Februari 1 na 16, mwaka jana, jijini Dar es Salaam waliku a njama ya kutenda kosa la kufanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko la kutawanyika.

TANGAZO

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## PRESIDENT'S OFFICE - REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
## KAHAMA TOWN COUNCIL

KAHAMA TOWN COUNCIL

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION
### AS AT 30 JUNE 2018

| | Notes | 2018 TZS | 2017 TZS |
|---|---|---|---|
| **ASSETS** | | | |
| **Current assets** | | | |
| Cash and cash equivalents | 20 | 3,795,113,654 | 3,594,682,817 |
| Receivables and prepayments | 21 | 10,475,782,345 | 10,499,534,893 |
| Inventories | 22 | 1,181,787,435 | 1,326,820,489 |
| Other financial assets | 25 | - | - |
| | | 15,452,683,434 | 15,421,038,199 |
| **Non-current assets** | | | |
| Other financial assets | 25 | 36,000,000 | 24,000,000 |
| Property plant and equipment | 23 | 75,613,659,863 | 77,912,287,983 |
| Intangible assets | 24 | - | - |
| Investment property | 30 | - | - |
| | | 75,649,659,863 | 77,936,287,983 |
| **TOTAL ASSETS** | | 91,102,343,298 | 93,357,326,183 |
| **LIABILITIES** | | | |
| **Current liabilities** | | | |
| Payables | 26 | 4,133,438,856 | 3,000,774,148 |
| Employee benefits | 27 | 771,429,331 | 497,065,450 |
| Deferred recurrent (Grant) | 11 | 743,619,240 | 2,297,660,800 |
| | | 5,648,487,427 | 5,795,500,398 |
| **Non-current liabilities** | | | |
| Deferred capital (Grant) | 28 | 7,429,308,958 | 11,104,593,493 |
| | | 7,429,308,958 | 11,104,593,493 |
| **TOTAL LIABILITIES** | | 13,077,796,385 | 16,900,093,891 |
| **NET ASSETS** | | **78,024,546,912** | **76,457,232,292** |
| **NET ASSETS** | | | |
| Accumulated surplus/(deficit) | | **78,024,546,912** | **12,540,903,442** |
| Available for sale financial assets | | - | - |
| Revaluation surplus | | - | 63,916,328,850 |
| **TOTAL NET ASSETS** | | **78,024,546,912** | **76,457,232,292** |

The notes on pages 20 to 67 form part of these financial statements.

These financial statements were approved by the Full Council Meeting on 28th September 2018 and signed on its behalf by:

Mr. Anderson D. Msumba
Town Director
TOWN DIRECTOR
KAHAMA TOWN COUNCIL

Hon. Abel S. Kishushu
Town Council Chairman
CHAIRMAN
KAHAMA TOWN COUNCIL

### STATEMENT OF FINANCIAL PERFORMANCE
### FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2018

| | Notes | 2018 TZS | 2017 TZS |
|---|---|---|---|
| **Revenue** | | | |
| Local taxes | 9 | 3,934,279,718 | 5,127,756,292 |
| Fees, fines, penalties and licenses | 10 | 777,918,954 | 1,551,905,590 |
| Recurrent grants | 11 | 27,361,700,367 | 27,245,537,673 |
| Amortisation of capital grant | 28 | 560,768,226 | 1,346,471,990 |
| Other own revenue | 13 | 502,307,972 | 206,228,627 |
| | | **33,136,975,236** | **35,477,900,172** |
| **Expenses** | | | |
| Wages, salaries and employee benefits | 14 | 22,064,631,093 | 22,520,905,616 |
| Supplies and consumables used | 15 | 4,060,416,807 | 5,243,542,661 |
| Maintenance expenses | 16 | 1,204,497,775 | 2,426,501,223 |
| Grants and other transfer payments | 17 | 3,708,993,923 | 1,122,010,060 |
| Finance costs | 18 | - | - |
| Depreciation of property, plant and equipment | 23 | 858,581,237 | 1,759,240,689 |
| | | **31,897,120,835** | **33,072,200,250** |
| Share of associates surplus/(deficit) | | - | - |
| **Surplus/(deficit) during the year before adjustments** | | **1,239,854,401** | **2,405,699,923** |
| Own source fund contributed to capital grants | | 1,134,571,284 | 1,442,994,217 |
| **Surplus/(deficit) during the year** | | **105,283,116** | **962,705,706** |

These financial statements were approved by the Full Council Meeting on 28th September 2018 and signed on its behalf

Mr. Anderson D. Msumba
Town Director
TOWN DIRECTOR
KAHAMA TOWN COUNCIL

Hon. Abel S. Kishushu
Town Council Chairman
CHAIRMAN
KAHAMA TOWN COUNCIL

### CASH FLOW STATEMENT
### FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2018

| | Note | 2018 TZS | 2017 TZS |
|---|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | | |
| ***Receipts*** | | | |
| Taxes and levies | WI | 3,804,402,318 | 5,380,126,499 |
| Fees, fines, penalties and licenses | W2 | 735,313,954 | 1,325,342,090 |
| Recurrent grants | W3 | 25,209,917,655 | 27,623,845,562 |
| Other income | W7 | 175,843,222 | 206,228,627 |
| Receipts for Deposit Account | | 2,235,543,289 | 2,192,866,335 |
| **Total Cash Received from Customers** | | **32,161,020,437** | **36,728,409,113** |
| ***Payments*** | | | |
| Employee costs | W4 | (21,790,267,212) | (22,298,707,666) |
| Payments to suppliers | W5 | (2,597,146,754) | (6,970,854,144) |
| Maintenance expenses | W8 | (1,204,497,775) | (2,426,501,223) |
| Grants and other transfer payments | W6 | (3,894,566,214) | (1,121,119,854) |
| Other expenses | | - | - |
| Payments for Deposit Account | | (1,409,178,960) | (1,324,407,516) |
| **Total Cash Paid to Suppliers and Employees** | | **(30,895,656,915)** | **(34,141,590,403)** |
| **Net cash from operating activities** | | **1,265,363,521** | **2,586,818,710** |
| **Cash flows from investing activities** | | | |
| Acquisition of property, plant, and equipment & investment properties | 23 | (2,180,192,722) | (3,134,303,246) |
| Acquisition of investments (LGLB) | 25 | - | - |
| **Net cash from investing activities** | | **(2,180,192,722)** | **(3,134,303,246)** |
| **Cash flows from financing activities** | | | |
| Development grants received | 39 | 1,115,260,037 | 1,491,501,665 |
| **Net cash used in financing activities** | | **1,115,260,037** | **1,491,501,665** |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | | **200,430,836** | **944,017,129** |
| **Cash and cash equivalents at beginning of period** | | **3,594,682,817** | **2,650,665,689** |
| **Cash and cash equivalents at end of period** | 20 | **3,795,113,654** | **3,594,682,817** |

These financial statements were approved by the Full Council Meeting on 28th September 2018 and signed on its behalf by:

Mr. Anderson D. Msumba
Town Director
TOWN DIRECTOR
KAHAMA TOWN COUNCIL

Hon. Abel S. Kishushu
Town Council Chairman
CHAIRMAN
KAHAMA TOWN COUNCIL

### STATEMENT OF CHANGES IN NET ASSETS
### FOR THE YEAR ENDED 30 JUNE 2018

| | Accumulated surplus/deficit TZS | Revaluation surplus TZS | Total TZS |
|---|---|---|---|
| **Balance at 1 July 2016** | 11,578,197,736 | - | 11,578,197,736 |
| Amount previously recorded as expenses | - | - | - |
| Changes in accounting policy/errors | - | - | - |
| **Restated balance** | 11,578,197,736 | - | 11,578,197,736 |
| Surplus/(Deficit) for the year | 962,705,706 | - | 962,705,706 |
| Own source fund capitalised | | | |
| Changes in revaluation surplus/(deficit) | - | 63,916,328,850 | 63,916,328,850 |
| Transfer to and from surplus/deficit | - | - | - |
| **Balance at 30th June 2017** | **12,540,903,442** | **63,916,328,850** | **76,457,232,292** |
| **Balance at 01st July 2017** | 76,457,232,292 | | 76,457,232,292 |
| Surplus/(Deficit) for the year | 105,283,116 | - | 105,283,116 |
| Own source fund capitalised | | | |
| Changes in revaluation surplus/(deficit) | | | - |
| Transfer to and from surplus/deficit | 1,462,031,504 | - | 1,462,031,504 |
| | | - | - |
| **Balance at 30th June 2018** | **78,024,546,912** | **63,916,328,850** | **78,024,546,912** |

These financial statements were approved by the Full Council Meeting on 28th September 2018 and signed on its behalf by:

Mr. Anderson D. Msumba
Town Director
TOWN DIRECTOR
KAHAMA TOWN COUNCIL

Hon. Abel S. Kishushu
Town Council Chairman
CHAIRMAN
KAHAMA TOWN COUNCIL

In my opinion, the accompanying financial statements of the Kahama Town Council are prepared in all material respects, in accordance with International Public Sector Accounting Standards (IPSAS) Accrual basis of accounting and in the manner required by the Local Government Finances Act 1982, revised 2000.

Prof. Mussa Juma Assad,
Controller and Auditor General
31st March, 2019

National Audit Office of Tanzania,
P.O. Box 950,
11101 Dodoma, Tanzania.
Tel: 255 (026) 2321759
Fax: 255 (026) 2117527
Email: ocag@nao.go.tz

215431602

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusaidie wenye ulemavu huduma za wakalimani

**KATIKA** mambo ambayo watu wenye ulemavu wanayaainisha kuwa yanawakwamisha kwenye kupata huduma ni ukosefu wa mawasiliano hasa ya lugha ya alama kwenye maeneo nyeti na ya muhimu.

Tatizo jingine ni kukosa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu iwe kwenye ofisi za serikali, ndani ya usafiri, shuleni na pia hospitalini ambako kila mtu ni lazima anakwenda.

Tukianza na changamoto za kukosa mawasiliano ya lugha ya alama, ni ukweli kuwa hakuna wakalimani wa kutosha kusaidia wasiosikia wanapotafuta huduma kwenye vituo vya polisi, mahakamani, gerezani na mahabusu.

Kukosekana wakalimani kunawalazimisha kuomba serikali kuona ulazima na uharaka wa kuajiri watu hao kwenye maeneo hayo muhimu kwenye huduma za kutafuta haki.

Katika kufikisha ujumbe huo kwa serikali Chama cha Visiwi (Chavita), Wilaya ya Hai kinaeleza umuhimu wa kupata wakalimani kwenye maeneo hayo ambayo yako ndani ya sheria na haki za binadamu.

Viongozi wa Chavita wanatoa ujumbe huo katika mafunzo kwa maofisa wa polisi, magereza na mahakimu kuhusu matumizi ya lugha ya alama katika maeneo wanayofanyia kazi.

Tunaungana na Chavita kwenye kutafuta wakalimani hasa upande eneo hilo la sheria na haki za binadamu ambalo watu wengi wameumia kutokana na kushindwa kufahamu wenye ulemavu walitaka kusema nini na iwapo kilichofanyika kimewapa haki. Pamoja na umuhimu wa kuwa na wakalimani kwenye eneo hilo ikumbukwe kuwa kuna changamoto nyingi hata ndani ya huduma za afya kama hospitalini ambako pia wagonjwa hawawezi kuwasiliana na wauguzi na madaktari.

Wakati mwingine inakuwa vigumu hata kwenye masuala ya uzazi kuwasiliana na wasiosikia kutokana na kukosekana mtaalamu wa lugha ya alama.

Ni dhahiri kuwa si mahakamani wala gerezani, polisi au mahabusi wanapohitajika wakalimani hao, bali hata hospitalini kwenye hospitali za wilaya, mikoa, rufani na za kitaifa.

Mkalimani pia anahitajika kwenye ofisi nyingi zikiwamo za ustawi wa jamii, ofisi za wakuu wa mikoa na wilaya pia.

Kunahitajika wakalimani hao kwa kuwa serikali imeweka utaratibu wa kuwapatia mikopo vijana wanawake na watu wenye mahitaji kama wanaoishi na ulemavu ndiyo maana wakalimani wanahitajika.

Aidha, tunaona kuwa suala la wenye ulemavu kupewa kupewa kipaumbele kwenye miundombinu hasa lifti kwenye majengo ni la kuangaliwa kwa jicho la pili.

Tunaona kuwa hospitalini ni eneo muhimu la kuhakikisha kunakuwa na miundombinu rafiki kama lifti maalumu ya watu wenye ulemavu ili hata kama umeme unakatika kuwe na njia ya kuwahudumia.

Lakini mambo hayaishii hapo katika kutoa huduma ni dhahiri kuwa shuleni nako wenye ulemavu wanahitaji vyoo maalumu. Kwa hiyo juhudi zinapofanywa kujenga vyoo shuleni huko vijijini ni vyema kuwakumbuka watoto wenye ulemavu.

Miaka inavyokwenda ni wakati pia wa kujipanga ili kuwa na usafiri unaowasaidia watu wenye ulemavu. Kwa mfano, daladala muda mwingi hazijawa na mfumo wala namna ya kumhudumia mwenye uhitaji.


Licha ya mabasi ya mwendo wa haraka kutoa huduma hizo ni vizuri kuboresha huduma zaidi ili kuwasaidia Watanzania hawa ambao wana haki kama walivyo watu wengine wasio na upungufu wa kimaumbile.

Tunashauri kuwa ni vyema hata kwenye mabasi ya mikoani nako kukawa na maelekezo ya kuwasaidia wasafiri hawa. Suala la miundombinu rafiki na kuwa na wakalimani ni lipewe kipaumbele kwa kuwa si suala la kuomba tena bali ni haki ya wanaoishi na ulemavu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Coco Beach inaweza kuwa ya kisasa, ni kujifunza tu

Na Salome Kitomari

**NIMEPATA** bahati ya kutembelea fukwe mbalimbali za Afrika na Asia, na kujionea jinsi zilivyoendelezwa na kuwa za manufaa kwa wananchi wote bila kujali uwezo wa kifedha.

Mwaka 2016 nilitembelea mji wa Durban Afrika Kusini ambao ni maarufu kwa fukwe nzuri ambazo hutembelewa na watu wote.

Ni fukwe zinazomilikiwa na jiji hilo, huku wananchi wa kawaida wakipata fursa ya kuzitalii ikiwa ni pamoja na kuendesha shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa ajili ya ustawi wa maisha yao.

Zimejengwa kwa muundo rahisi na rafiki, zisizo na majengo makubwa. Zina maeneo ya kutembelea, kukaa, kulala kwa watu wanaotaka kupunga upepo.

Aidha, kuna njia nyingi zilizojengwa za kumuwezesha mtembeaji kuingia baharini kwa umbali wa mita 200 zikiwa kama barabara pana zenye taa za juu.

Ni eneo ambalo mtembeaji anaweza kuingia hadi umbali fulani wa bahari na kuona mawimbi makubwa ya maji yanavyoruka na kuanguka, pia na kupiga picha nyakati zote usiku na mchana.

Mbali na eneo la kupumzikia, mama lishe na wachuuzi wengine wanaendelea na biashara zao kama kawaida wakichagizwa na mabango mbalimbali yanayoelekeza sheria na taratibu za eneo hilo. Kwa ujumla utunzaji wa mazingira katika fukwe hii ni mkubwa yakinakishiwa kwa bustani zenye mandhari nzuri zinazowezeshwa na usafi wa mara kwa mara.

Aidha, nilipata fursa ya kutembelea fukwe za nchi ya Thailand, ambako nako kumejengwa maeneo ya vizimba vya kukalia na kulala kadri mtu anavyotaka mapumziko yake yawe.

Kuna njia za kutembea na bustani za kupiga picha, huku biashara tofauti zikiendelea katika eneo hilo.

Eneo ni la wazi kwa wananchi wote wenye kipato cha chini na cha juu wanaohitaji kupumzisha akili kwa kupunga upepo wa bahari. Nimeanza kueleza nilichokiona kwa wenzetu, nikijaribu kuvuta taswira ya kilichokuwa kimeandaliwa kujengwa kwenye eneo la fukwe ya Coco, baada ya Rais John Magufuli kutoridhishwa nacho.

Kabla ya Dk. Magufuli kueleza kwa kina suala la fukwe hiyo, alibainisha kusikitishwa kwake na kukwama kwa mradi huo na miradi mingine ya maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam.

Siku iliyofuata alionekana Meya wa Kinondoni na viongozi wengine wakitangaza kupatikana kwa mkandarasi na kwamba ujenzi ungeanza wakati wowote.

Rais alibainisha kushangazwa na miundombinu iliyopangwa kujengwa eneo hilo ambayo haitaendana na watu wa kawaida, wakati kukiwa vilevile na ujenzi wa barabara inayopita baharini inayoweza kuharibu miundombinu iliyopangwa kujengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 14.

Kwa jinsi Rais alivyoeleza na kutoa mfano wa fukwe za Jiji la Durban, inapatikana picha kwamba kulikuwa na umuhimu kwa wahusika kujifunza jinsi ya kuendeleza fukwe hizo na kunufaisha watu wote kutoka nchi zingine.

Jiji la Dar es Salaam halina fukwe iliyojengwa vyema ambayo wananchi wote wanaweza kuitembelea na kufurahia zaidi ya Coco beach, ambayo licha ya kuleta watu wengi kwa pamoja hakuridhishi kwa kukosa miundombinu bora na usafi usioridhisha.

Ilitarajiwa kuwa itajengwa miundombinu ya kawaida itakayojumuisha bustani mbalimbali, ili wananchi waliokuwa wakifanya biashara eneo hilo waendelee na biashara zao, huku kila anayetaka pa kupumzika na kupunga upepo wa bahari, apate huduma hiyo kirahisi. Kwa ujumla Jiji la Dar es Salaam limekosa maeneo ambayo wananchi wanaweza kutembea na kupunga upepo.

Unapotembelea majiji kama Nairobi nchini Kenya na mengine ya nchi za Magharibi, utaona bustani nzuri ambazo wananchi hutembelea kwa ajili ya kupunga upepo.

Lakini kwa jiji letu bustani kama hizo zimepotea kutokana na mabadiliko au kutotunzwa vyema, lakini lipo la kukosa maeneo ya kuegesha magari kwa wanaokwenda matembezini wakitamani kubeba wapendwa wao.

Muungwana anasema basi ni vyema Manispaa zikajenga fukwe ambazo ni rahisi na zenye kuvutia.

Zijifunze kutoka kwenye majiji mengine ambayo yameweza kujenga vitu kama hivyo.

HABARI KITAIFA

# Gari laweka vigogo kuti kavu kituo afya

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

WAKAZI wa Jimbo la Bunda mkoani Mara, wamelalamikia kitendo cha kuombwa fedha za kununua mafuta kwa ajili ya gari la wagonjwa, wanapohitaji huduma hiyo kuwapeleka wajawazito na wagonjwa wenye hali mbaya kwenye vituo vya kutolea huduma ya afya.

Wananchi hao walitoa kero hiyo kwa nyakati tofauti mbele ya Mbunge wa Bunda, Boniphace Mwita Getere, wakati akihutubia kwenye mikutano ya hadhara katika vijiji mbalimbali jimboni humo.

Walisema wajawazito na wagonjwa wenye hali mbaya wanapoomba gari la wagonjwa ili liwapeleke vituo vya kutolea huduma ya afya, dereva wa gari hilo amekuwa akiwaomba fedha kati ya Sh. 30,000 hadi Sh. 40,000, akidai ni lazima wachangie gharama za mafuta.

"Mheshimiwa mbunge, sisi wananchi tunataka kujua hiyo gali ya wagonjwa ni lazima tutoe pesa ndipo mgonjwa au mjamzito achukuliwe na kupelekwa hospitalini au ni vipi, maana dereva amekuwa akituomba kati ya Sh. 30,000 hadi Sh. 40,000, tena kwa nguvu," alisema Hamisi Saidi.

"Mimi niliambiwa nitoe Sh. 40,000 nilipogoma huyo dereva akataka kuondoka, ikanilazimu nitoe tu hizo hela ndipo alipokubali kumchukua mgonjwa wangu," alisema Mwasi Togoro.

Katika mikutano yote aliyohutubia mbunge huyo alikutana na kero hiyo ya wananchi kuombwa fedha za kuchangia mafuta katika gari hilo la wagonjwa.

Kufuatia hali hiyo, Getere alisema gari ya wagonjwa limeletwa kwa ajili ya kutoa huduma hiyo bure.

"Huduma ya gari ya wagonjwa ni bure na tulishasema sana, lakini naona kitendo hicho kinaendelea. Fedha za mafuta zinatolewa kwenye kituo cha afya siyo kuchangisha wananchi. Na leo hii nimemwambia mganga mkuu kwamba kama anataka kutumbuliwa atatumbuliwa," alisema Getere.

**Mheshimiwa mbunge, sisi wananchi tunataka kujua hiyo gali ya wagonjwa ni lazima tutoe pesa ndipo mgonjwa au mjamzito achukuliwe na kupelekwa hospitalini au ni vipi, maana dereva amekuwa akituomba kati ya Sh. 30,000 hadi Sh. 40,000, tena kwa nguvu.**

# Upelelezi kesi anayedaiwa kuua mke haujakamilika

**Na Hellen Mwango**

KESI ya mauaji inayomkabili mfanyabiashara Hamis Said (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe, Naomi Marijani, imepigwa kalenda baada ya Jamhuri kudai upelelezi wake bado haujakamilika na kwamba uko katika hatua za mwisho kukamilika.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon alitoa madai hayo jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Salum Ally.

Alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo upo katika hatua nzuri na za mwisho kukamilika na kwamba Jamhuri inaomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa tena Oktoba 7, mwaka huu.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa Mei 15, mwaka huu, katika oneo la Gezaulole, Kigamboni jijini Dar es Salaam, mtuhumiwa alimuua mtu anayeitwa Naomi Marajani.

Mtuhumiwa anadaiwa kumuua mke wake Naomi kisha kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa na kuchukua majivu ya marehemu na kwenda kuyafukia shambani kwake.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, akipata maelezo kuhusu mitambo ya kuchakata mahindi na kusaga unga wa sembe kutoka kwa Mkuu wa Kikosi cha JKT Mlale, Kanali Absolomon Shausi, alipotembelea kukagua shughuli za kikosi hicho, wilayani Songea, Mkoa wa Ruvuma juzi. **PICHA: OWM**

# NBS yawatoa woga wanahabari

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) imewahakikishia waandishi wa habari kuwa kifungu cha 37(4) cha Sheria ya Takwimu 2015 hakina adhabu yoyote isipokuwa zipo za ujumla katika kifungu cha 37(3) cha sheria hiyo.

Kifungu cha 37(4) cha sheria hiyo kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2018, kilikuwa kinazuia mtu yeyote kutoa takwimu bila kuwa na kibali kutoka NBS, ambapo adhabu yake ilikuwa ni faini isiyopungua Sh. milioni 10 au kifungo cha miaka mitatu jela, lakini sheria hiyo imefanyiwa marekebisho tena mwaka 2019 na kufuta adhabu katika kifungu hicho.

Akizungumza katika semina ya wahariri na waandishi waandamizi wa vyombo vya habari nchini kuhusu masuala ya kitakwimu yakiwamo marekebisho ya sheria hiyo, Mwanasheria wa Ofisi hiyo, Oscar Mangula, aliwahakikishia waandishi kuwa kifungu cha 37(4) hakina adhabu yeyote na kuwataka kukusanya na kutoa takwimu kwa kuzingatia misingi na miongozo ya NBS.

"Kifungu cha 37(4) haipo adhabu yoyote isipokuwa kifungu cha 37(3) kimeainisha adhabu mbalimbali ikiwamo kinazuia mtu yeyote kujifanya ofisa wa takwimu, kukataa kujibu maswali unayoulizwa kuhusu utafiti na kuchana nyaraka ya utafiti ambapo kuna adhabu ya kifungo cha miezi sita jela au faini isiyopungua Sh. milioni moja," alisema.

Akifungua semina hiyo, Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, aliwatoa hofu waandishi kuhusu mabadiliko ya sheria hiyo kwa kuwa yana madhumuni mazuri husussan kwa karne ya 21.

"Kama mtakwimu wa serikali, naomba niwaambie msiwe na hofu kabisa mabadiliko ya marekebisho haya madhumuni yake ni mazuri sana, hususan kwa karne hii ya 21 ambayo kuna mabadiliko ya takwimu tunaita data revolution."

"Mabadiliko ya takwimu hayahitaji serikali peke yake au vyombo vya serikali peke yake kutoa takwimu la hasha, inahitaji vyombo vyote vitoe takwimu lakini takwimu hizi sasa zifuate taratibu zake na katika Umoja wa Mataifa chombo chetu kikubwa kile Commission (Tume) ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa imeelekeza huko kwamba ofisi ya takwimu duniani zote zihakikishe kwamba zinafanya kazi na vyombo vingine vyote," alisema.

Alisema kupanuliwa kwa wigo huo kukusanya, kuchambua, kuzisambaza takwimu kwa teknolojia ya kisasa ili kupatikane takwimu nyingi zaidi kwa ajili ya kufuatilia na kutathmini mipango ya maendeleo ya nchi.

Kadhalika, alisema mabadiliko ya sheria hiyo yameifanya nchi ya Argentina na kufanya mabadiliko ya sheria yao ya takwimu.

"Ukienda kuangalia mabadiliko ya sheria ya Argentina mambo mengi yaliyopo kwenye sheria ya Argentina na wametuletea hapa NBS tuwape maoni, mengi yaliyopo kule ni namna gani ya kutumia fursa za takwimu za kutoka katika asasi zisizo za kiraia kutoka sekta binafsi ili ziweze kusaidia takwimu za serikali ya Argentina na ndicho ambacho Tanzania tumefanya hivyo sio kitu kipya," alisema.

Aliwataka waandishi na wahariri kuwa mabalozi wazuri kwa kutangaza takwimu na namna ya kuzitumia, huku akisema kuwa katika maadhimisho ya siku ya takwimu kila mwaka kutakuwa na tuzo kwa mwandishi wa habari bora wa masuala ya takwimu.

Alieleza kuwa NBS ipo tayari kusaidia asasi za kiraia ili kuzalisha takwimu sahihi kwa kutumia miongozo na kanuni za ukusanyaji na uchakataji wa takwimu sahihi na pia itaendelea kuvijengea uwezo vyombo vya habari ili viweze kuelimisha umma kwa kutoa habari sahihi za kitakwimu.

Mkurugenzi wa Utawala, Fedha na Masoko, Daniel Andrew, alisema NBS inatambua umuhimu wa vyombo vya habari katika kuelimisha umma kuhusu masuala ya takwimu.

# IGP Sirro atema cheche

INATOKA UK. 2

Makamanda hao ni kutoka Dodoma, Mwanza, Katavi, Tabora na Mjini Magharibi ambapo kila mmoja alieleza changamoto na baadhi waliahidi mwishoni mwa mwezi huu zitakuwa zimekamilika. IGP Sirro pia alisema Jeshi la Polisi lilikuwa na changamoto ya upatikanaji wa sare kwa ajili ya askari wake na ilifikia mahali askari anamuuzia sare askari mwenzake.

**MWANGOSI, AKWILINA**

IGP Sirro aliwataka maofisa na makamanda hao kuhakikisha wanasimamia kanuni za jeshi hilo, akikumbusha changamoto zilizojitokeza katika kesi mbili za mauaji dhidi ya mwandishi wa habari Mwangosi na mwanafunzi wa Chuo cha Usafirishaji Dar es Salaam (NIT), Akwilina Akwilini, aliyepigwa risasi wakati wa maandamano ya wanaodaiwa wafuasi wa Chadema.

"Changamoto zilizojitokeza wakati ule lazima tuzibadilishe ziwe fursa, uchaguzi hauwezi kushusha thamani, ili uende vizuri lazima uwe na mpango mkakati wa kuzuia, kubaini na kupambana na wahalifu.

"Hizi kesi zilizojitokeza za Akwilina na Mwangosi, kwanini zilitokea? Utaona changamoto kubwa ni amri, amri ikiwa 'weak' (dhaifu), hayo yanatokea.

"Kwa mfano, lililotokea Kinondoni (Akwilina), siwezi kusema lakini wote ni mashahidi, hatuwezi kusema, kuna mahali ambako sisi kama Jeshi la Polisi hatukutimiza wajibu wetu," IGP Sirro alisema.

Alitaja changamoto za utendaji ndani ya jeshi hilo na kutaka kuundiwa mikakati ya kutafuta majawabu ya pamoja kuwa ni pamoja na mmomonyoko wa maadili, nidhamu na miiko kwa baadhi ya maofisa wa polisi na uhaba wa askari.

Alisema changamoto nyingine ni kuzorota kwa mafunzo ndani ya jeshi hilo, akieleza kuwa amekuwa akiona askari anakwenda kwenye tukio na kurusha mambo ya ovyo mtandaoni.

"Unasimamia sheria halafu unavunja sheria maana yake ni nini? Lazima kamanda akae kwenye mabaraza yake, kamanda una makachero pale, kuna shida gani kwa mwezi ukafanya tathmini ya hao makachero wako ili ujue amepeleleza kesi ngapi, changamoto ni zipi na mafanikio?

"Nani anafanya hivyo, utajuaje utendaji kazi bila kufanya tathmini, kunatendeka makosa ya kimtandao lakini watu hawajui kabisa," alisema.



Meneja Mkuu wa Kampuni ya Usambazaji ya Route Pro, Duane Edwards (kulia), akimkabidhi Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, pikipiki 30 kwa ajili ya kutumiwa na vijana kuwawezesha kushirikiana na kampuni hiyo katika biashara ya usambazaji mikoa mbalimbali katika hafla ilifanyika jijini Dodoma jana. Nyuma ni baadhi ya wanufaika wa msaada huo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaridhia kufuta mapori

INATOKA UK.4

ya shughuli za makazi, kilimo na mifugo ili kuwaondolea kero za uhaba wa ardhi.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu amesema serikali imeridhia kumega hifadhi za misitu 14 kwa ajili ya kilimo na mifugo na kufuta mashamba 16 yasiyoendelezwa ili yapangiwe matumizi ya kilimo na mifugo.

"Vijiji 55 vilivyobaki vinaendelea kufanyiwa tathmini ya kina maeneo yaliyobaki ndani ya hifadhi na kuwasilisha mapendekezo yake kwa ajili ya uamuzi. Uchambuzi na taarifa itatolewa," alisema na kuongeza kuwa orodha ya maeneo ya vijiji, mapori ya wanyama, misitu na mashamba yaliyofutwa itatangwa baadaye.

Pia alisema baraza limeamua ardhi ya mita 500 zilizotengwa kama buffer zone (eneo kinga) kwenye maeneo ya vijiji vinavyopakana na hifadhi za wanyama ziachiwe vijiji husika na wananchi wasiondolewe kwenye maeneo hayo.

Aliyataja maamuzi mengine yaliyofikiwa kwenye kikao hicho kuwa ni Ofisi ya Makamu wa Rais imetakiwa ikamilishe mwongozo utakaobainisha matumizi ya ardhi ndani ya hifadhi ya mita 60 za mito, vyanzo vya maji, maziwa na bahari.

Maamuzi mengine ni kuzitaka wizara na taasisi zote za serikali zilinde maeneo yao kwa kuweka alama za kudumu zinazoonekana; na kwamba wananchi hawaruhusiwi kuvamia maeneo mapya na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya uvamizi wowote kuanzia juzi.

Januari, mwaka huu, Rais Magufuli alitoa maagizo kwa mawaziri wanane wa sekta zinazohusika na matumizi ya ardhi wachambue na kuandaa taarifa ya mapendekezo ya kutatua migogoro ya matumizi ya ardhi nchini.

Maagizo hayo yalikuwa ni pamoja na: Kutoviondoa vijiji na vitongoji 366 vilivyomo ndani ya hifadhi; Kubainisha maeneo ya hifadhi ambayo yamepoteza sifa ili yaweze kugawiwa kwa wananchi kwa shughuli za ufugaji na kilimo na kuhakiki za misitu, wanyama na makazi.

Mengine ni kumega baadhi ya hifadhi za taifa, mapori tengefu na misitu, kugawia wafugaji na wakulima; Kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazohusiana na matumizi ya ardhi; Kupitia upya sheria ya vyanzo vya maji inayozungumzia uhifadhi ndani ya mita 60; Kuwasilisha mapendekezo ya kufutwa mashamba yasiyoendelezwa na kugawa kwa wananchi kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo na kuendelea kulinda na kuhifadhi maeneo ya hifadhi za misitu, wanyamapori na vyanzo vya maji.

# Kairuki aipa TIC siku 7 kwenda Ruvuma

INATOKA UK. 3

"Naelewa kuwa ipo miradi mingi iliyofikiwa na TIC zaidi ya asilimia 72 hivyo niwatake mfike haraka mkoani Ruvuma hususan katika viwanda hivi vya kahawa, ili kuvitambua na kueleza fursa na umuhimu wa kujisajili na taasisi hii ili kuendelea kuchangia na kuwa na tija zaidi katika uchumi wa nchi," alisisitiza.

Mkurugenzi wa sera mipango na utafiti wa TIC, Mafutah Bunini, alisema katika kuboresha utendaji wao wamefungua ofisi za kanda saba ili kuwafikia kwa urahisi wawekezaji wa ndani na kwamba wanatoa uzito sawa kwa wawekezaji wa ndani na nje.

"Viwango vya mitaji ya uwekezaji vinatofautiana kwa wawekezaji wa nje na ndani, wa ndani anatakiwa awe na mtaji wa Dola 100,000, lakini mwekezaji wa nje ni Dola 500, 000," alisema.

Naye Meneja wa kiwanda cha kutengeneza kahawa cha Wilaya ya Mbinga (MCCCO), amemhakikishia waziri kuwa wataendelea kuboresha mazingira mazuri ya wafanyakazi na kuongeza thamani ya bidhaa zao za kahawa na kuhakikisha jamii iliyowazunguka inanufaika na kiwanda hicho.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha kutengeneza kahawa cha DAE, Danistan Komba ambaye pia ni mkulima wa kahawa, alimpongeza waziri kwa kutembelea kiwandani hapo na kueleza changamoto za masoko ya kahawa na kuiomba serikali kuendelea kuwaangalia wawekezaji hao wazawa.

"Kipekee napongeza ujio wako, japo tunachangamoto ya masoko kwa kuzingatia kiwanda kina uwezo wa kuzalisha tani 36,000 kwa mwaka na kuuza katika baadhi ya nchi.

Alifafanua kuwa, pamoja na changamoto za uhaba wa soko, kiwanda kimekuwa kikishiriki katika maonyesho ya nchi zinazolima kahawa ikiwamo Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Ethiopia.

Mkuu wa Wilaya ya Mbinga Cosmas Nshenye alieleza kuwa, ziara hiyo imeleta chachu kwa wafanyabiashara na wawekezaji wazawa.

# Waziri atumbua mameneja maji

INATOKA UK. 4

vizuri na kuzifuta zisizo na uwezo wa kujiendesha.

Kuhusu jumuiya ya Msalaza, Aweso alisema haikuwa ikijiendesha kwa mijibu wa taratibu na kwamba kasoro zilizopo zimesababisha hasara ya mamilioni ya fedha za serikali.

Pamoja na kuivunja, pia aliagiza uongozi wake kuchunguzwa na kuchukua hatua kwa watakaobainika kuhusika.

Naibu Waziri Aweso yuko mkoani hapa kwa ziara ya kikazi na anatarajiwa kutembelea miradi mbalimbali ya maji na kutoa maelekezo ikiwamo kuchukua hatua stahiki katika miradi ambayo haijaleta tija licha ya kutumia fedha nyingi.

# RC Moro apokelewa na tukio wizi dawa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MKUU mpya wa Mkoa wa Morogoro, amepokelewa na tukio la dawa siku ya kwanza ya kuanza kazi.

Mbali na tukio hilo, mkuu huyo, Loata Ole Sanare, amewataka viongozi na watendaji wa ngazi mbalimbali katika Mkoa wa Morogoro kumsaidia Rais John Magufuli kukabiliana na kuzitatua kero na changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi wanyonge.

Pia amewataka na kujitafakari upya kila mmoja kwa nafasi yake kilichosababisha Rais akatengua uteuzi wa aliyekuwa Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Kebwe Stephen Kebwe.

Sanare alisema hayo baada ya kukabidhiwa rasmi nyenzo zikiwamo taarifa na nyaraka mbalimbali za mkoa kutoka kwa Kebwe Stephen, ambapo akawataka watendaji na viongozi hao kushirikiana na kuhakikisha anatambua kuwa yupo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi na sio vinginevyo.

Sanare alisema atakuwa tayari kuwahudumia wananchi ndani ya saa zote 24 kila siku katika nafasi hiyo.

**Kamanda wa Polisi Mkoa nakuagiza mtuhumiwa huyu atafutwe popote alipo na akamatwe, na sio yeye peke yake, hii lazima ni cheini.**

Alisema changamoto kubwa inayoonekana mbele yake na iliyotajwa hata na Rais ni migogoro ya ardhi inayohusisha wakulima na wafugaji, ambapo alisema licha ya yeye kutoka jamii ya wafugaji, hatakuwa mkuu wa mkoa wa jamii ya wafugaji, bali ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro ambao ni wa jamii ya Watanzania wote.

"Sitakuwa na simile kwa yeyote atakayevunja sheria na taratibu zilizopo, kama ni Masai kakosea, huwa tunajua pia namna zetu za kuwajibishana na kwenye hili la migogoro ya wakulima na wafugaji itabidi kwanza nijue tatizo ni nini, mbona zamani makundi yote yaliishi pamoja, kulikoni sasa hivi na kila mwenye haki atapata haki yake bila kujali kabila lake," alisema.

**WIZI WA DAWA**

Hata hivyo, wakati kikao hicho cha utambulisho na makabidhiano kikiendelea, Mkuu wa Wilaya ya Ulanga, Ngolo Malenya, alitoa taarifa ya tukio la wizi wa dawa katika hospitali ya wilaya yake, baada ya kukamatwa kwa maboksi zaidi ya 41 ya dawa za serikali yaliyokuwa yakisafirishwa kutoka Ulanga kwenye basi la abiria mali ya kampuni ya Al Saedy.

Aliyetuhumiwa kuhusika na wizi wa dawa hizo ni mtumishi wa hospitali ya wilaya wa maabara, aliyemtaja kwa jina la Albert Mahodanga, ambaye inadaiwa alipakiza maboksi hayo Ulanga na kuondoka na gari binafsi, hadi walipofuatilia na kulikamata gari hilo eneo la Mikumi wilayani Kilosa.

Alisema mtuhumiwa huyo hata hivyo hataweza kupatikana baada ya kutokomea kusikojulikana, hivyo kumtaka popote alipo kujisalimisha kwenye vyombo vya dola.

Sanare, alieleza kusikitishwa na vitendo hivyo vya wizi, hasa wakati huu ambapo serikali imeongeza kasi ya utoaji wa dawa za kutosha kwenye hospitali na vituo vya afya ili kuhakikisha maisha ya Watanzania yanakuwa salama.

"Kamanda wa Polisi Mkoa nakuagiza mtuhumiwa huyu atafutwe popote alipo na akamatwe, na sio yeye peke yake, hii lazima ni cheini, wapo walioona wakamwacha, waliomsaidia, wakamatwe watuhumiwa wote waliohusika katika wizi huu," alisema Sanare.

Naye Katibu Tawala Mpya wa Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, akawaomba watendaji na viongozi hao kuimarisha ushirikiano kwani hakuna jambo lolote jema linaloweza kufanikiwa bila ushirikiano.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Morogoro, Innocent Kalogores, aliwashauri watendaji na viongozi kutumia hotuba ya Rais wakati wa kuwaapisha wakuu hao wapya, kama dira tosha ya kufanya marekebisho ya utendaji wao wa kazi, na kumsisitiza Katibu Tawala wa Mkoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi kumsaidia mkuu mpya wa mkoa kufanikisha utendaji na usimamizi wa shughuli za maendeleo ya wananchi.

"Dk. Kebwe hajastaafishwa, amepumzishwa wakati bado ana nguvu na uwezo wa kuendelea kulitumikia taifa, ubadhirifu uliokuwapo kwenye ngazi mbalimbali za halmashauri ambao hata Waziri Mkuu aliupigia kelele, kusua sua kwa maendeleo, yote haya yamegeuka ni mzigo wa Mkuu wa Mkoa," alisema Kalogores na kuongeza:

"Amefanya mengi mazuri, lakini yapo kweli aliyoshindwa, na yote yalichangiwa na ninyi, badilikeni na mumsaidie Mkuu wa Mkoa."

## Bil. 1.5/- ujenzi Chuo cha Veta

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema serikali imetenga kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi (VETA) wilayani Kongwa, ambapo ujenzi wake unatarajiwa kuanza Oktoba mwaka huu.

Ndugai (pichani chini) alitoa kauli hiyo jana katika ziara ya Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Taifa, Jesca Mbogo, wilayani humo.

Alisema kujengwa kwa chuo hicho kunalenga kuwaendeleza vijana kiufundi ili waweze kujiimarisha kiuchumi kutokana na Taifa kuelekea katika uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda.

Aidha, aliwataka wanawake kupambana ili kujiimarisha kiuchumi ili waweze kuendesha maisha yao ya kila siku.

"Wanawake ndiyo walioshika uchumi hivi sasa kuliko wanaume, pambaneni kuhakikisha familia haziyumbi," alisema Ndugai.

Aidha, Spika aliwataka kujikita katika kilimo cha korosho na kuhakikisha kila mwananchi anapanda mikorosho katika nyumba yake.

"Kilimo cha korosho ni muhimu na kinafaida sana, hivyo ni muhimu kila nyumba kuhakikisha watu wamepanda mikorosho kwa manufaa yao na familia zao," alisema Ndugai.

Pamoja na hayo, aliahidi kutafuta fedha kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kupata miche hiyo.



Aliwasisitiza kuendelea na ufugaji wa kuku na shughuli nyingine za kujiingizia kipato ili kuendelea kuimarika kiuchumi.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Fountain Gate Academy ya Tabata, jijini Dar es Salaam (kulia), wakitoa msaada wa vitu mbalimbali kwa watoto yatima wa vituo vya Yatima Group Trust Fund na Umra vya jijini humo jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Bashe aagiza bil. 4/- zirudishwe

**Na Hellen Mwango**

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ameiagiza Bodi ya Korosho Tanzania kuhakikisha Kampuni ya Bajuta inayojihusisha na biashara ya mbolea na viuatilifu kurudisha Sh. bilioni 4.5 kati ya Sh. bilioni 10 zilizotolewa na bodi hiyo kinyume cha sheria.

Kadhalika ameagiza wakaguzi kutoka Hazina kuchunguza viongozi wote waliobadilisha matumizi ya Sh. bilioni 10 zilizoelekezwa kwenda Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC) kuchukuliwa mara moja.

Naibu Waziri Bashe aliyasema hayo katika ziara yake ya kukagua kontena zaidi ya 350 za mbolea na viuatilifu yaliyopo katika bandari kavu tatu ikiwamo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na Azam za jijini Dar es Salaam.

"Bodi ya Korosho imeilipa Kampuni ya Bajuta Sh. bilioni 4.5, pia ikaiagiza mbolea na viuatilifu vya Sh. bilioni 4.5 nyingine kinyume cha makubaliano na serikali wakati fedha hizo zilitolewa kwa TFC ili iweze kusambaza mbolea na dawa hizo kwa wakulima kwa bei nafuu," alisema.

"Rais John Magufuli alipotoa fedha hizo kwenda TFC alikusudia wakulima wapate unafuu wa mbolea na viuatilifu ili kuwaboreshea kilimo chao, nasisitiza kwamba Kampuni ya Bajuta irudishe Sh. bilioni 4.5 mali ya serikali," alisema Bashe.

Akifafanua alisema TFC ilipewa jukumu la kuagiza mbolea na dawa aina ya Salfa ili iweze kuuzwa kwa wakulima kwa bei nafuu, lakini ilipokea Sh. bilioni moja kati ya 10 iliyotolewa na Hazina na hivyo bodi hiyo kuwakwamisha kutimiza malengo ya serikali.

Alisema mwaka mmoja sasa TFC, bandari kavu hizo zinashikilia kontena zaidi ya 350 zenye mbolea na Salfa.

HABARI KITAIFA

# India kufadhili masomo kwa Watanzania 400

Na Elizabeth Zaya

UBALOZI wa India umesema unatarajia kuwafadhili Watanzania zaidi ya 400 kwa kuwapeleka nchini humo kuwapatia ujuzi katika nyanja mbalimbali ikiwamo za kilimo, afya, elimu na nyinginezo.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Balozi wa India nchini, Sanjiv Kohli, katika hafla iliyoandaliwa na ubalozi huo na Kituo cha Umahiri wa Teknolojia ya Habari kinachoshirikisha India na Tanzania (ITEC)kwa ajili ya kuwakutanisha wafanyakazi na wanafunzi waliowahi kufadhiliwa kwenda kusoma nchini humo.

Balozi Kohli alisema lengo ni kuendelea kudumisha ushirikiano uliopo kati ya nchi hizo mbili.

Balozi Kohli alisema India itaendelea kushirikiana na Tanzania katika mambo mbalimbali, na kwamba sehemu nyingine ambayo wamekubaliana kushirikiana ni katika eneo la Tehama.

**India imekuwa msaada mkubwa katika maeneo mbalimbali hususan katika sekta ya elimu, Tehama, na uwekezaji wa viwanda vikubwa na vidogo.**

"Kwa kipindi kirefu sana tumekuwa tukishirikiana na Tanzania katika mambo mengi na kila mwaka tumekuwa tukichukua watu kuwapeleka India kwa ajili ya kwenda kujifunza mambo mbalimbali katika sekta tofauti tofauti, na mwaka huu tunapanga kuchukuza watu karibu 500," alisema Balozi Kohli.

Mkuu wa Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Prof. Preksedia Ndomba, alisema kwa sasa nchi hizo mbili zimekubaliana kushirikiana katika sekta ya afya.

Prof. Ndomba alisema wamekubaliana kwamba Watanzania kwa sasa watakuwa na uwezo wa kupatiwa matibabu kwa kuonana na daktari kwa njia ya mtandao (tiba mtandao).

Alisema katika mpango huo watakuwa wanashirikiana na hospitali zote za rufani nchini kwa ajili ya kufanikisha wagonjwa wanaohitaji kuonana na madaktari wa India kufanya hivyo.

"Kwa kushirikiana na ubalozi wa India tumeshakamilisha mchakato huo na tumeanza kwa majaribio kwanza," alisema Prof. Ndombo.

"Tunafahamu kwamba Watanzania wengi wamekuwa wakienda India kwa ajili ya matibabu, lakini kupitia mpango huu wa tiba mtandao, watakuwa na uwezo wa kuonana na daktari uso kwa uso na haya yote yatafanyika kwa ushirikiano wa sisi DIT, Ubalozi wa India kupitia hospitali zetu za rufani nchi nzima," alisema Prof. Ndombo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, alisema India imekuwa msaada mkubwa katika maeneo mbalimbali hususan katika sekta ya elimu, Tehama, na uwekezaji wa viwanda vikubwa na vidogo.



Viongozi wa Kanisa la Mennonite Tanzania (KMT) na baadhi ya wakazi wa mji wa Musoma mkoani Mara, wakiwa kwenye ufunguzi wa ofisi za kanisa hilo, katika eneo la Nyabange, juzi, ambapo walitangaza utoaji wa mikopo kwa vikundi vya ujasiriamali vya mjini humo, kupitia taasisi ya Jamii Impact Ltd. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Shahidi mpelelezi kikwazo kesi ubakaji

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KUTOKUWAPO kwa shahidi mpelelezi kunasababisha Mahakama ya Mkoa Chakechake kuiahirisha kesi ya ubakaji inayomkabili mtuhumiwa Mussa Juma Othman (19), mkaazi wa Michakaeni Chakechake Mkoa wa Kusini Pemba.

Baada ya mtuhumiwa kuitwa jina lake mahakamani hapo, ndipo Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Seif Mohamed Khamis, alipodai shauri hilo lipo kwa ajili ya kusikilizwa ingawa shahidi ambaye ni mpelelezi hayupo.

Alidai shahidi huyo aliondoka kwenda kwenye mafunzo, ambapo anatarajia kurudi mwishoni mwa Septemba ama mwanzoni mwa Oktoba mwaka huu, hivyo aliiomba mahakama kuliahirisha shauri hilo hadi tarehe nyingine kwa ajili ya kusikilizwa.

"Mheshimiwa hakimu, shauri hili lipo kwa ajili ya kusikilizwa, lakini shahidi wetu ambaye ni mpelelezi alikwenda kwenye mafunzo, tunategemea kurudi hivi karibuni," alidai.

Wakili wa upande wa mshtakiwa, Abeid, alidai shauri hilo ni la muda mrefu sasa halijamaliza kusikilizwa mashahidi, na kuiomba mahakama kulifuta shauri hilo, kwani upande wa mashtaka hauna sababu za msingi.

"Upande wa mashtaka umekuwa ukiliburuza shauri hili, kinyume cha miongozo, hivyo tunaiomba mahakama yako kuliondosha shauri hili, ili mtuhumiwa akaendelee na majukumu yake mengine," alidai wakili huyo.

Hakimu Luciano Makoye Nyengo baada ya kusikiliza hoja za pande zote mbili, alitoa nafasi ya mwisho kwa upande wa mashtaka kuwasilisha mashahidi mahakamani hapo.

Alisema shauri hilo litarudi tena mahakamani Oktoba 3, mwaka huu kwa ajili ya kusikilizwa sambamba na kusisitiza kuitwa kwa mashahidi.

Ilidaiwa mahakamni kuwa, mtuhumiwa alitenda kosa siku isiyofahamika Desemba 2017 Michakaeni Chakechake, bila ya halali alimbaka mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 17, jambo ambalo ni kosa kisheria.

# Chanjo mpya kuku, ng'ombe

**Na Boniface Gideon,** TANGA

TAASISI ya chanjo ya mifugo Tanzania iliyopo mkoani Pwani imegundua aina tano za chanjo ya mifugo ya ngombe na kuku ambao wamekuwa wakikumbwa na magonjwa mbalimbali na kusababisha vifo.

Hali hiyo imekuwa ikiwasababishia hasara wafugaji, hivyo kuzikimbilia chanjo hizo licha ya ubora na gharama yake kuwa nafuu.

Chanjo hizo ni mbadala kwa wafugaji kwani mifugo yao imekuwa ikisumbuliwa mara kwa mara magonjwa na itawasaidia wafugaji kuondokana na hasara wanayokumbana nayo, pia kupoteza ubora wa mazao ya mifugo yao.

Akizungumza wakati wa mafunzo ya uandishi wa habari za kisayansi kati ya watafiti na waandishi wa habari wa mikoa ya Tanga, Pwani na Morogoro yaliyofanyika jijini Tanga yaliyoratibiwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), Meneja wa Wakala wa Maabara za Vetinari (TVLA) mkoani Tanga, Dk. Imna Malele, alisema katika Mkoa wa Tanga chanjo hizo zimeleta tija na matokeo makubwa kwa wafugaji.

Dk. Malele alisema awali wafugaji wengi walikuwa wanapata hasara na mifugo yao mingi kufa kutokana na chanjo hizo nyingi zilikuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi, hivyo wakawa wanashindwa kumudu gharama zake.

Ameeleza katika wilaya mbalimbali za Mkoa wa Tanga hasa maeneo ya wafugaji wa ng'ombe, walikuwa wanasumbuliwa na magonjwa ya homa ya mapafu, chambavu, kimeta na ugonjwa wa kutupa mimba, tishio ambalo hivi sasa wanaweza kuliepuka.

Chanjo hizo ni CBPP ya homa ya mapafu ya ng'ombe, S-19 Brucellosis kwa ajili ya ugonjwa wa ng'ombe kutupa mimba, chanjo ya ugonjwa wa kimeta (anthrax), ugonjwa wa ng'ombe wa chambavu (BQ) na ya ugonjwa wa kideri cha kuku.

Dk. Malele alisema Wakala wa Maabara za Vetinari nchini kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo ya Kenya wamegundua kemikali zenye harufu ya mnyama aina ya kuro ambaye harufu yake inafukuza wadudu wasumbufu kwa ng'ombe aina ya mbung'o.

Alisema harufu hiyo watawekewa ng'ombe kwenye kifaa maalum watakachofungwa nacho sikioni ili akijitikisa inamsaidia kusambaza harufu hiyo ya kemikali ambayo inafukuza mbung'o na sasa wapo katika hatua za kusajili.

Mmoja wa wafugaji anayejishughulisha na shughuli za kilimo na mifugo ambaye ana shamba la mifugo ya kuku na ng'ombe wa maziwa, alisema mifugo yake ilikuwa inasumbuliwa na maradhi ambapo alikuwa anaagiza chanjo na dawa za mifugo kutoka Uholanzi na Denmark.



# Waombwa kuchangia damu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAKAZI wa Mkoa wa Arusha wametakiwa kujenga utamaduni wa kujitolea damu ili kutatua tatizo la upungufu wa damu salama, katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha, Mount Meru.

Ombi hilo lilitolewa jana na Mratibu wa Damu Salama Jiji la Arusha, Anna Meena, kwa niaba ya Mratibu wa Damu Salama Mkoa wa Arusha, wakati

wa kuchangia damu salama, zoezi lililoandaliwa na taasisi ya kijamii ya Who Is Hussain.

Anna alisema katika hospitali hiyo, kuna uhitaji mkubwa wa damu salama, hivyo wananchi wanapaswa kujiwekea utamaduni wa kuchangia ili kupunguza tatizo la uhitaji wa damu lililopo katika hosipitali hiyo.

"Uhitaji wa damu ni mkubwa kutokana na matumizi yake kuongezeka siku hadi siku, na hii inatokana na matukio mbalimbali yanayotokea kwenye jamii ikiwamo ajali za mara kwa mara," alisema.

Alisema katika uchangiaji wa damu walikuwa na matarajio ya kupata watu 100, lakini walipata watu 80, na matarajio yalikuwa kukusanya chupa 60, lakini zilizopatikana zilikuwa 40.

Mwakilishi na Mkurugenzi wa taasisi hiyo Mkoa wa Arusha, Tahera Abbas, alisema waliandaa hafla hiyo kwa lengo la kuokoa uhai wa watu wanaopoteza maisha kwa kukosa damu.

Alisema kila mara taasisi hiyo, imekuwa ikiitembelea Hospitali ya Mount Meru na wamekuwa wakiambiwa kuwa bado kuna changamoto ya uhitaji wa damu salama hospitalini hapo.

"Tulikuja na wazo hili kutokana na watu kupoteza maisha kwa magonjwa mbalimbali, ajali pamoja na kukosekana kwa damu," alisema Tahera.

Alisema binadamu wanatakiwa kusaidiana bila kujali uwezo wa mtu, sura, dini, kabila na rangi katika suala la kuchangia damu ili kuokoa maisha ya Watanzania wenye uhitaji.

Hata hivyo, alisema Agosti 9, mwaka huu taasisi hiyo, kwa kushirikiana na taasisi ya KICJ, waliendesha uchangiaji wa damu na kupata uniti 55, zilizopelekwa Hospitali ya Mount Meru.

"Tunatarajia kukusanya damu nyingi zaidi, kila uniti moja ya damu itasaidia kuokoa uhai wa watu watatu," alisema Tahera.

# Wasimamizi uchaguzi Longido wafundwa

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WASIMAMIZI wa uchaguzi wa serikali za mitaa Wilaya ya Longido mkoani Arusha, wametakiwa kusimamia uchaguzi huo kwa weledi, uadilifu na ufanisi, ili ukamilike kwa wakati.

Akizungumza jana wilayani hapa wakati akitoa maelekezo ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, msimamizi wa uchaguzi serikali za mitaa ambaye ni Ofisa Elimu Msingi, Natanagwak Mollel, alisema uchaguzi huo ni wa kitaifa na unatambulika kisheria.

Alisema ni vyema kila mmoja atakayesimamia akatanguliza mbele weledi na uadilifu na amani, sababu kuna maisha baada ya uchaguzi.

"Katika wilaya yetu hii ina vitongoji 176 na vijiji 49, hivyo sio kazi ndogo, hakikisheni kila kitu kinaenda sawa na uchaguzi ukamilike kwa wakati uliopangwa," alisema.

Natanagwak, aliwataka wakazingatie kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa kanuni ya 9(1) ambayo inamtaka msimamizi kutoa maelekezo ya uchaguzi siku 62 kabla ya uchaguzi na kutangaza siku ya kufanyika.

Alisema kwa wilaya hiyo Oktoba 29, itakuwa siku ya kugawa fomu kwa wagombea wote wenye sifa, kuanzia wenye umri wa miaka 21 na kuendelea na fomu hizi zitapatikana kwenye ofisi ya msimamizi wa uchaguzi, msimamizi msaidizi wa uchaguzi ngazi ya kata na vijiji.

**Fomu hizo zitatakiwa kurejeshwa Novemba 4, kabla ya saa 10:00 jioni, ambayo ni siku ya mwisho wa kurejesha fomu, baada ya hapo ni marufuku msimamizi kupokea fomu nje ya muda huo.**

"Fomu hizo zitatakiwa kurejeshwa Novemba 4, kabla ya saa 10:00 jioni, ambayo ni siku ya mwisho wa kurejesha fomu, baada ya hapo ni marufuku msimamizi kupokea fomu nje ya muda huo," alisisitiza Mollel.

Alisema, baada ya kurejesha fomu uteuzi wa wagombea utafanyika Novemba 5, na msimamizi wa uchaguzi atabandika majina ya wagombea walioteuliwa na wenye sifa za kuwania nafasi hizo.

"Kama kuna mgombea hajaridhika na uteuzi, kuna muda wa kuweka pingamizi dhidi ya uteuzi ambao ni Novemba 5 hadi 6 mwaka, 2019 au anayepinga uteuzi kuhusu mtu yeyote anayeweza kuwasilisha pingamizi na kumwomba msimamizi msaidizi wa uchaguzi kupitia upya," alieleza Mollel.

Alisema kuwa siku ya kusikiliza rufani itakuwa Novemba 5 hadi 8 chini ya mwongozo wa kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019.

Alisema mikutano ya kampeni za uchaguzi itaanza Novemba 17 hadi 23, mwaka huu na zitafanyika ndani ya siku saba na kila chama kitakachoshiriki uchaguzi kitawasilisha ratiba yake ya mikutano ya kampeni kwa msimamizi wa uchaguzi siku saba kabla ya mikutano kuanza.

Samweli Mollel, mkazi wa Longido, alidai katika uchaguzi wa 2014 baadhi ya raia wa Kenya walipiga kura Tanzania na kusababisha mgongano na uvunjifu wa amani kwa wananchi na viongozi waliojitokeza kuwania nafasi hizo.

Naye Mtendaji wa Kata ya Namange, Nevely Mungaya, alisema, kata hiyo ipo mpakani na nchi jirani ya Kenya na mwingiliano ni mkubwa, lakini wamejipanga vizuri kuhakikisha wapigakura watakuwa ni wazaliwa wa Tanzania.

Alisema kila kitongoji wananchi watajiandikisha na majina yatabandikwa kwenye ubao mbalimbali za matangazo na wananchi watapewa uhuru wa kutoa taarifa kama kuna raia wa nchi nyingine ameingilia uchaguzi huo.

Kiongozi wa mila Philipo Kilaye, aliyeshiriki mkutano huo, alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya watu wanaohitaji nafasi za uongozi kuwanunulia kadi wananchi ili wawachague, hivyo hawataki mwaka huu lijirudie hilo.



Ofisa Elimu ya Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Silvanus Tairo, akielezea mikakati ya elimu ya wilaya hiyo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mradi wasaidia wananchi milioni 13/-

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

MRADI wa 'Two mountains lodge Ltd' umetoa msaada wa Sh. milioni 13.5, kuchangia miradi mbalimbali ya huduma za kijamii na maendeleo kwa wakazi wa Kijiji cha Ngorika, Kata ya Nkoaranga wilayani Arumeru, ili kuunga mkono juhudi za serikali za kuwaletea wananchi maendeleo na kufikia uchumi wa kati.

Akizungumza jana na Nipashe kwenye ofisi za mradi huo, mshauri wa mradi huo, Laisser ole Mattasia, alisema kampuni hiyo ilitoa mchango huo kuanzia mwaka 2014 ulipoanza kutekelezwa hadi 2019 kwa nyakati tofauti.

Alisema mradi huo umegharimu Sh. bilioni 3.5 hadi kukamilika, kwa hatua ya kutoa huduma, ulitumia Sh. milioni 1.5 kujenga kisima cha kuhifadhia maji, kwenye eneo la Lodge ambalo wanakijiji cha Ngorika hupata huduma ya maji.

"Vile vile, tumetumia Sh. milioni 10 kukarabati barabara yenye urefu wa kilomita 1.4 inayokatiza kijijini hapa, kwa kiwango cha kuweka vifusi na wananchi kuondokana na barabara mbaya iliyokuwa haipitiki hasa wakati wa masika," alisema.

Alisema kwa sasa wakulima wanasafirisha mazao yao kama mboga na ndizi kwa urahisi kupeleka sokoni.

Hata hivyo, wameiomba serikali kuiboresha kwa kiwango cha changarawe na hata lami.

Alisema mradi huo umechangia Sh. milioni mbili kwa ajili ya ukarabati wa chumba cha kuhifadhia maiti kwenye Hospitali ya Nkoaranga, eneo lililopo karibu na mradi huo na kuwasaidia wakazi kuondokana na gharama za usafiri kupeleka miili ya ndugu zao katika Hospitali ya Mount Meru.

Ole Mattasia, alisema mradi huo wenye vyumba 34 vya kulaza wageni, umetekelezwa na kugharamiwa na Watanzania wazawa toka wilayani hapo akiwamo Dk. Ndosi, ambaye alishastaafu kazi nchini na kwenda kufanya kazi nchini Botwsana.

# Waitaka LATRA iwaondolee kero

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WANANCHI wamelalamikia gharama kubwa za usafiri wa daladala kati ya mji wa Moshi kwenda Kijiji cha Mkalama wilayani Hai, wakiiomba Mamlaka ya Usafiri Nchi Kavu (Latra) kuingilia kati ili kuondoa usumbufu huo.

Baadhi ya wakazi wa kijiji hicho walitoa malalamiko hayo jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika kujadili mambo mbalimbali likiwamo tatizo la usafiri.

Kutokana na hali hiyo, wameiomba Latra mkoani Kilimanjaro kuhakikisha magari ya abiria kutoka Moshi kwenda Mkalama na Longoi yanapunguza nauli ili kuwapa unafuu wateja wa vyombo hivyo.

"Kama Latra hawataziangalia upya bei zinazotozwa na mabasi yanayotoa huduma za usafiri kati ya Moshi na Mkalama pamoja na Longoi, sisi tutakwenda kuwashtaki kwa Mkuu wa Mkoa kumweleza kilio chetu," alisema Joseph Nzomo.

**Ni maajabu kwa sababu kila gari linalofanya safari katika maeneo haya linakuwa na bei tofauti na wala hawaangalii umbali. Kimsingi hatutaki kila gari litoze nauli tofauti kila kukicha.**

Nzomo ambaye ni Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji hicho alisema wananchi wake wamechoshwa na changamoto hiyo na wanajipanga kuwaita viongozi wakuu wa serikali ngazi ya wilaya na mkoa kulishughulikia ndani ya siku saba, lasivyo watamwandikia barua Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kumlalamikia kuhusu tatizo hilo.

"Ni maajabu kwa sababu kila gari linalofanya safari katika maeneo haya linakuwa na bei tofauti na wala hawaangalii umbali. Kimsingi hatutaki kila gari litoze nauli tofauti kila kukicha," alieleza Nzomo.

Zaidi alieleza: "Utakuta nauli kutoka Moshi hadi Mkalama tunalipa hadi Sh. 2,500 jambo ambalo si haki, kwani kutoka Moshi hadi Mkalama ni kilometa 16. Tunataka Latra iliangalie hili kwa sababu tunalipa nauli ya kilometa 80 badala ya kilomita 16, jambo ambalo tunaona si haki tena ni kuwaumiza wananchi."

Alipotafutwa kuzungumzia malalamiko hayo, Meneja wa Latra Kilimanjaro, Jones Makwale, hakupatikana jana, licha ya simu yake kuita mara kadhaa.

Hata hivyo, Nipashe ilimtafuta Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya kutoa maelezo kuhusu malalamiko hayo na katika majibu yake alisema ofisi yake inafuatilia jambo hilo kuanzia sasa na itakapokamilisha itatoa mwongozo baada ya vyombo vya usalama kuchunguza malalamiko hayo.

Pamoja na mambo mengine, katika mkutano huo wananchi hao walimchagua Ridhiwan Kisumo kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wazee wa Kijiji cha Mkalama.

Baraza hilo litashughulika kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wazee ikiwamo suala la upatikanaji wa matibabu na kusuluhisha migogoro mbalimbali ya kijamii ikiwamo utatuzi wa migogoro ya ardhi.



Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, Shaban Ndendetu (kulia), akifanya usafi na vijana wenzake walioko kwenye kambi ya kuwajengea uzalendo na uhamasishaji wa kushiriki shughuli za maendeleo, wilayani humo jana. **NA MPIGA PICHA WETU**

# Vituo vya maji kadhaa vyakauka

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

VITUO vinne kati ya sita vinavyotoa huduma ya majisafi na salama kwa wananchi wa vitongoji vya Mbughuni na Mwasiti katika Halmashauri ya Wilaya ya Hai, havitoi maji na kusababisha kero kubwa kwa wateja wa huduma hiyo.

Kwa sasa wakazi wa vitongoji hivyo wanalazimika kutembea zaidi ya kilomita 10 kila siku kufuata huduma hiyo vijiji vya jirani.

Hali hiyo ilibainika jana, baada ya Nipashe kutembelea vitongoji hivyo kuzungumza na wananchi kuhusu adha ya maji namna inavyokwamisha shughuli za kiuchumi.

Mmoja wa wakazi wa vitongoji hivyo, Peter Massawe, alisema wanapokwenda kutafuta maji vijiji jirani huuziwa maji hayo ndoo tatu kwa Sh. 1,100.

Akieleza kuwa jambo hilo linawawia vigumu wanawake na watoto kushiriki kikamilifu shughuli za kiuchumi kutokana na kutumia muda mwingi kutafuta maji tena kwa bei kubwa.

Vitongoji hivyo vyenye uhaba wa maji vipo katika Kijiji cha Mkalama, Tarafa ya Masama Mbughuni.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Vitongoji cha Mbughuni, Vincent Chami, alisema licha ya jitihada za serikali kufikisha huduma ya maji katika kitongoji hicho vituo viwili au sehemu mbili, kati ya sita, ndivyo pekee vinavyotoa huduma ya maji.

Alisema tatizo la vituo vingine kutokutoa maji linatokana na nguvu ndogo ya maji kushindwa kusambaa katika vilula vyote.

Kutokana na changamoto hiyo, wameiomba Mamlaka ya Majisafi na Usafiri wa Mazingira (Muwsa) ambayo imepewa kazi ya kusambaza huduma Wilaya ya Hai, kulitazama tatizo hilo.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, gharama za nyaraka na vifaa vya kuomba kuunganishwa na huduma ya maji zimepandishwa ghafla kutoka Sh. 250,000 hadi Sh. 290,000 jambo linalochangia wananchi wengi kushindwa kuunganishwa na mtandao wa huduma hiyo.

# Manispaa yatangaza kudhibiti ujenzi holela

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

UJENZI wa makazi holela hasa katika vijiji vinavyopakana na Manispaa ya Moshi, unaelezwa kuwa ni moja ya changamoto kubwa zinazoikabili Idara ya Mipango Miji kuzuia ongezeko la makazi holela.

Ofisa Tarafa ya Moshi Magharibi, Sencia Lushino, alisema jana na kuongeza kuwa kasi ya ujenzi huo inatisha na kuna kila sababu ya serikali kupambana na hali hiyo.

Ili kuzuia ujenzi huo kuendelea, Lushino amewaagiza watendaji kata kuanza kuchukua hatua kwa kuzuia ujenzi holela wa makazi na nyumba za biashara.

Pia watendaji hao wameaswa kuisaidia serikali kukomesha vitendo vya uvamizi wa maeneo ya wazi katika sehemu nyingi za mji wa Moshi.

"Nia ya serikali ni kudhibiti ujenzi holela ili wananchi wawe na makazi bora yaliyopimwa. Lakini pia kuondoa ama kumaliza migogoro ya ardhi. Sasa hivi kila eneo ambalo halijarasimishwa ni lazima lirasimishwe," alisema Lushino.

Kwa mujibu wa ofisa hiyo, watu wote waliovamia maeneo ya wazi na kuyaendeleza wanapaswa kulipia kodi katika Halmashauri ya Wilaya Moshi au Manispaa ya Moshi, kulingana na eneo alipo.

"Kuna maeneo mengi ya wazi yamevamiwa na baadhi ya wafanyabiashara na kuzitumia sehemu hizo bila kuzilipia kodi na hawa tusiwafumbie macho, kwa sababu serikali inapoteza mapato," alisisitiza.

Aidha, alisema hatua hiyo itaisaidia serikali kuongeza makusanyo ya mapato yake kwa kutoa vibali halali vya ujenzi.

Aliwaambia kuwa anataka watendaji wote kuhakikisha wanatoa huduma kwa wananchi bila upendeleo na kuhakikisha wananchi wanachanga michango ya chakula cha watoto ili waweze kupata chakula cha kutosha mchana shuleni.

Ukurasa 18



Chuki kwa wageni zaathiri heshima ya Afrika Kusini

## Kura ya mapema kisheria, mitazamo tofauti Zanzibar



Ukurasa 14

## Kimataifa



## Dunia yatathmini kuondoka Ikulu ya Trump kwa 'mwenye mustachi'

Ukurasa 20


# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 25, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




## Nyerere mrithi wa Marx mtangulizi kufikia Ujamaa

Ukurasa 15

# Chadema: Upinzani kurejesha wabunge wengi uchaguzi ujao- 2

- Ubabe unaoendelea ni sehemu ya siasa
- Sifa mgombea Chadema serikali za mitaa ni uadilifu
- Kesi ya Lissu imeonyesha Mahakama haziko huru nchini

**Na Enock Charles**

TANZANIA inatarajiwa kufanya uchaguzi wake wa Serikali za Mitaa, Novemba mwaka huu na uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani mwaka ujao.

Kwa hivi sasa vyama vya siasa viko katika maandalizi kwa ajili ya kuibuka na ushindi kwenye ngazi mbalimbali za chaguzi hizo.

Nipashe kupitia kwa mwandishi wake ilifanya mahojiano na Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Vicent Mashinji kuhusiana na mambo mbalimbali lakini zaidi chaguzi zijazo nchini. Wiki iliyopita tuliwaletea sehemu ya kwanza ya mahojiano hayo.

Tuliishia kwenye swali la uamuzi wa Mahakama kuhusu umbali wa mita 100 kutoka kwenye kituo cha kupigia kura ambapo Dk. Mashinji aliliweka vizuri. Sasa endelea na sehemu hii ya pili na ya mwisho ya mahojiano hayo:

**SWALI:** Kwa sasa Chadema ina wanachama wangapi?

**JIBU:** Bado hatujafanya tathmini ya nchi nzima, lakini si chini ya milioni sita na tumerecruit (sajili) wapya na sasa hivi tunamalizia ku-compile (kukusanya), au unataka kusema ile ya Polepole ya wanachama milioni 15? Ha ha ha, hizo ni hadithi za Alinacha.

**SWALI:** Ni lini umejiunga na Chadema?

**JIBU:** Mwaka 2011, lakini mimi nimekuwa ni mfuasi wa Chadema ila sikuwa mwanachama rasmi kutoka mwaka 1998.

**SWALI:** Ni changamoto zipi kubwa umekutana nazo toka ushike nafasi ya Ukatibu Mkuu wa Chadema?

Endelea 16



Katibu Mkuu wa Chadema, Dk. Vicent Mashinji.**PICHA: MTANDAO**

## Sakaya: Sina diwani Kaliua, lakini kazi inakwenda sawa

Ukurasa 19

# Kura ya mapema kisheria, mitazamo tofauti Zanzibar




Sehemu ya wapigakura kwenye Uchaguzi Mkuu Zanzibar. **PICHA: MTANDAO**

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

TUME ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) imefanya mabadiliko ya sheria na kuja na Sheria mpya ya Uchaguzi ya Mwaka 2018, ambayo tayari imeshatiwa saini na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein.

Katika sheria hiyo Kipengele cha 82 (1), kinaeleza kuwa ZEC itaweka utaratibu utakaoruhusu upigaji wa kura ya mapema ambayo itafanyika siku moja kabla ya siku ya upigaji kura, au siku nyingine yoyote kama itakavyoamuriwa na tume.

Sheria hiyo mpya imezusha mjadala mkubwa miongoni mwa wanasiasa huku baadhi yao wakiamini kuwa uwepo wa kura hiyo ya mapema, kunaweza kusababisha udanganyifu kwenye uchaguzi mkuu.

Wakati sheria hiyo ikiwa tayari imeshapitishwa ambayo ndani yake kutakuwa na kura ya mapema, baadhi ya watendaji wa ZEC wanatarajiwa kuzitembelea nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC).

Lengo ni kwenda kujifunza uendeshaji wa kura hiyo ya mapema ili iweze kutumika kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

Watazitembelea nchi za Botswana, Afrika Kusini, Zimbabwe na Namibia. Aidha, Serikali ya Zanzibar tayari kwa hivi sasa imo kwenye mchakato wa kutunga kanuni ili kuiwezesha sheria hiyo kutumika mwaka 2020 kwenye uchaguzi Mkuu kama ilivyokusudiwa.

**KURA YA MAPEMA NI NINI?**

Kura ya Mapema ni ile ambayo inapigwa siku moja kabla ya uchaguzi kwa lengo la kutumia haki ya kidemokrasia ya kuchagua viongozi akiwamo Rais wa Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani.

Kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar, wanatakaostahili kupiga kura hiyo ni wapigakura wanaotekeleza majukumu yao ya kikazi siku ya uchaguzi.

Hao ni pamoja na msimamizi wa uchaguzi, msimamizi msaidizi wa uchaguzi, msimamizi wa kituo, askari polisi na mjumbe au mtendaji wa tume.

Wengine ni mpigakura ambaye atahusika na kazi za ulinzi na usalama siku ya kupiga kura.

**TUME**

Mkurugenzi wa ZEC, Thabit Idarous, anasema kura hiyo itawahusisha watu waliotajwa katika sheria ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu siku ya uchaguzi.

"Tumegundua kuwa wasimamizi wa uchaguzi hasa wale wanaohusika na kazi ya ulinzi na usalama, wanakosa haki yao ya kupigakura kutokana na kutingwa na majukumu ya ulinzi siku ya uchaguzi," anasema.

Idarous anabainisha kwamba hatua hiyo ya kura ya mapema imetokana na Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Uchaguzi (ZEC) NO.4 ya mwaka 2018, ambayo inatoa nafasi kwa makundi hayo.

Anafafanua kuwa marekebisho hayo yamekuja baada ya kubainika kwamba wapiganaji wa vikosi vya ulinzi hawaitumii haki yao ya kidemokrasia kupigakura na kuwachagua viongozi kutokana na kutingwa na majukumu ya kazi siku ya kupigakura.

"Marekebisho hayo sasa yatawapa nafasi baadhi ya watendaji waliokabidhiwa majukumu muhimu kupigakura siku moja kabla ya uchaguzi mkuu kufanyika," anasema.

**KAZI LENGWA**

Mkurugenzi huyu anabainisha kuwa kazi kubwa inayokusudiwa kufanywa na ZEC ni kuanza kwa maandalizi ya kuandikisha wapigakura wapya pamoja na kufanya uhakiki katika Daftari la Kudumu la Wapigakura kwa ajili ya uchaguzi mkuu ujao.

Anasema kazi hizo ni muhimu kufanyika kabla ya uchaguzi mkuu kwa sababu wenye sifa hawawezi kupiga kura bila ya kusajiliwa katika Daftari la Kudumu la Wapigakura.

"Tunakusudia kuanza kuandikisha wapigakura wapya wenye sifa kwa ajili ya uchaguzi mkuu pamoja na kuhakiki Daftari la Kudumu la Wapigakura na kuondoa waliopoteza sifa, wakiwamo waliokufa," anasema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Kurugenzi wa Huduma za Uchaguzi wa ZEC, Idrisa Haji Jecha anasema kuwa kura hiyo itawahusisha askari na watendaji ambao watasimamia uchaguzi na wala si kwa askari wa jeshi lote kama inavyodhaniwa na baadhi ya wanasiasa.

Anasema upigaji kura huo utakuwa na utaratibu maalum ambapo askari au watendaji watakaosimamia uchaguzi watatakiwa kuiandikia barua tume hiyo mapema ili wapewe kipande maalum kitakachowatambulisha kupigakura hiyo.

Anabainisha kuwa askari au mtendaji yoyote atakayesimamia uchaguzi na akaomba nafasi hiyo, ataruhusiwa kwenda kupigakura katika kituo alichojiandikisha siku moja kabla ya uchaguzi.

"Naona hii kura ya mapema watu wameielewa vibaya, haitakuwa na udanganyifu wowote kwa sababu kabla ya uchaguzi, kutakuwa na orodha kamili ya watu wote watakaopigakura ya mapema na majina yao yatawekwa hadharani," anasema Jecha.

Anabainisha ZEC itakaa pamoja na wadau wa uchaguzi ili kuwapa elimu juu ya sheria hiyo kuwawezesha wakatoe elimu kwa wanachama wao.

**OFISA MWANDAMIZI**

Naye Ofisa Mwandamizi wa ZEC, Mbaraka Said Hassan anasema tume ipo kwenye mchakato wa kutayarisha kanuni zitakazoongoza na kuweka mfumo mzuri wa upigaji kura ya mapema kwa makundi yatakayoshiriki kwenye uchaguzi mkuu wa Zanzibar.

"Hivi sasa tume imeandaa jopo la watendaji wake watakaokwenda kujifunza katika nchi za SADC zenye mfumo huo wa kura ya mapema," anasema.

Anasisitiza lengo ni kujifunza namna ya utekelezaji mzuri wa kura ya mapema.

**WADAU**

Wakitoa maoni yao kuhusu kura ya mapema, baadhi ya wasiasa na wanaharakati wanasema nchi nyingi duniani zimekuwa na kura inayofanana na hiyo, hivyo iwapo sheria hiyo itatekelezwa vizuri hakutakuwa na tatizo.

Naibu Mkurugenzi Uchaguzi, Mipango na Uendeshaji wa chama Cha ADC, Juma Ali anasema sheria hiyo si mbaya iwapo itasimamiwa vizuri kuwezesha askari wanaosimamia uchaguzi kufanya kazi zao kwa ufanisi ili kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi.

"Tuna sheria nyingi na nzuri Zanzibar, lakini tatizo linakuja katika utekelezaji wake, hivyo nina imani sheria hii mpya ya uchaguzi itaweza kuepusha mitafaruku na migogoro, iwapo itatekelezwa kama ilivyokusudiwa," anasema.

Ali anasema iwapo sheria hiyo itatekelezwa vizuri, wananchi watapiga kura bila ya wasiwasi, kwani chaguzi nyingi zilizopita ziliambatana na vurugu na watu kutoaminiana.

Aidha, anabainisha kwamba viongozi wa vyama vya siasa wana wajibu wa kutoa elimu kwa wafuasi na wanachama wao kuhusu kura ya mapema ili waielewe vizuri sheria hiyo.

**MWANAHARAKATI**

Mwanaharakati wa masuala ya kijamii Dadi Kombo Maalim anasema hakuna haja ya kuwa na kura ya mapema, badala yake walioorodheshwa katika sheria ya uchaguzi kupiga kura hiyo watengewe muda siku yenyewe ya uchaguzi ili wapige kura.

Anasema kuwapo kwa kura hiyo ya mapema kutasababisha uchaguzi usiwe huru na haki, kwani uwepo wa sheria hiyo ni kutoheshimu mabadiliko ya 10 ya kuwepo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

"Sheria hiyo ya uchaguzi haina tija na mantiki yoyote kwa sababu huwezi kutengeneza sheria kwa kikundi cha watu fulani kwa fursa ya kupiga kura," anasema.

**ACT**

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Habari na Mawasiliano wa Chama cha ACT Wazalendo Salum Bimani, anasema hakubaliaani na kuwapo kura ya mapema kwani ni utaratibu ambao umelenga kuvuruga uchaguzi. Anasema utaratibu huo utasababisha kuingiza wapiga kura hewa kwa lengo la kukilinda chama tawala kiendelee kubaki madarakani.

Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Vuai Ali Vuai anasema kura ya mapema ni muhimu kwani itawapa haki wale ambao walioanishwa katika sheria hiyo kuweza kutumia haki yao ya kidemokrasi kuweza kupiga kura.

"Licha ya kwamba wamepewa dhamana ya kusimamia uchaguzi lakini nao wana haki ya kupiga kura, hivyo ni vyema wakapiga kura mapema ili kuweza kuendelea na majukumu yao," anasema.

# Nyerere mrithi wa Marx mtangulizi kufikia Ujamaa

**Na Miki Tasseni**

MABADILIKO katika nchi au dunia kwa jumla mara nyingine hufichwa katika yalipita, kiasi kwamba kwenda mbele, na hata kufanya mapinduzi ya kina, ni kama kurudi nyuma kuelekea maadili yaliyofahamika zamani, halafu yakasahaulika.

Ndiyo maana bingwa wa fikra ya mabadiliko duniani, Karl Marx wa Ujerumani, aliwahi kusema 'Hegel (bingwa mtangulizi wake kuelekea karne ya 19) anasema mahali fulani kuwa, watu mashuhuri wanatokea katika historia kana kwamba ni mara mbili.

Alisahau kuongeza, kwanza kama mkasa, na baadaye kama mzaha.'

Picha hii inakuja kichwani kwa sababu karibu kila miaka 20 katika nchi za Magharibi kuna wimbi jipya la kuunda fikra ya Marx kuhusu ubepari, kwani kimsingi hakuandika kuhusu Ujamaa ila kugusa tu kuwa utakuwa mfumo usio na harakati za kitabaka.

Kwa lugha ya sasa au taswira ya uchumi ya sasa, unaweza kusema ni mazingira ambako ushindani wa kimaisha wa kukata na shoka umeondolewa na jamii inaishi kwa misingi ya kina ya uelewano na kujali ustawi wa jamii yote kwa jumla.

Ilidhaniwa katika fikra ya kiliberali katikati ya karne iliyopita kuwa ongezeko la teknolojia lingeondoa misukumo, lakini imebaki na sasa maandamano hayaishi nchi za Magharibi, watu hawaridhiki na kilichopo, wanataka maisha bora.

Katika historia yote ya fikra ya siasa na uchumi hakuna mwandishi au mfikiriaji aliyewahi kuingia kwa kina katika fani takriban zote za masuala ya jamii kwa jumla kupata jawabu toshelezi la kile kilichopo kama Marx.

Alisaidiwa kupata sifa katika uhai wake kutokana na uhusiano wake na kundi la 'League of the Just,'enzi hizo wakiwa ni wanamapinduzi na si tu wachumia tumbo na kutoa makafara kupata utajiri, na ni kwa ajili yao aliandika kinachoitwa 'The Communist Manifesto.'

Ni kitabu kilichotabiri kuanguka kwa ubepari na kiliandikiwa hao hao waliokuwa na uhusiano wa karibu na vyama vya wafanyakazi na wanaharakati njozi kama ilivyo leo.

Kwa mujibu wa Profesa Sam Maghimbi wa Idara ya Sosholojia (utafiti jamii) ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, hayati Mwalimu Nyerere alikuwa mwanaharakati njozi wa kwanza duniani kuchukua madaraka ya nchi na kujaribu kwa vitendo na sera kamili kufikia njozi za uanaharakati huo.

Mijadala ilirindima kote duniani katika miaka ya 1980, nini kiliiwekea vikwazo kazi hiyo; ni mazingira ya uchumi wa kimataifa?

Ambacho kisingeweza kujadiliwa kwa kina ni kama mawazo yake yatarudi tena wakati ujao (mwa mfumo aliyousema Hegel na kuafikiwa na Marx) au tuseme suala hilo lilishamalizika.

Kujua kama fikra ya Mwalimu Nyerere imepitwa na wakati au la, lazima kwanza kutatua swali tangulizi kama fikra ya Marx imepitwa na wakati au la?



Mwalimu Julius Nyerere (mbele) akiwa katika moja ya matembezi ya kuunga mkono Azimio la Arusha.
**PICHA: MTANDAO**

Kuna makundi tofauti ya kiharakati bado yanapambanisha fikra mfumo huo wa Ujamaa utaboreshwaje, ili uendane na dhamira msingi ya fikra ya harakati katika historia, yaani masikini wasiachwe nyuma na ikiwezekana umasikini wenyewe ufutwe.

Swali linakuja ni katika mazingira gani maskini watalindwa wasishindwe katika mikondo ya maisha, na mfumo kama huo ni ubepari huo huo au Ujamaa upi hasa?

Suala ambalo si rahisi kuligundua ni kuwa taswira ya siku za mwisho ni pamoja na kutatuliwa kwa suala hilo, kuwa ni tatizo ambalo likitatuliwa kunakuwa na kitu kama hali mpya, ambayo Marx anasema ni 'kunyauka kwa mfumo wa dola.'

Ni kupoteza ukandamizaji wake ambao msingi wake ni hitilafu za kina katika uchumi na hivyo kuathiri utulivu na maelewano katika jamii kwa jumla, kutokana na mazingira kutokuwa bora, siyo tu kwa kuendelea kuwapo umaskini ila tofauti ya kina kati ya matazamio ya msingi kimaisha na hali halisi.

Ndiyo maana mahangaiko siyo ya nchi maskini peke yake bali ni dunia kwa jumla.

Inabidi kurudi katika suala la siku za mwisho kupata picha kamili, kwani waliotafsiri vipindi vya utabiri waligundua kunako miaka 1820 na kuendelea.

Baadhi wanadhani ndiyo 'kutwaliwa,' lakini hakuna jibu katika vitabu vya utabiri ila mkondo wa fikra, kwani mwaka 1844 ndiyo Marx alichapisha tungo ya kukinzana na fikra ya Hegel kuhusu haki, au sheria, na kwa njia hiyo, kufikia tafsiri tofauti ya historia kwa jumla.

Aliikataa dhana ya dini kutaka kutaabika duniani na kwenda mbinguni. Akabuni kaulimbiu ya ukombozi hapa duniani, kuwa paradiso si baada ya kufa, katu.

Kingine ambacho bado hakijafahamika ni kuwa kila hatua ya alichokiandika Marx ilipewa tukio kubwa katika karne iliyofuata, kuonyesha kuwa fikra ya Marx ni sehemu ya utatuzi wa mazingira yaliyopo, tofauti na ile ya katikati ya Karne ya 19.

Mojawapo ni changamoto ya teknolojia kuondoa hitaji la nguvukazi katika maeneo mengi na kuzagaa kwa vijana barabarani iwe ni nchi maskini au hata zilizoendelea kwa viwango tofauti.

Halafu kuna changamoto maalum ambazo zinatoka katika mpangilio wa kawaida wa masuala ya uchumi kuingia katika haki za binadamu, wanawake na watoto, utapiamlo na mtindio wa akili.

Alichoandika Marx mwaka 1844 kilionekana 1944 kwa kuundwa Benki ya Dunia (mfuko wa maendeleo wa kimataifa) na IMF (aina ya benki kuu ya dunia, kurekebisha mizania ya malipo hasa ya nje katika nchi wanachama).

IMF imeondoa uwezekano wa vita kati ya nchi moja na nyingine, kutokana na kudaiana na kulazimisha malipo tena ya riba kubwa kwa silaha, wakati Benki ya Dunia inatoa nyongeza kwa nchi wanachama, kwa kile wanachojipangia kwa miradi ya maendeleo, kusaidia kulinganisha maendeleo nchi na mabara tofauti.

Mwaka 1848 alichapisha kinachoitwa 'The Communist Manifesto' na mwaka 1948 ndiyo likatoka 'Tangazo la Ulimwengu la Haki za Binadamu' kuondoa kabisa manyanyaso ya kimfumo katika utawala.

Ni mwaka 1867 ambako Marx alichapisha 'Das Kapital' au kwa Kiingereza 'Capital,' yenye maelezo ya ziada 'Critical Analysis of Capitalist Production,' (mchanganuo kinzani wa uzalishaji wa kibepari).

Dhana muhimu ya Marx katika tungo hiyo ilikuwa ni 'kanuni ya mwelekeo wa viwango vya faida kupungua,' hadi ifikie mahali uzalishaji wa kibepari ukwame.

Ujamaa ulioingia kwa njia ya mapinduzi, ulitazamia kubadilisha hali hiyo, lakini ukaishia kuzuia ushindani, nyenzo muhimu ya matumizi bora ya rasilimali kwa kuthaminisha katika soko, kupatikana bidhaa bora kwa bei ya chini, kila mtu amudu.

Changamoto iliyotawala dunia hivi sasa, ni kutohitajika nguvu kazi, wakulima wazalishe mazao yaoze.

Miaka 100 baada ya 'Capital' tukio linaloendana nalo kwa nchini ni Azimio la Arusha inaweza kuleta majawabu mapya.

Badala ya vijana kuamka asubuhi kukaa barabarani kungoja mtu atake 'deiwaka' au mama ahangaike kuuza hiki au kile awanunulie wanae unga, sukari kwanini isiwepo miundombinu ya kuzalisha mboga na mifugo rahisi kama kuku kila kaya na kila mtu mwenye shauku hiyo, unga upatikane mtu akiuza kuku wa ziada?

Ndicho alichoashiria Mwalimu katika Elimu ya Kujitegemea na katika Ujamaa Vijijini. Aliitangulia dunia kugundua tatizo la ukandamizaji wa wanawake.

Bila ya kuweka miundombinu ya chakula katika familia mikononi mwa wanawake na kuwa na uhakika wa kuwapo kwake katu hatuondoi mtindio wa ubongo unaowasibu asilimia 35 ya watoto wetu.

UCHAMBUZI

# Chadema: Upinzani kurejesha wabunge wengi uchaguzi ujao-2

**Inatoka Uk. 13**

**JIBU:** Changamoto ni nyingi na changamoto nyingi zinaendana na organization culture (mila ya kitaasisi) kwamba mtu unapobadilika kutoka kwenye corporate world (dunia ya mashirika) kuja kwenye political environment (mazingira ya kisiasa), kunakuwa na changamoto nyingi. Kunakuwa na vitu ambavyo unavichukulia katika corporate aspect (mtazamo wa mashirika) ambavyo wanasiasa wanavichukulia poa. Kwa hiyo katika mazingira ya kisiasa, inakuwa ni changamoto kubwa sana kwenda pamoja na kasi ya wanasiasa.

Na hii inaonyesha kabisa kwamba katika kukiunda na kukirudisha chama kuwa taasisi, inakuwa ni kazi ngumu. Mwanasiasa anaamini kwa yale anayoyawaza yeye. Nadhani unaona hata serikali inavyoendeshwa sasa hivi, haifuati taratibu wala kanuni. Kwa hiyo ndio mifumo mingine iliyopo kwenye mifumo ya kisiasa. Watu wanakuwa na haraka na kila kitu kinachukuliwa kama dharura. Kwa hiyo muda wa kufanya planning ni mdogo.

**SWALI:** Ni mafanikio gani makubwa uliyoyapata katika uongozi wako?

**JIBU:** Najivunia kwanza utulivu wa kisiasa ndani ya chama, kwangu mimi naona ni asset (mali) kubwa sana na tumekuwa more organized (tuko vizuri) sasa hivi na system (mifumo) za chama zina function (fanya kazi) kutoka chini kuja juu. Kwa hiyo communication channel (utaratibu wa mawasiliano) umekuwa na heshima kubwa ndani ya chama na kwa muktadha huo, chama kinakuwa tayari kuiongoza dola.

Unajua ili chama kiweze kuongoza dola, lazima kwanza kiweze kujiongoza chenyewe. Kwa sasa hivi naweza kusema kabisa with confidence (kwa uhakika) kwamba sasa hivi chama kina uwezo wa kujiongoza chenyewe.

**SWALI:** Unawaambiaje wanaokulinganisha wewe na mtangulizi wako, Dk. (Wilbroad) Slaa?

**JIBU:** Ukiona unalinganishwa na mtu yeyote, ujue kuwa wanatambua uwepo wako. Kwa hiyo it is a good thing (ni kitu kizuri), ukishaona watu wanaanza kukulinganisha, wanaweza wakakulinganisha kwa sababu wana m-miss (wanamkosa) yule au kwa sababu unaperform (fanyakazi) vizuri. Sasa hatujawahi kupata ile opinion (maoni) yao ya moja kwa moja, kwamba imekuwaje. Lakini kimsingi kila zama na kitabu chake, yule alipita kwenye mazingira ya (Jakaya) Kikwete, ambapo tulikuwa huru kufanya siasa kukimbizana nchi nzima.

Sisi tupo kwenye Mazingira ya (Rais John) Magufuli, ambayo hatupo huru kufanya siasa na kuna watu wanapotea. kwa hiyo ni mazingira mawili tofauti ya kisiasa. Sasa hivi hutakiwi kutumia nguvu kuwaongoza watu, unatakiwa kutumia hekima sana, kwa sababu ukiteleza kidogo tu unaweza kukuta unakiingiza chama chako chote hatarini, kwenye hatari ya kufutwa au hatari ya kukosa wanachama. Kwa hiyo tupo kwenye mazingira ambayo yapo very sensitive (tahadhari) na kila tunachokifanya LAZIMA KICHUJWE KWA KINA.



Baadhi ya viongozi wa Chadema, akiwamo aliyekuwa Katibu Mkuu wa chama hicho Dk. Wilbroad Slaa (aliyefunga bandeji mkono).

> Unajua ili chama kiweze kuongoza dola, lazima kwanza kiweze kujiongoza chenyewe. Kwa sasa hivi naweza kusema kabisa with confidence (kwa uhakika) kwamba sasa hivi chama kina uwezo wa kujiongoza chenyewe.

**SWALI:** Pamekuwa na kesi nyingi sana za viongozi wa Chadema, Je hiyo inawapa funzo gani?

**JIBU:** Kwanza kuna kitu ambacho tunajifunza kwamba katika utawala, kuna mifumo ambayo inatakiwa itegemeane. Unaona, eeeh kwa hiyo kuna mfumo wa dola, yaani Serikali, Mahakama na Bunge ambavyo vinatakiwa vifanye kazi pamoja. Muingiliano wa wazi wa mfumo wetu unaonekana kabisa kwamba kuna baadhi ya level zipo deep rooted kuliko nyingine. Kwa mfano mhimili wa Mahakama kidogo unaingiliwa. Bunge nalo linaingiliwa. Kwa hiyo kimsingi, hii mifumo inaingiliana na inaadhiriana. Lakini pia kwa sisi inatuchukulia muda mwingi sana kwa sababu by the time (wakati) unatoka mahakamani, inakuwa ni ngumu sana kutulia na kufanya kazi. Kwa hiyo hilo ni suala ambalo linatupotezea muda sana.

**SWALI:** Mwaka huu mmejipanga vipi kwa wale waohamia ili kuja kugombea kutoka vyama vingine?

**JIBU:** Watu wote watakaokuja kugombea watashindanishwa kwa kufuata tu taratibu za ushindani, kwa hiyo atakayeshinda atapewa fursa. It doesn't matter (haijalishi) mtu anatoka wapi. Kwamba ile unaongelea kuwa mtu huyu ni wa asili, hamna kitu kama hivyo, mtu yeyote atakayekuja atashindana, akishinda tutaenda naye kama mgombea.

**SWALI:** Una mpango wowote wa kuja kugombea ubunge ama urais?



Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Zanzibar, Salum Mwalim, akihutubia moja ya mikutano ya hadhara mjini Magu, mkoani Mwanza. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**JIBU:** Hiyo ni mipango ya mwanasiasa yoyote na kwa sasa hivi kwa nafasi ambayo nimefikia ya kiuongozi kwenye chama yawezekana kukawa na ugumu kidogo kugombea hizo nafasi kwa sababu natakiwa pia kukiongoza chama kwenda kwenye uchaguzi na kwenda kushinda na hiyo si kazi ndogo. Kwa hiyo yawezekana kutokana na kazi hii niliyonayo ikawa ni ngumu sana kufanya kazi mbili ya ukatibu Mkuu na at the same time (kwa wakati huo) kuwa ni mgombea, lakini still (bado) ningeli-prefer (pendelea) kupata nafasi kubwa zaidi ya kiserikali.

**SWALI:** Tukio la wewe kufukuzwa chuo na kuokolewa na Wakili Ndumbaro lilikupa funzo gani?

**JIBU**: Chuo gani? Kwanza huyo Ndumbaro simfahamu.. hii si unaongelea ile aliyoongea Mlinga juzi bungeni. Mimi sijawahi kufukuzwa chuo Kikuu na wala sijawahi kutetewa na huyo Wakili Ndumbaro, na hata simjui ni nani kwa hiyo ni maneno tu yaliyoibuliwa na wahuni ambao wanakaa tu wanaongea. Mimi nimesoma Chuo Kikuu Makerere, baada ya kumaliza nikaja nikasoma Chuo Kikuu Muhimbili, wakati ninasoma Chuo Kikuu Muhimbili nilikuwa nasoma at the same time (wakati huo huo) ninafanya kazi. Kwa hiyo wakati tunafanya kazi, tuligoma tukafukuzwa kazini, si chuoni.

Sasa ukifukuzwa kazini kwa sheria za serikali, wizara inabidi automatically (moja kwa moja) wanaondoa ile sponsorship (ufadhili) ambao baadaye walinirudishia ila nilikutwa ninafanya kazi nyingine. Kwa hiyo nisingeweza kufanya kazi mbili kwa wakati mmoja, niliamua kuacha moja na kuacha kazi moja.

**SWALI:** Ikitokea ukapata nafasi ya kukutana na Rais Magufuli ni kitu gani unaweza kumwambia?

**JIBU:** Nitamwambia azingatie mambo matatu, uhuru wa watu, demokrasia na uchumi wa soko.

**SWALI:** Watanzania wangependa kufahamu historia yako kwa ufupi mpaka kufikia hapa ulipo, Je ni ipi?

**JIBU:** Mimi kama inavyojulikana kwa wengi ni daktari by professional (kwa taaluma) na nimefanya mafunzo yangu Makerere University nchini Uganda. Nimefanya kazi Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), nimefanya kazi kwenye mashirika ya Kimataifa, kwenye taasisi za dini. Ni mcha Mungu na ni mwanamichezo mzuri tu. Nimecheza kwenye timu za basket ball (mpira wa kikapu) hapa, timu maarufu ya Oilers. Kwa hiyo ni mwanabasketi ball anayejulikana kwenye community (jumuiya) ya basket ballers wa Tanzania.

Nimeanza siasa kutoka shuleni, siasa za wanafunzi. Nimekuwa rais wa Watanzania wanaosoma Makerere University. Nilikuwa pia mjumbe wa baraza la uongozi linalojulikana kama University hall. Kwa hiyo ni mwanasiasa wa Makerere University mzuri tu. Nimefanya pia siasa za NGO, siasa za wafanyakazi kwa trade union (vyama vya wafanyakazi), nimekuwa member (mwanachama) wa Medical Council of Tanzania (Baraza la Tiba Tanzania).

Kuhusu Sekondari, nimesoma Mzumbe High School na Saint Pius Seminary, na kote huko hata primary nimekuwa nikishiriki katika uongozi. Nimeoa na nina watoto wanne, wote wa kiume. Kwa hiyo nina jeshi kubwa na tunaweza tukaunda timu ya basket ball nyumbani. Ni mcha Mungu, ninatimiza wajibu wangu wote katika imani yangu ya Kikatoliki.



Waandamanaji wanaompinga Rais Abdel Fatah al-Sisi katika mji wa bandari wa Suez. **PICHA: MTANDAO**

## Polisi Misri yakabiliana na watu walioandamana

VIKOSI vya usalama nchini Misri, vimepambana na waandamanaji wanaompinga Rais Abdel Fatah al-Sisi katika mji wa bandari wa Suez.

Polisi walitumia gesi ya kutoa machozi pamoja na risasi za moto dhidi ya waandamanaji.

Maandamano yalifanyika katika miji kadhaa ya kumtaka Rais al-Sisi aondoke madarakani.

Maandamano kama hayo ni nadra baada ya Misri kuweka amri ya kupiga marufuku maandamano chini ya sheria iliyopitishwa mwaka 2013, kufuatia kuondolewa madarakani na wanajeshi Rais wa zamani wa nchi hiyo Mohamed Morsi.

Hali ya kutoridhika imeongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya bidhaa nchini humo, ambapo serikali ya al- Sissi imechukua hatua kali za kubana matumizi tangu mwaka 2016, kama sehemu ya kukabiliana na mkopo wa dola bilioni 12 kutoka shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Karibu kila mtu mmoja kati ya raia watatu wa Misri, anaishi chini ya kiwango cha kimataifa cha umaskini kilichowekwa.

Watu hao wanajikimu kwa kutumia chini ya dola 1.40 kwa siku, kulingana na takwimu rasmi zilizotolewa mwezi Julai.

Jumamosi iliyopita, waandamanaji walikusanyika kuelekea katikati ya jiji la Suez, ikiwa ni siku ya pili mfululizo, ambapo walikabiliwa na vikosi vya usalama vilivyozuia barabara kwa vifaru vya kijeshi.

Chanzo kimoja kimeliambia shirika la habari la AFP kwamba, karibu watu 74 walikamatwa katika mji mkuu wa Cairo.

Maandamano hayo yalifanyika baada ya Mohamed Aly, mfanyabiashara aliye uhamishoni na mpinzani wa Rais al-Sisi kuposti mtandaoni wito wa kuwataka watu waandamane kumpinga kiongozi huyo wa Misri.

Mkandarasi huyo wa ujenzi amekuwa akichapisha video ambazo zimezagaa katika mitandao ya kijamii tangu mwanzoni mwa mwezi wa Septemba, akimtuhumu Rais al-Sissi na jeshi kwa kuhusika na rushwa iliyoenea nchini humo.

Rais al Sisi amekanusha madai hayo akisema kuwa yeye ni muadilifu na mwaminifu kwa watu wake na jeshi la nchi yake.

Kundi la kimataifa la kutetea haki za binadamu Human Rights Watch limetoa wito kwa serikali nchini Misri kulinda haki ya watu wanaoandamana kwa amani na kuwaachia mara moja wale waliozuiwa.

**BBC**

UCHAMBUZI

Na Mashaka Mgeta

# Chuki kwa wageni zaathiri heshima ya Afrika Kusini



Mashambulizi kama haya ya raia wa Afrika Kusini yaliyoichafua sura ya nchi hiyo katika uga wa kimataifa: **PICHA: MTANDAO**

VURUGU zilizoibuka nchini Afrika Kusini baada ya 'magenge' ya watu wanaosadikiwa kuwa raia wa nchi hiyo kuwashambulia wageni kwa kisingizio cha kuchukua ajira na biashara zao, zimeichafua taswira ya Taifa hilo kubwa kiuchumi barani Afrika.

Awali, mashambulizi hayo yakatajwa kuanzia kwa baadhi ya madereva wa malori walio raia wa Afrika Kusini, kuanzisha mgomo, wakipinga ajira zinazotolewa kwa raia wa kigeni.

Afrika Kusini ni moja ya nchi zinazokimbiliwa na wageni wakiwamo wahamiaji haramu kutoka sehemu mbalimbali za Afrika, ikisadikiwa kuwa maendeleo yake yamekuwa kivutio kwa wahusika kukimbilia huko.

Lakini kiuhalisia, nchi hiyo bado inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa ajira, hivyo kujenga dhana miongoni mwa raia wake kwamba wageni wanaoishi nchini humo wanahusika kuchangia kadhia hiyo.

Mashambulizi dhidi ya wageni yalishamiri hasa mwishoni mwa Agosti mwaka huu kwenye jiji la Johannesburg ambapo mali za raia wa kigeni ziliharibiwa, maduka kuchomwa moto na watu kuuawa, wengine wakijeruhiwa.

Miongoni mwa nchi ambazo raia wake wakalalamika kwa wingi kuathirika kutokana na mashambulizi hayo ni Nigeria, Zambia, Msumbiji, Tanzania na Kenya.

Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, akazilaani na kukemea vurumai hizo, akisema mamlaka hazitaruhusu vurugu hizo na vitendo vya uvunjaji sheria kuhatarisha usalama wa mamilioni ya raia wa nchi hiyo na wale wa kutoka mataifa ya nje wenye haki kwa mujibu wa sheria kuishi na kufanya biashara kwa amani.

**BUTHELEZI AKWAMA**

Wapo raia kadhaa wakiwamo viongozi wa kisiasa waliojitokeza kupinga mashambulizi hayo, miongoni mwao akiwa ni kiongozi wa chama cha upinzani cha Inkatha Freedom, Mangosuthu Butelezi.

Buthelezi alilazimika kuhutubia kwenye uwanja wa Jules akielezea kusitikishwa na mashambulizi na vurugu hizo zilizoashiria chuki zaidi dhidi ya Waafrika, lakini hakufanikiwa, badala yake aliambulia kuzomewa.

Baada ya hotuba ya Buthelezi, vurugu hizo zikaendelea hadi pale vikosi vya usalama vilipoingilia kati.

Watu kwa makumi waliuawa nchini humo baada ya makundi ya watu kuvamia na kuharibu ikiwamo kuchoma moto maeneo ya biashara zinazofanywa na raia wa kigeni.

Vurumai hizo zikasababisha mvutano wa kidiplomasia na nchi nyingine za kiafrika, hasa Nigeria.

Siku ya kwanza ya mashambulizi hayo, watu kadhaa wenye silaha za jadi walisambaa kwenye viunga vya jiji la Johannesburg, wakipaza sauti zao na kuwataka wafanyabiashara na wafanyakazi wa kigeni kuondoka nchini humo.

Kundi hilo lilielekea kwenye bustani ya Jules mjini Johannesburg mahali ambapo Buthelezi, Kiongozi wa zamani wa upinzani wa chama cha Inkatha Freedom, wakati huo akitarajiwa kutoa hotuba yenye kulaani vurugu hizo.

Msimamo wa Buthelezi ulikuwa kuonyesha jinsi machafuko hayo yalivyoharibu na kuichafua sifa ya Afrika Kusini barani Afrika.

Lakini alizomewa wakati wote alipokuwa akizungumza na watu walionekana 'kumpuuza' wakawa wanatoka kama ishara ya kususia mkutano huo.

Mkuu wa Polisi jijini Johannesburg, David Tembe, akakaririwa akisema baada ya mkutano wa Buthelezi aliyeelezea kuchukizwa na mashambulizi dhidi ya wageni, watu 'hawakumuelewa' na badala yake walianza kushambulia na kuchoma moto magari na majengo.

Licha ya mashambulizi hayo kuwalenga raia wa kigeni, Mkuu wa Polisi huyo akasema yapo maduka na mali za raia wa Afrika Kusini, zilizoharibiwa ikiwamo kuchomwa moto na kuteketea.

Mamia ya watu walikamatwa wakituhumiwa kuhusika katika mashambulizi hayo.

**NCHI YACHAFUKA**

Kama 'alivyotabiri' Buthelezi kwamba mashambulizi na uharibifu wa mali za wageni Afrika Kusini, utalichafua taifa hilo, ndivyo ilivyotokea.

Wanamuziki wenye nafasi kubwa katika kuihamasisha jamii, wakajitokeza sehemu tofauti za Afrika kutunga tungo za kukemea vitendo vya chuki dhidi ya wageni.

Hapa nchini, wimbo wa mwanamuzi Mutalemwa Jason maarufu kama Maalim Nash au Nash Mc ukapenya katika jamii za Waafrika kutokana na jinsi ulivyokuwa na maudhui yenye kukemea chuki za walioshiriki mashambulizi dhidi ya wageni nchini Afrika Kusini

Miongoni mwa maneno yaliyomo kwenye wimbo huo ulio katika mahadhi ya Hip Pop yakasema, "Beti nakutuma mpaka Afrika ya Kusini waambie Wazulu (moja ya makabila makubwa ya nchini humo) waweke silaha chini, kisha wasikilize neno lako kwa makini..."

"Vurugu na mauaji ya Waafrika wenzao, Beti waeleze kwamba sisi ndugu zao, ajira haipatikani kwa kumuua Mtanzania, Msomali, Mmalawi ama ndugu zangu kutoka Nigeria..."

"Lini mtabadilika muwe na roho za kiutu...ninashangaa iweje mfike huku, mnauwa ndugu zenu utadhani mnauwa kuku...TZ (Tanzania) tunasema mgeni aje, mwenyeji apone, kwenu ni tofauti ni mgeni njoo nishike panga nikupige, nikukimbize, nikukamate nikumalize...."

Katika mahojiano yake na BBC, mwanamuziki huyo anasema kuna haja kutumia sanaa kufikisha ujumbe kukemea kile kinachoendelea Afrika Kusini.

"Muziki wa hip pop unatuelekeza kutengeneza watu kifikra na kuhakikisha misingi ya kibinadamu na utu pia unafuatwa," mwanamuziki huyo amekaririwa akisema.

**NIGERIA YAWA 'MBOGO'**

Hadhi ya Afrika Kusini ikazidi kushuka pale Nigeria ilipowaondoa mamia ya raia wake waishio nchini Afrika Kusini na kurejea makwao.

Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Nigeria, ikatumia ukurasa wake wa twitter kuandika kutaarifu kwamba zaidi ya raia 313 walipaswa kuchukuliwa kwa ndege maalum kutoka Afrika Kusini katika awamu ya kwanza na waliosalia watasafirishwa katika awamu ya pili, ndani ya siku zisizozidi tano.

Pia, Nigeria ikawaonya raia wake waliopo Afrika Kusini wajitenge na maeneo yalipotokea mashambulizi dhidi ya wageni.

Uhusiano wa Nigeria na Afrika Kusini ukaingia katika hali tete kiasi cha kumlazimu Rais Muhammadu Buhari, kutuma mwakilishi wake kwenda Afrika Kusini kueleza 'hasira' walizokuwa nazo kutokana na mashambulizi hayo.

Marais Ramaphosa wa Afrika Kusini na Buhari wa Nigeria, mataifa yenye nguvu kubwa za kiuchumi barani Afrika, wanatarajia kukutana nchini Afrika Kusini baadaye mwezi ujao.

UCHAMBUZI

Na Sabato Kasika

# Sakaya: Sina diwani Kaliua, lakini kazi inakwenda sawa



Mbunge wa Kaliua, Magdalena Sakaya.**PICHA: MTANDAO**

JIMBO la Kaliua mkoani Tabora linaongozwa na Chama cha Wananchi (CUF), Mbunge wake akiwa ni Magdalena Sakaya, ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho cha upinzani.

Kaliua ni jimbo lenye kata 13 ambazo 10 kati yake zinaongozwa na madiwani kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) na nyingine tatu zikiwa chini ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Kwa jinsi ambavyo vyama vya CCM na Chadema vilivyogawana kata hizo zote, CUF inabaki na mbunge tu ambaye ni Sakaya, anayetamba kwamba hali hiyo haimsumbui kutekeleza ahadi zake kwa wananchi.

Katika mazungumzo yake na gazeti hili, Sakaya anasema tangu achaguliwe kuwa mbunge amefanikiwa kutekeleza ahadi zake kwa wananchi kwa asilimia 80, na kwamba zilizobaki atazikamilisha kabla ya uchaguzi mkuu wa 2020.

Anasema wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, aliahidi kuunganisha wana Kaliua ambao anadai hawakuwa na umoja na sasa wameungana kwa ajili ya maendeleo ya jimbo lao.

"Hakukuwa na umoja wala ushirikiano, kulikuwa na matabaka na pia vijana kuamkia vijiweni bila kufanya kazi, lakini baada ya kuchaguliwa niliunganisha wana Kaliua na sasa tunaongea lugha moja ya maendeleo," anasema.

Fuatilia mahojiano na Mbunge huyo:

**SWALI:** Unasema umewaunganisha wana Kaliua katika kukabili changamoto mbalimbali zinazowakabili, hebu fafanua, ulitumia mbinu gani?

**JIBU:** Jambo la kwanza niliitisha semina mbalimbali na kuzungumza na wananchi kuhusu umuhimu wa kuungana kwa ajili ya maendeleo ya jimbo letu na kuwaeleza madhara ya matabaka, bahati nzuri wakanielewa. Pia nilikuwa ninazungukia vijiwe vya vijana na kuwahamasisha jinsi ambavyo wanaweza kuachana na mtindo huo na kufanya kazi za kuwaletea maendeleo na sasa kila mmoja anafanya shughuli hasa za kilimo, kwani Kaliua mbali na kilimo cha mazao ya biashara kama tumbaku na pamba, tunalima pia mazao ya chakula yakiwamo mahindi, mpunga, mihogo na karanga. Nikwambie tu tangu niwe mbunge kila mtu akiamka anakwenda shamba na kwa kweli watu wamelima tumbaku na pamba kwa wingi hadi sasa imekosa soko.

**SWALI**: Mbali na ahadi hiyo, ni zipi nyingine ulizokuwa umeahidi na umezifanyia kazi au unaendelea kuzitekeleza?

**JIBU:** Elimu ilikuwa ni moja ya vipaumbele vyangu, kwani wakati ninaingia kwenye ubunge, Kaliua ilikuwa ni ya mwisho kimkoa na kitaifa kwenye elimu ya msingi na sekondari. Kuna wakati ambapo tatizo la watoto la kutojua kusoma na kuandika lilikuwa kubwa mkoani kwetu na watoto wengi wenye tatizo hilo walikuwa wanatoka Kaliua. Mimi kama mwakilishi wa jimbo nilikutana na walimu na kuzungumza nao, ikabainika kuwa chanzo kikubwa cha tatizo ni wazazi kutojua wajibu wao na walimu kukata tamaa kutokana na changamoto mbalimbali. Kwa ujumla ni kwamba tulijadili tatizo hilo kwa kina na kuangalia uwezekano wa kulitafutia ufumbuzi ukiwamo wa kutoa motisha kwa walimu na sasa hatuna sifuri wala divisheni 'four.' Mwaka jana, tulitoa mwanafunzi bora kitaifa wa darasa la saba. Yaani kutoka kushika mkia hadi kuwa wa 14 kiwilaya. Vilevile kwa upande wa afya ni kwamba Kaliua ilikuwa inaongoza kwa vifo vya mama na mtoto kimkoa. Kwa kuwa niliahidi kujenga vituo vya afya, hadi sasa kwa kutumia Fedha za Mfuko wa Jimbo, tumejenga vituo vinne. Yaani ni kwamba kulikuwa na kimoja na vituo vingine vitatu vilianza kujengwa na kuishia njiani. Ndipo mimi nikaja kumalizia, sasa vinafanya kazi na tuna zahanati 14 na tunaendelea na ujenzi wa hospitali ya wilaya na pia kama mbunge nilishatoa msaada wa vitanda 12 kwenye kituo kimoja cha afya cha binafsi ambacho kina jengo la upasuaji. Ninaweza kusema kuwa nimeweza kutekeleza ahadi zangu jimboni kwa asilimia 80 na ninaendelea kutekeleza asilimia 20 iliyosalia.

> "Hakukuwa na umoja wala ushirikiano, kulikuwa na matabaka na pia vijana kuamkia vijiweni bila kufanya kazi, lakini baada ya kuchaguliwa niliunganisha wana Kaliua na sasa tunaongea lugha moja ya maendeleo," anasema.

**SWALI:** Jimbo lako linapata kiasi gani ya cha Fedha za Mfuko wa Jimbo?

**JIBU:** Vigumu kutaja kiasi kamili cha fedha hizo, kwasababu wakati mwingine huwa kinabadilika na mara nyingi Kaliua huwa tunapata Sh. milioni 52 na wakati kiasi hicho kinaweza kupungua kulingana jinsi ambavyo serikali yenyewe imepanga. Hicho tunachokipata ndicho tunatusukuma kwenye shughuli za maendeleo ya jimbo letu. Na ninaamini kwa ushirikiano tulionao kama wana Kaliua tunafika mbali, kwani tumechelewa sana kupata maendeleo kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za watangulizi wetu kutozingatia maendeleo ya jimbo na kufanya mambo yao wenyewe na kuacha jimbo likiwa nyuma. Sasa tunajitahidi kuhakikisha tunapiga hatua kwenda mbele na tunakwenda vizuri.

**SWALI:** Katika jimbo la Kaliua, unasema chama chako hakina diwani hata mmoja, umewezaje kufanya kazi kwa ufanisi?

**JIBU:** Kwa wale wasiojua ni kwamba kaulimbiu yetu ni 'Kaliua Maendeleo, Maendeleo Kaliua'. Tunachozingatia ni kwamba hakuna mambo ya chama, wote tunaongea lugha moja ya maendeleo tu. Kwa hiyo, CUF kutokuwa na diwani si kikwazo cha kutimiza ahadi zangu kwa wananchi wala kuleta maendeleo Kaliua. Ninafanya kazi na madiwani wote 13 wa CCM na Chadema, tena kwa ushirikiano mkubwa. Kama unafuatilia kwenye vyombo vya habari, hata viongozi wa CCM wa Mkoa wa Tabora walishanipongeza kwa jinsi ninavyotekeleza majukumu yangu ya kibunge kwa ufanisi. Kwamba licha ya CUF kutokuwa na diwani, lakini ninatekeleza majukumu yangu vizuri. Hii inatokana na kutambua kuwa maendeleo hayana chama. Wote ni wana Kaliua bila kujali itikadi za vyama vyetu, tunatakiwa kuijenga Kaliua yetu. Watanzania wote tukitambua kwamba maendeleo hayana chama tutafika mbali kimaendeleo. Sisi tunaendelea kuongozwa na kaulimbiu yetu ambayo tunaamini inatufikisha kule tunakoelekea.

# Dunia yatathmini kuondoka Ikulu ya Trump kwa 'mwenye mustachi'

**Na Anil Kija**

KILA mwenye pumzi katika masuala ya mambo ya nje alikuwa akitafakari au kuzungumzia kuondoka Ikulu ya Marekani kwa John Bolton, mwanaharakati na mpambanaji wa kihafidhina aliyekuwa mstari wa mbele kuchochea vita kati ya Marekani na maadui zake.

Rais Donald Trump alitangaza kumwondoa katika nafasi ya Mshauri wa Usalama wa Taifa kabla ya sherehe za kumbukumbu ya Septemba 11, 2001 ambako ndege tatu ziligonga 'minara maghorofa mia' ya Kituo cha Kimataifa cha Biashara na jengo la Wizara ya Ulinzi ya Marekani.

Trump alisema alihitilafiana na Bolton katika masuala kadhaa, hasa kusumbukia mwelekeo wa kuinua vita na Iran.

Zilikuwapo pia tofauti za kina baina ya Trump na Bolton (ambaye amewahi kukataliwa na Bunge la Marekani kuwa balozi wa nchi hiyo Umoja wa Mataifa wakati wa Rais George W. Bush lakini akateuliwa Bunge likuwa likizoni).

Hata hivyo, baadhi ya wachunguzi na hasa wasemaji wa nchi tofauti, na zaidi Iran, wanajaribu kuona sera za Marekani na uwezekano wa uhasama kufikia vita kana kwamba ulitokana tu na ushauri wa Bolton.

Wengi zaidi kati ya wachunguzi wanaona kuwa licha ya kuvuka mipaka, mwelekeo wa Trump na Bolton ni pacha.

Kinachokubaliwa bila ubishi ni kuwa kuondoka kwa mshauri huyo wa Usalama wa Taifa kunaondoa sauti yenye nguvu zaidi katika utawala wa Trump inayoshauri mtazamo mkali wa kusukuma malengo ya Marekani, ikibidi kwa kuinua vita.

Licha ya kuwa kwa wachambuzi wengi, washiriki wa Trump kama Waziri wa Mambo ya Nje, Mike Pompeo ni watu wa 'siasa kali' kama Trump mwenyewe na Bolton, kuna hisia kuwa kutakuwa na 'afueni' kwa baadhi ya washindani wa Marekani kutokana na kupungua kwa waunga mkono 'siasa kali' Ikulu.

Hata hivyo, baadhi kama wapiganaji wa Taliban nchini Afghanistan wamechochea hisia hiyo upya.

Dalili za utofauti kati ya Trump na Bolton zilikuwepo kwa muda kutokana na mwelekeo wa Trump wa kujaribu kutatua migogoro mikubwa kwa njia ambazo siyo za kawaida, kwa mfano kutaka maelewano na Rais Vladimir Putin wa Russia bila maendeleo yoyote kufikiwa katika ajenda muhimu zinazomgombanisha Putin na nchi za NATO (Ulaya Magharibi na Amerika ya Kaskazini).

Sababu ni kuwa mwelekeo wa jumla wa NATO na Umoja wa Ulaya umelenga mno uelewano wa kiliberali (kwa hisia za Marekani, udhaifu) wakati Trump anataka Marekani ijizatiti zaidi kama nchi, na siyo iwe kiongozi wa mkumbo. Putin ana hisia kama hizo maeneo kadhaa.



Aliyekuwa Mshauri wa Usalama wa Rais Donald Trump wa Marekani. **PICHA: MTANDAO**

Mojawapo ya mikanganyiko kuhusu mwelekeo wa sera za Marekani baada ya kuondoka Bolton ni suala la Afghanistan, ambako mwelekeo wa Trump ni kumaliza vita hivyo, hisia yake halisi ikiwa ni kuachana na vita hivyo ila – kama ilivyo kwa Boris Johnson na Brexit analazimishwa kutafuta mkataba, yaani suluhu.

Kama ilivyo kwa Umoja wa Ulaya kutokuwa na mpango wa mkataba mpya wowote na Uingereza, kundi la Taliban pia halina mpango wowote wa kufikia amani halisi na Marekani.

Inachotaka ni kuwa Marekani itoke; inashambulia huku inaitwa Ikulu. Hatua ya kumwua askari mmoja wa Marekani na kujeruhi watu wengine kadhaa karibu na ubalozi wa Marekani jijini Kabul ukavuruga mpango wa mazungumzo ya faragha nchini Marekani, hatua ambayo Bolton alikuwa akiipinga.

Rais Trump ameahidi kuzidisha kipigo kwa Taliban.

Shirika la habari mtandaoni la Bloomberg lilisema kuwa kuondoka kwa Bolton kunaweza kuwa habari mbaya kwa Rais Ashraf Ghani wa Afghanistan, kwani kundi la Taliban muda wote lilikataa kukaa meza moja kujadiliana na utawala wa Kabul.

> Hivyo kwa Rouhani na wapambe kusema hapatakuwa na mazungumzo na Marekani bila kuondolewa vikwazo vyote ni kama kudhani kuwa hakuna mwelekeo wa kupambana na Iran ila ushauri tu wa kina Bolton.

Unataka ujadiliane na Marekani pekee, lakini hivi karibuni Rais Trump kupitia waziri Pompeo aliwezesha mazungumzo ya pande hizo mbili kufanyika, au labda kuahidiwa kufanyika kwani Bloomberg linasema kuwa Ghani hakuwa mshirika wa moja wa moja katika majadiliano yanayoendelea.

Taliban inajua kuwa Marekani imeanza kuchoshwa na vita ya Afghanistan, na kuwa ikiondoka tu, Taliban inakamata.

Ila ni kuhusiana na Iran ambako mwelekeo wa kujikanganya ulikuwa unaonekena wazi, kwa jinsi Iran ilivyofurahia kuondoka kwa Bolton na kuanza kutoa ushauri kwa Marekani 'kuachana na wachochea vita.'

Wachunguzi walisema utawala wa Iran ulijitahidi kutumia tukio la kufukuzwa kazi Bolton kama udhihirishaji wa usahihi wa msimamo wa Rais Hassan Rouhani, ambako waziri wake wa Mambo ya Nje, Javad Zarif alisema kuwa Bolton alikuwa mmoja katika ile 'B-Team' ya maadui wa Iran, yaani Bolton, mwanamfalme Mohamed bin Salman wa Saudi Arabia na Benjamin Netanyahu, waziri mkuu wa Israel ambaye kimsingi yuko vitani na Iran.

Hata hivyo, balozi wa Iran katika Umoja wa Mataifa alisema Iran haihusiki na masuala ya utawala wa Marekani.

Msimamo wa Trump kuhusu Iran umeendelea kuwa ule ule wa 'maximum pressure' kulazimisha Iran ibadilike na kuwa nchi ya kawaida, na siyo kuwa na malengo ya kijeshi ya kubadili sura ya Mashariki ya Kati iendane na utawala wa Kishia nchini humo.

Alichokosana na Bolton ni kasi ya kutaka kubadili utawala nchini Iran, ambako mwelekeo wa Trump na Pompeo ni kuelekeza nguvu katika vikwazo vya uchumi ili Iran iyumbe na hatimaye utawala wa makuhani uporomoke na siyo kupeleka meli kubwa za kivita kama Bolton alivyokuwa anashauri.

Hivyo kwa Rouhani na wapambe kusema hapatakuwa na mazungumzo na Marekani bila kuondolewa vikwazo vyote ni kama kudhani kuwa hakuna mwelekeo wa kupambana na Iran ila ushauri tu wa kina Bolton.

Baadhi ya wachunguzi walisema kuwa Iran inalenga 'kugema' katika hisia za 'kupiga dili' za Trump na kutokana vita, mwelekeo uliomfanya akutane na kiongozi mkuu wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un.

Wanaomwangalia Trump kwa mtazamo huo ni pamoja na Rais Emmanuel Macron wa Ufaransa ambaye wakati wa mkutano wa hivi karibuni wa kundi la nchi saba tajiri za G7 nchini mwake alijaribu kupata uhakikisho wa mkutano kati ya Trump na Rouhani kandokando ya kikao kijacho cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa jijini New York.

Trump amesema mara kadhaa kuwa angekuwa tayari kufanya mazungumzo na Iran bila masharti, lakini Iran imekuwa ikitaka uhakikisho vikwazo kuondolewa, ina maana Marekani iutambue tena mkataba wa nyuklia.

Licha ya kuwa kuna wasiwasi mkubwa miongoni mwa wasaidizi wa Netanyahu kuhusu azma ya Marekani baada ya kumtosa Bolton, mtetezi mkuu wa sera ya kula sahani moja na Iran, baadhi ya wachunguzi wanasema kuwa suala la Israel ni tofauti na Iran, au Afghanistan.

Watetezi wa kina wa Israel nchini Marekani ni kundi la wahafidhina wa kidini (fundamentalists) ambao wanaona Palestina kama eneo la nchi ya ahadi iliyotolewa kwa Wayahudi, 'hadithi' ambayo watu wa sera za kiliberali (kiharakati) wanaibeza, kwani wanaona Wayahudi na Israel yenyewe ni wavamizi tu Mashariki ya Kati.

Pia kuna suala la Korea Kaskazini ambako Kim Jong-un amekuwa akizidisha majaribio ya makombora ya masafa mafupi kuwatishia ndugu zake wa Korea Kusini, siyo yale ya 'kuvuka mabara' yaliyomfikisha kutazamia vita na Marekani wakati wowote.

Na wakati huo Bolton hakuwa mshauri wa Usalama wa Taifa, na aliyekuwa waziri wa Mambo ya Nje, Rex Tillerson aliondolewa na Trump kwa kutetea mkataba wa nyuklia na Iran. ()



# Wataka sheria uchaguzi mitaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKATI hekaheka za maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa zikiendelea nchini, viongozi wa dini mkoani Mbeya wamewataka wanasiasa kuzingatia sheria ili ufanyike kwa amani na utulivu.

Wakizungumza jana kwenye kikao cha wadau wa uchaguzi kilichowahusisha viongozi wa vyama vya siasa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) na Jeshi la Polisi, viongozi hao wa dini waliwataka wanasiasa kuepuka matumizi ya fedha ili viongozi wapatikane kwa haki.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wakristo Mkoa wa Mbeya, Askofu Dk. Donald Mwanjoka, alisema mkoa wa Mbeya ndio unaotazamwa zaidi nchini katika masuala ya dini, hivyo ni vyema hata katika masuala ya amani yakazingatiwa ili kuupa heshima.

**Kazi ya jeshi hilo katika shughuli za uchaguzi ni kuhakikisha amani na utulivu vinakuwapo ili kila mwananchi atimize haki yake ya kupiga kura.**

Alisema wakiwa viongozi wa dini watahakikisha wanawaelimisha washirika wao juu ya kushiriki katika uchaguzi huo bila kuvuruga amani ikiwamo kuheshimu uamuzi wa wananchi wengine bila kulazimishana.

"Kuna watu kwenye hizi shughuli huwa wanabeba fedha. Sasa tunaomba wasije wakaanza kuzitumia kwa ajili ya rushwa ambayo inaweza kuvuruga uchaguzi. Sisi viongozi wa dini hatugombei na hatuegemei upande wowote isipokuwa tunaombea amani," alisema Dk. Mwanjoka.

Alisema amani wanayoombea si kwa uchaguzi wa serikali za mitaa pekee bali hata uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwakani. Naye Mwenyekiti wa Maimam wa Mkoa wa Mbeya, Shekh Iddy Tuwa, aliwaomba wasimamizi wa uchaguzi kuwa waadilifu ikiwa ni pamoja na kuwatangaza washindi halali bila kujali chama wanachotoka ili kuepusha vurugu.

Alisema katika uchaguzi huo, wananchi ndio wanaoamua waongozwe na nani na si msimamizi wa uchaguzi au mdau mwingine yeyote wa uchaguzi huo.

"Sisi viongozi wa dini lazima tuwaelimishe waumini wetu ili wajue kuwa uchaguzi ni kitu cha kupita. Bada ya hapo maisha yanaendelea, hivyo amani na utulivu ni vitu vya msingi kuzingatiwa na hili litafanikiwa endapo wote tutakuwa waadilifu," alisema Shekh Tuwa.

Mwakilishi wa Takukuru kwenye kikao hicho, Patrick Mselele, ambaye ndiye atakuwa anasimamia masuala ya uchaguzi, aliwatahadharisha wagombea wote na washirika wao kuepuka kutoa zawadi za aina yoyote wakati wa uchaguzi.

Alisema kuna baadhi ya watu wana tabia ya kukitumia kipindi hicho kuwagawia wananchi zawadi ndogo ndogo vikiwamo vitenge, chumvi, soda na fulana.

Mselele alisema kwa sasa wanaendelea kutoa elimu ya masuala ya rushwa kwa wananchi na kwamba kabla ya Novemba 24 watakuwa wamemaliza kazi hiyo na baada ya hapo itabaki usimamiaji wa sheria.

Naye Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Mbeya, James Chacha, alisema kazi ya jeshi hilo katika shughuli za uchaguzi ni kuhakikisha amani na utulivu vinakuwapo ili kila mwananchi atimize haki yake ya kupiga kura.

Aliwataka wanasiasa kuwaeleza washirika wao ukweli ili kuepuka kuwachochea kufanya fujo kitu ambacho alisema kinaweza kikawasababishia matatizo.

Kaimu Msimamizi wa Uchaguzi Wa Jiji la Mbeya, Gregory Emmanuel, alisema uandikishaji wa wapigakura utafanyika kwa siku saba kuanzia Oktoba 8 mpaka Oktoba 14, mwaka huu, hivyo akawataka wananchi kujitokeza kujiandikisha.

## Wafanyakazi afya wapewa somo utendaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, amewataka wafanyakazi wa afya kufanya kazi kwa kuzingatia maadili ya kazi yao ili kulisaidia taifa kusonga mbele kimaendeleo.

Alitoa ushauri huo juzi alipokuwa anafungua mafunzo kwa waajiri na viongozi wa matawi ya Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya Tanzania (Tughe) kutoka katika mikoa minane ya Tanzania.

Aliwataka kuepuka kujipa likizo za mara kwa mara na badala yake wautumie muda mwingi katika kuokoa maisha ya watanzania wenzao ambao wanasumbuliwa na magonjwa mbalimbali.

Vilevile aliwataka waajiri kuwatimizia haki waajiriwa wao ili kuongeza ufanisi kwenye utendaji kazi kwa madai kuwa watumishi wanapotimiziwa haki zao huwa wanaongeza kasi ya kujituma.

Alisema baadhi ya watumishi huwa wanashindwa kutimiza majukumu yao kutokana na kutotimiziwa haki zao na waajiri na kwamba huwa wanaamua kupoteza muda kwa kufanya mambo ambayo hayastahili.

"Mimi katika kipindi cha miaka 31 ya utumishi wangu serikalini niliwahi kwenda likizo mara moja pekee maana kila nikitaka kwenda nakuta kuna majukumu yananikabili, sasa natamani hata ninyi ndugu zangu mpunguze hizo likizo," alisema Ntinika.

Katibu Mkuu wa Tughe, Hery Mgunda , alisema viongozi wa Tughe kwa kushirikiana na waajiri watahakikisha wanatimiza wajibu wao ili kuhakikisha nchi inasonga mbele.

Mgunda alisema chama kinaipongeza serikali ya awamu ya tano kwa kuwashirikisha katika vikao mbalimbali vya uamuzi hali ambao inaongeza ufanisi kwenye kazi.



Mfanyausafi akiondoa takataka kwenye mtaro wa maji ya mvua katika Mtaa wa Muheza eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Wakutana kutathmini maendeleo kilimo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATAFITI 110 wa mazao na mifugo kutoka katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na halmashauri zake, wameshiriki mkutano wa tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya kilimo ya mwaka wa fedha 2018/19 katika ukanda huo.

Mkutano huo ulifanyika kwa siku mbili katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) Kituo cha Uyole, jijini Mbeya na taasisi hiyo iliwajulisha kuwa imeandaa aina 55 za mbegu mpya za mazao mbalimbali ambazo zinaendana na uchumi wa viwanda.

Mkurugenzi wa Tari- Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema lengo la mkutano huo ilikuwa kuangalia changamoto zilizowakabili wakulima katika msimu uliopita na kujadili namna ya kuzitatua ili zisikwamishe juhudi za uzalishaji msimu mpya unaokuja.

Alisema pia mkutano huo ulilenga kutambulisha mbegu mpya za mazao zilizofanyiwa utafiti ili wataalamu hao wakazisambaze kwa wananchi na kwamba mbegu hizo zina manufaa makubwa kutokana na uzaaji wake.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, wanataka kumuondoa mkulima wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwenye kilimo cha mazoea na kumfanya azalishe kibiashara ili anufaike zaidi na shughuli hiyo.

Dk. Bucheyeki alisema mbegu hizo mpya zitawafikia Watanzania wote wanaojishughulisha na kilimo na si kama ilivyokuwa awali ambapo wanufaika wakubwa walikuwa wakulima wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

"Mwaka jana tulikuwa na mbegu 50 za mazao ambazo tulizifanyia utafiti lakini mwaka huu tumeongeza mbegu zingine tano na kufikisha mbegu 55. Sasa hawa wataalamu wa utafiti kutoka maeneo ya ukanda huu tumejumuika nao ili tuelezane mwelekeo mpya. Wataeleza changamoto zinazowakabili na tutakubaliana namna ya kuzikabili," alisema Dk. Bucheyeki.

Alitaja baadhi ya mbegu za mazao walizozifanyia utafiti kuwa ni mahindi, maharage, viazi mviringo na viazi lishe, ndizi, ngano, soya, maparachichi na mboga.

Naye Mtafiti wa mahindi katika Tari - Uyole, Leonard Sabula, alisema kwa sasa wanalenga kuwainua wakulima kwa kuwaelimisha kutumia mbegu zilizofanyiwa utafiti ili wanufaike zaidi na kilimo hicho kwa kupata mavuno mengi.

Alisema mbegu hizo zilizofanyiwa utafiti zipo katika ubora nawanazalisha zina uwezo wa kukinzana na magonjwa pamoja na mabadiliko ya tabia nchi ambayo ndiyo yanawatesa zaidi wakulima kwa sasa.

Alisema wakati huu ambao serikali ya awamu ya tano inasisitiza kuingia kwenye uchumi wa kati ambao unaendana na mapinduzi ya viwanda ni lazima watafiti na wataalamu wa kilimo washirikiane kuhakikisha wananchi wanazingatia mbinu bora za kilimo.





# Wakazi walilia zahanati

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

WAKAZI wa Kijiji cha Singonhali wilayani Mpwapwa mkoani Dodoma, wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa huduma ya afya na kulazimika kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Kijiji hicho hakina zahanati, hali inayosababisha vifo vya wajawazito na watoto kutokana na kutembea umbali wa zaidi ya kilometa saba kufuata huduma ya matibabu katika kijiji cha jirani.

Wakazi hao wameiomba serikali kusaidia kukamilisha ujenzi wa zahanati ambayo wananchi wameanza kuijenga, lakini ujenzi umesimama kwa zaidi ya miaka mitano kutokana na ukosefu wa fedha. Akizungumza na waandishi wa habari, mmoja wa wakazi wa kijiji hicho, Jonas Homange, alisema ukosefu wa huduma ya afya ni kero kubwa kwao.

Alisema wajawazito wamekuwa wakipata shida wakati wa kujifungua na wengine kujifungulia njiani wakielekea kijiji jirani cha Rudi, chenye kituo cha afya.

**Hivi karibuni kilitokea kipindupindu watu walipata shida sana kutokana na kutokuwapo kwa wataalamu wa afya ambao wangeweza kutusaidia kutupa mbinu za kukabiliana na ugonjwa huo.**

Mwaka 2013, wakazi wa kijiji hicho waliamua kuanzisha ujenzi wa zahanati na walichangia michango ya fedha pamoja na nguvu kazi ya kubeba mawe na mchanga, lakini hawajaweza kukamilisha ujenzi huo.

Alieleza kuwa serikali pia ilitoa kiasi cha Sh. milioni 48, ili kukamilisha ujenzi huo.

"Lakini toka wakati huo pamoja na serikali kutoa hiyo milioni 48 zahanati hii bado haijakamilika na fedha zote zimeliwa na wananchi tunaendelea kupata shida hii ya kupata matibabu katika kijiji chetu hasa kinamama wajawazito na watoto," alisema Homange.

Alisema wamepeleka malalamiko yao kwa uongozi wa juu, lakini bado hakuna hatua zozote zilizochukuliwa.

Naye Afronsina Witike, alisema amepitia changamoto kubwa kutokana na kukosekana kwa huduma ya zahanati kijiji hapo hali ambayo imekuwa ikimlazimu kujifungulia nyumbani kinyume na kanuni za afya.

"Hapa kwetu hatujawahi kuwa na zahanati lile jengo tuliojenga hadi hii leo halijakamilika, lakini hatuwezi kuacha kuzaa, unapokuwa mjamzito kupata usafiri wa kukufikisha kule kwenye kituo cha afya fedha hakuna inabidi kujifungulia nyumbani, lakini unapofika katika kituo cha afya unapigwa faini kwanini umezalia nyumbani," alilalamika.

Alisema pamoja na umbali wa huduma ya afya, lakini pia bado wanakabiliwa na changamoto ya miundombinu mibovu ikiwamo ubovu wa barabara.

"Wajawazito tunatumia usafiri wa pikipiki tukishikwa na uchungu wa kujifungua sasa mpaka ufike kule tayari unakuwa umepata shida hivyo pale kituo cha afya Rudi itabidi wakupe rufaa ya kwenda hospitali ya wilaya nako wanataka fedha ya nauli ni kiasi kikubwa, kama zahanti yetu ingekuwa tayari imekamilika tusinge kutana na adha hii," alisema.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Msigala Furahisha, alisema kijiji hicho kina zaidi ya wakazi 3,000 kaya 618.

"Hivi karibuni kilitokea kipindupindu watu walipata shida sana kutokana na kutokuwapo kwa wataalamu wa afya ambao wangeweza kutusaidia kutupa mbinu za kukabiliana na ugonjwa huo," alisema Furahisha.



Kijana akinadi mbwa ili kujipatia kipato katika mitaa ya Uhindini, jijini Dodoma jana. Mbwa huyo alikuwa akimuuza kwa bei ya 80,000/-. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Watafiti afya waaswa kumaliza changamoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imezitaka taasisi za umma na binafsi zinazofanya utafiti wa afya kuhakikisha matokeo ya kazi yanaendana na sera na utekelezaji wa afua (mikakati ya kukabiliana na magonjwa), ili kutatua changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

Mkurugenzi wa Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe, Dk. Ntuli Kapologwe, kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), alitoa ushauri huo.

Aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa kongamano la tatu la ufuatiliaji na tathmini kuhusu masuala ya afya lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Mzumbe kwa kushirikiana na Chuo cha St.Francisco, lililojumuisha wataalamu mbalimbali wa afya.

Dk. Kapologwe alisema utafiti na machapisho mengi yanayofanyika yanaishia kwenye kumbukumbu na kushindwa kusaidia kutatua changamoto kwenye sekta ya afya.

Aidha, alitaka vyuo kufanya utafiti ili kutoa takwimu sahihi kuhusiana na ujenzi wa vituo vya afya kuondoa msongamano wa wagonjwa.

"Tunawakaribisha mje mfanye utafiti katika vituo vya afya vilivyojengwa ili kuona huduma ikoje na jitihada za kupunguza vifo vya kinamama na watoto," alisema Dk. Kapologwe.

Alisema wakifanya hivyo itasaidia kujua takwimu sahihi kulingana na kilichokuwa awali na hivi sasa kupitia takwimu ambazo zimetolewa na watafiti.

Sambamba na hilo, aliagiza waganga wakuu wa mikoa na wilaya kuanzia mwaka huu kutenga fedha kwa ajili ya ushiriki wa makongamano ya afya na ufuatiliaji takwimu ambazo zitawasaidia kuleta matokeo chanya katika sekta ya afya.

Alisema waganga hao wanapaswa kutenga bajeti ya fedha ambayo itawasaidia upatikanaji wa takwimu sahihi.

# Watakiwa kusaidia mabinti kufikia masomo ya juu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wa elimu wametakiwa kuangalia njia sahihi itakayosaidia kuondokana na tatizo la watoto wa kike kushindwa kuendelea masomo wanapomaliza shule ya msingi na kidato cha nne.

Mwenyekiti wa mtandao wa mashirika yanayojihusisha na masuala ya elimu(TENMET), Dk. John Kalaghe, alisema katika mkutano wa mwaka wa wadau wa sekta hiyo ulio tathmini utekelezaji wa malengo ya sekta hiyo yaliyowekwa mwaka jana.

Alisema pamoja na kuwapo na uwiano wa kijinsia kwenye udahili, lakini watoto wa kike wanaoendelea baada ya shule ya msingi hupungua.

"Kwa takribani miaka mitano hadi sita ni asilimia tano mpaka sita ya watoto wanaomaliza kidato cha nne wanapata nafasi kuendelea na kidato cha tano, sasa sisi kama wadau wa elimu tunatakiwa kuishauri serikali namna ambayo itasaidia idadi ya mabinti wanaoendelea na masomo ya juu inaongezeka," alisema Kalaghe.

Aidha, alisema mafanikio kama ongezeko la udahili kwa elimu ya msingi ambao umefikia zaidi ya asilimia 90 ni kiwango kikubwa na cha kujivunia.

"Idadi ya watoto wanaopita kutoka shule za msingi kwenda sekondari imefikia asilimia 70 na uwiano wa kijinsia kwenye udahili kwa sasa upo sawa," alisema.

Hata hivyo, licha ya mafanikio kuna changamoto ya miundombinu ambapo ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2016/17, inaonyesha kuna upungufu mkubwa wa madarasa, nyumba za walimu na vyoo kwa shule za msingi kwa zaidi ya asilimia 50.

"Sasa tunafanyaje kuhakikisha kwamba haya mafanikio ya kuongezeka kwa watoto yasiathiri utoaji wa elimu kwasababu ukiwa na darasa lenye watoto 150 au 200 ni vigumu mwalimu kufundisha ipasavyo, tuhakikishe ongezeko hili haliathiri ubora wa elimu," alisema mwenyekiti huyo.

Dk. Kalaghe ambaye ni Mkurugenzi wa HakiElimu, alisema bado kuna ukatili shuleni licha ya kuwapo kwa sheria nzuri na kwamba changamoto ni katika usimamizi.

Awali, akifungua mkutano huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, alisema wizara imefanya mambo mengi katika upanuaji wa miundombinu kwa ngazi zote.

Hata hivyo, alisema hakuna nchi inayoweza kujisifu hivi sasa kwamba elimu yake ni bora na kwamba ni suala la mchakato wa kufanya marekebisho mbalimbali ikiwamo mitaala.

"Suala la kusema elimu yetu ni mbaya nimekuwa nikilikataa kwa sababu elimu ni nzuri ukimtoa mhitimu wa kidato cha nne aliyefaulu ukampeleka kidato cha tano nchi nyingine yeyote ana 'fit' vizuri, mtu aliyefaulu kidato cha sita anaweza kujiunga na shahada ya kwanza katika taifa lolote kama wanatumia lugha ya Kiingereza na wanafanya vizuri," alisema Dk. Akwilipo.

Alieleza kuwa kuna changamoto kadhaa zinahitaji kufanyiwa kazi ili kuwa na wanafunzi na wahitimu bora.





# Sera ya Elimu Zanzibar kufanyiwa marekebisho

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema iko haja ya kuipitia na kuifanyia marekebisho Sera ya Elimu ya Mwaka 2006 kutokana na mabadiliko yaliyojitokeza kitaifa na kimataifa.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Simai Muhammed Said, aliyasema katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said.

Mwakilishi huyo alihoji kama serikali haioni kwamba wakati umefika kwa sera hiyo kupitiwa na kufanyiwa marekebisho ili iendane na mahitaji ya sasa ya elimu.

**Msingi inatolewa kwa muda wa miaka sita kwa Zanzibar, wakati kwa Tanzania Bara inatolewa kwa muda wa miaka saba.**

Naibu Waziri huyo wa elimu alisema wizara yake kwa kulielewa hilo imefanya mapitio na marekebisho ya sera hiyo ili kwenda sambamba na mabadiliko hayo.

Alisema hadi sasa rasimu ya mapitio ya sera hiyo imetayarishwa na kuwasilishwa katika ngazi za uongozi wa wizara kwa maoni zaidi.

Said alieleza kwa mujibu wa Sera ya Elimu na Ufundi ya Tanzania, elimu ya sekondari inatolewa kwa miaka minne kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne na kwa upande wa Sera ya Elimu Zanzibar nayo inatolewa kwa miaka minne.

Aidha, alisema kwa upande wa elimu ya maandalizi na msingi pia hutolewa kwa miaka minane kwa Zanzibar na Tanzania Bara miaka minne lakini tofauti iliyopo ni kwa Zanzibar kutoa elimu ya maandalizi kwa miaka miwili na Tanzania Bara mwaka mmoja.

Naibu Waziri alisema elimu ya msingi inatolewa kwa muda wa miaka sita kwa Zanzibar, wakati kwa Tanzania Bara inatolewa kwa muda wa miaka saba.

"Miaka minane hiyo ya elimu ya msingi na maandalizi kwa pande zote mbili za Muungano zinatosha kukamilisha mitaala ya ngazi hizo kwa kumtayarisha mtoto kwa masomo ya elimu ya sekondari na kufanya mitihani ya sekondari ya kidato cha nne kwa pamoja hasa ukizingatia mtaala wa sekondari unaotumika pande zote mbili ni mmoja," alisema.




Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ussi Yahya Haji, akisoma gazeti la Nipashe nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Vitongoji 200 bado kufikiwa na umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati imesema vitongoji 200 bado havijafikiwa na kuunganishwa na nishati ya umeme Unguja na Pemba.

Naibu Waziri hiyo, Juma Makungu, alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi na kujibu swali la Mwakilishi wa Konde, Omar Seif Abeid, aliyetaka kujua juhudi za kuvipatia umeme baadhi ya vijijini katika jimbo lake zimefikia wapi hadi sasa.

Makungu alisema vijiji vyote vikubwa vilivyoko Unguja na Pemba vimepatiwa nishati ya umeme na vilivyosalia ni vitongoji vidogo vidogo ambavyo kazi ya kuviunganisha umeme imeanza katika mwaka wa fedha 2018/19.

Alisema katika mwaka wa fedha 2018/19 Shirika la Umeme Zanzibar (Zeco) linakusudia kuvifikia vitongoji 70 kwa kuviunganishia nishati hiyo na wananchi wake kufaidika na huduma hiyo.

Pia aliwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba kazi ya kusambaza umeme katika visiwa vidogo vidogo wanavyoishi watu huko Pemba inaendelea vizuri na tayari vitano kati ya hivyo wananchi wake wanafaidika na huduma ya umeme.

## Wajumbe baraza waipongeza SMT

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wameipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuipatia Zanzibar eneo la ardhi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za serikali jijini Dodoma ambako ni makao makuu ya serikali ya Muungano.

Hayo yalisemwa na Mwakilishi wa Mtoni, Hussein Ibrahim Makungu, alipokuwa akichangia taarifa ya serikali ya utekelezaji wa ahadi za wajumbe wa baraza iliyowasilishwa na Kaimu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Haroun Ali Suleiman katika Baraza la Wawakilishi.

Makungu alisema kitendo kilichofanywa na Serikali ya Muungano kuipatia eneo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kujenga ofisi za zerikali kinastahili kuigwa na mfano wa kuimarishwa kwa Muungano.

Alisema eneo ambalo Zanzibar imepewa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ni zuri likiwa tayari limefikiwa na huduma mbalimbali muhimu ikiwamo miundombinu ya umeme.

Mwakilishi huyo aliitaka serikali kuanza haraka kulifanyia kazi eneo hilo kwa matayarisho ya ujenzi wa majengo ya ofisi mbalimbali za serikali katika makao makuu ya nchi Dodoma.

"Sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tunaipongeza kwa dhati Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa kuchukua uamuzi wa haraka kuipatia Zanzibar eneo la ujenzi wa ofisi za serikali katika makao makuu ya nchi huko Dodoma. Ni uamuzi unaostahili kupongezwa wenye dhamira ya dhati ya kustawisha Muungano wetu," alisema.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Serikali, Panya Ali Abdalla, alisema kitendo kilichofanywa na Serikali ya Muungano kutoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za serikali ni dhamira ya dhati ya kudumisha Muungano.

Alizitaka mamlaka za serikali kuharakisha kuanza kulifanyia kazi eneo hilo ikiwamo kulizungusha uzio na kulipima tayari kwa ajili ya ujenzi.

"Sisi wajumbe wa kamati ya ofisi ya viongozi wakuu wa serikali tulipata nafasi ya kulitembelea eneo hilo na tumeridhishwa. Liko eneo zuri likiwa limefikiwa na miundombinu muhimu ikiwamo umeme," alisema.

Kamati ya ofisi ya viongozi wakuu wa serikali ilifanya ziara maalumu kutembelea mji wa Dodoma na kulikagua eneo ambalo Zanzibar imepewa kwa ajili ya kujenga ofisi za serikali.

# Waliovamiwa na tembo sasa wasaidiwa mahindi

**Na Happy Severine,** MEATU

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), imetoa msaada wa mahindi gunia mbili kwa kila familia zinazopakana na pori la akiba la Maswa katika Kata za Mwasengela na Tindabuliga wilayani Meatu mkoani Simiyu ambazo hivi karibuni zilivamiwa na tembo.

Tembo hao ambao wanatoka katika pori hilo walivamia jumla ya kaya 39 kutoka katika kata hizo na kuharibu nyumba kisha kula chakula chote ambacho kilikuwa kimehifadhiwa yakiwamo mahindi, mtama, mihogo, viazi pamoja na unga.

Akikabidhi msaada huo jana kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Dk. Joseph Chilongani, Meneja wa Pori hilo Lusato Masinde, alisema msaada huo unatokana na ahadi ya Kamishna Mkuu wa Uhifadhi kutoka Mamlaka hiyo, Dk. James Wakibara aliyoitoa Septemba 9, 2019 wakati alipotembelea familia hizo.

**Kamishna baada ya kuona uharibu ule kama binadamu aliona ni vyema mamlaka ikatoa msaada huu kama pole, lakini kuwasaidia wananchi ambao mazao yao yote yaliliwa, leo tutawakabidhi gunia mbili kila kaya ambazo ziko 39 zilizopatwa na janga hili.**

"Kamishna baada ya kuona uharibu ule kama binadamu aliona ni vyema mamlaka ikatoa msaada huu kama pole, lakini kuwasaidia wananchi ambao mazao yao yote yaliliwa, leo tutawakabidhi gunia mbili kila kaya ambazo ziko 39 zilizopatwa na janga hili," alisema Masinde.

Masinde alisema kuwa tembo hao walifanya uharibifu huo mwanzoni mwa mwezi huu, ambapo zaidi ya nyumba 39 ziliharibiwa huku akibainisha kuwa hapakuwapo na kifo cha mwananchi yeyote kilichotokea.

Alisema kilichofanywa na mamlaka hiyo kutoa msaada wa mahindi hayo siyo utaratibu wake, ila baada ya Kamishna Mkuu kuona hali hiyo aliwahurumia wananchi na kuona madhara yaliyotokea ni makubwa sana.

Meneja huyo aliwasisitiza wananchi wanaopakana na hifadhi hiyo kuendelea kuweka tahadhari juu ya wanyama hao ambao alieleza kutokana na uhifadhi wamekuwa wengi na wanavamia maeneo ya wananchi kila mara.

Diwani wa Tindabuligi, Antony Magembe, alisema tembo hao walikuwa wanavamia nyumba hizo kisha kutafuta chakula chochote kilichopo ndani na walipokuwa wanafanikiwa kukipata wanakula chote hadi kumaliza.

Mkuu wa Wilaya huyo aliushukuru uongozi wa Tawa kwa msaada huo ambao utawasaidia wananchi ambao walibaki bila chakula, huku akiwasisitiza kutumia vikundi vya vijana ambavyo vilipewa mafunzo ya jinsi gani ya kuwazuia wanyama hao ili wasiendelee kuleta madhara kwao.

Naye Lonzwe Kuhenda, mmoja wa wananchi hao kutoka Kata ya Mwasengela, aliishukuru serikali kwa msaada huo, huku akiomba kuongezewa kwa kuwa wanyama hao walikula chakula chao chote.



Mkurugenzi wa Biashara wa Benki ya DCB, James Ngaluko (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza kumalizika kwa kampeni ya bidhaa yake ya akaunti ya muda maalum ya 'DCB Lamba Kwanza', ambayo alisema imepata mafanikio makubwa na ikivuka lengo. Wengine (kutoka kushoto) ni Mkuu wa Idara ya Masoko, Rahma Mgassa, Mkurugenzi wa Wateja, Frederick Mwakitwange na Meneja wa DCB tawi la Magomeni, Fortunata Benedict. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# RC Gaguti: Walimu msiogope kukopa

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, amesema walimu nchini wana nafasi kubwa ya kushiriki kukuza uchumi wa viwanda kwa ajili ya kuanzisha miradi mbalimbali kwa kuwa ni kundi kubwa linalokopesheka.

Akifungua kongamano la walimu wa Mkoa huo maarufu kama 'Teachers Day', alisema hawana sababu ya kuogopa kukopa na kuanzisha miradi vikiwamo viwanda na kutoa fursa za ajira kwa makundi mengine kwenye jamii.

"Kama haukopi sahau kupata maendeleo, suala liwe unakopa wapi na kwa sababu zipi kupitia umoja wenu mnaweza hata kuanzisha viwanda vidogo vidogo na mkatoa ajira kwa wananchi kupitia biashara yenu," alisema Gaguti.

Alisisitiza kuwa sio jambo baya mwalimu kuwa ameajiriwa na serikali wakati huo akiwa na miradi ya kiuchumi na kuwataka waandae maandiko bora yatakayowawezesha kupata mikopo kwenye taasisi za fedha kama NMB.

"Ukiona umekosa mkopo kwenye taasisi za fedha fahamu kuwa tatizo lipo kwenye andiko lako la kuomba mkopo zipo fursa nyingi za kufanya biashara katika Mkoa wa Kagera na maeneo mengi nchini," aliongeza.

Aidha, aliwaomba walimu kutumia nafasi yao kutoa elimu ya ulipaji wa kodi katika maeneo yao akisema haridhishwi na mwamko uliopo mkoani Kagera ambapo watu wengi wanafanya manunuzi bila kuomba stakabadhi na kuwa chanzo cha serikali kukosa kodi.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Wateja Binafsi kutoka NMB, Omari Mtiga, alisema amesema benki hiyo imekuwa ikifanya maboresho mbalimbali kwa nyakati tofauti ikiwa ni pamoja na kupunguza viwango vya riba ya mikopo ambapo walimu ni miongoni mwa makundi yanayonufaika na fursa hizo.

# Mjadala wa haki kupata habari waibua mengi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

OFISA Mdhamini wa Wizara ya Katiba na Sheria, Mattar Zahor, amesema, upatikanaji wa habari kwa wananchi unasaidia kujua utekelezaji wa mipango ya nchi, hivyo kuwawezesha kuchangia mawazo katika utekelezaji bora wa mipango na kuwafanya wahoji.

Alisema haki ya kupata habari na kutoa maoni ni muhimu sana katika nchi, hivyo iwapo wananchi watanyimwa haki hizo kunasababisha migogoro ndani ya jamii na kupelekea kukosa maendeleo ndani ya nchi.

Akizungumza mjini Chackechake wakati akifungua mjadala wa wazi kuhusu Haki ya Kupata Habari, Uhuru wa Kujieleza, Uhuru wa Kujiunga na Kujikusanya, mdhamini huyo alisema upatikanaji wa haki kunajenga msingi imara wa demokrasia.

"Serikali yetu siku zote imekuwa ikifanya jitihada za kuhakikisha demokrasia inaimarika katika nchi yetu kwa kuendelea kuimarisha misingi yake ikiwamo upatikanaji wa haki za binadamu, ambapo katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 imeeleza," alisema.

Aliwataka viongozi wa serikali na mashirika ya umma kujenga ushirikiano na waandishi wa habari kwa kuwapa taarifa, ili jamii ipate habari na kutoa maoni yao, jambo ambalo linalenga katika mtazamo wa kuleta mabadiliko na maendeleo katika nchi.

Akizungumzia haki ya kujiunga na kujikusanya, alielezea kuwa, pia ni haki za msingi kwa mustakbali wa taifa lolote, kwa lengo la kuelezea kero na shida zinazolikabili taifa au kundi fulani.

"Lakini tunaposema haki ya kujikusanya, hatumaanishi lazima iwe maandamano na mikutano isiyo na tija au fujo, kwani hata huu mkutano wa leo tunatimiza uhuru wa kujikusanya, lakini kwa tija maana tunatoa tathmini yetu kuhusu utekelezaji na upatikanaji wa baadhi ya haki za binadamu kwa maendeleo yetu," alisema.

Akiwasilisha mada ya Haki ya Kupata Habari na Kutoa Maoni Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Pemba, Said Mohamed Ali, alisema, habari zinaleta mabadiliko kwa jamii kwani zinaelimisha, hivyo si vyema kwa viongozi kukataa kutoa taarifa kwa waandishi.

Mwanasheria wa dhamana kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) Mkoa wa Kusini Pemba, Ali Rajab Ali, akiwasilisha mada ya haki ya kujikusanya na kujiunga, alisema waangalie sheria wakati wanapotekeleza haki hizo, ili kuepusha migogoro kwani zinahitaji umakini mkubwa zinapotekelezwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Huduma za Sheria Pemba, Safia Saleh Sultan, alisema kituo hicho kinatoa huduma za msaada wa kisheria bure.

Washiriki hao walisema hakuna uhuru wa kutosha wa habari na ndio maana waandishi wanashindwa kufichua madudu yaliyojificha.

## HABARI KIMATAIFA

## Watu 500 mbaroni wakihusishwa na vurugu

**CAIRO, Misri**

WATU zaidi ya 500 wamekamatwa katika maeneo mbalimbali nchini Misri kwa kipindi cha siku kadhaa zilizopita, wakati wa maandamano dhidi ya Rais wa nchi hiyo, Abdel Fattah al-Sisi.

Watetezi wa haki za binandamu wametoa takwimu hizo kutokana na maandamano yaliyofanyika siku ya Ijumaa na Jumamosi iliyopita jijini Cairo na maeneo mengine ya nchi hiyo.

Miongoni mwa watu waliokamatwa ni mwanaharakati maarufu Mahienour el-Massry aliyewahi kushinda tuzo ya Kimataifa.

Maofisa wa usalama wanamshutumu el Massry kuwa mwanachama wa kundi la kigaidi lakini pia kuhusika na uchapishaji wa habari za uongo.

Waandamanaji nchini Misri wakati wa maandamano hayo, walikuwa wanalalamikia kuendelea kuteswa kwa wapinzani wa Rais el Sisi, na kuzuiwa kushiriki katika maandamano dhidi ya utawala wake.

Maandamano nchini Misri, yamepigwa marufuku nchini Misri tangu mwaka 2013 wakati Rais wa zamani wa nchi hiyo, Mohammed Morsi alipoondolewa madarakani

RFI

**Maofisa wa usalama wanamshutumu el Massry kuwa mwanachama wa kundi la kigaidi lakini pia kuhusika na uchapishaji wa habari za uongo.**

# Kiongozi wa upinzani Rwanda auawa kikatili

**KIGALI, Rwanda**

MWANASIASA maarufu wa upinzani nchini Rwanda, Syridio Dusabumuremyi ameuawa kwa kuchomwa kisu. Uongozi wa chama chake cha FDU-Inkingi umethibitisha.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na kiongozi wa chama hicho, Victoire Ingabire, Dusabumuremyi alikuwa kazini wakati aliposhambuliwa na wanaume wawili.

Dusabumuremyi ambaye ni baba ya watoto wawili alikuwa katika duka lake la kuuza chakula katika kituo cha afya wilaya ya kati ya Muhanga.

Idara ya upelelezi nchini Rwanda imetuma ujumbe katika mtandao wa kijamii wa twitter kueleza kwamba imewakamata washukiwa wawili wanaotuhumiwa kuhusika na mauaji ya Dusabumuremyi.

Katika ujumbe huo, idara hiyo imeeleza kwamba Dusabumuremyi alichomwa kisu hadi kufa na watu wasiojulikana, aliuawa akiwa kazini katika kituo cha afya wilayani ya Muhanga.

Ilieleza kwamba katika uchunguzi wa awali, washukiwa wawili wamekamatwa kwa kuhusika na mauaji hayo na kwamba uchunguzi bado unaendelea kubaini dhamira ya mauaji hayo.

Ingabire alieleza kuwa mauaji ya Dusabumuremyi ni mwendelezo wa matukio ya mauaji dhidi ya wafuasi wa chama chake kwa lengo la kuwatishia.

Miezi miwili iliyopita, Eugène Ndereyimana, mwakilishi wa chama cha FDU-Inkingi kutoka eneo la mashariki mwa Rwanda alitoweka. Mpaka sasa hajapatikana

Machi, mwaka huu msemaji wa chama hicho, Anselme Mutuyimana, alitekwa na baadaye kukutwa amefariki msituni magharibi mwa nchi hiyo.

Machi, 2016, mwanachama wa FDU-Inkingi, Jean Damascène Habarugira aliuawa.

Ingabire, ambaye ni mkosoaji mkubwa wa Rais Paul Kagame, alisema chama chake kinalengwa kwasababu kinapania kutetea haki za raia wa Rwanda na uhuru wao.

"Lengo letu ni zuri na hatutaacha kulipigania hata wakafanya lolote," alisema Ingabire.

Ingabire alizaliwa oktoba 3, 1968. Ni mke na mama wa watoto watatu. Alisomea Sheria na masuala ya uhasibu na hatimaye kufuzu kwa shahada ya uchumi na biashara nchini Uholanzi.

Tangu mwaka 1997, Ingabire amekuwa akijihusisha na harakati za upinzani nchini Rwanda akiwa mafichoni Uholanzi.

Aliteuliwa na muungano wa kundi la viongozi wa upinzani ambao una wanachama nchini Rwanda, barani Ulaya, Marekani na Canada.

Januari 2010, Ingabire alirejea Rwanda kutoka mafichoni nchini Uholanzi baada ya kutajwa kuhusika kwenye mauaji ya kimbari ya mwaka 1994, ili kugombea uchaguzi wa urais. Alikamatwa na kuzuiliwa kuwania urais.

Ingabire, ni mwanachama wa jamii ya Wahutu na alihoji kwa nini makumbusho rasmi ya mauaji ya kimbari ya mwaka 1994 nchini Rwanda hayakujumuisha Mhutu yeyote

Ingabire alikamatwa na hatimae kufungwa jela miaka 15 kwa makosa ya ugaidi pamoja na kuhatarisha usalama wa kitaifa.

Hata hivyo, sasa yuko huru baada ya kupewa msamaha na Rais Kagame.

*BBC*




Askari wa Burkina Faso wakiwa katika doria ya ukaguzi mjini Ouagadougou. **PICHA: REUTERS**

# Mahakama yatengua amri ya Waziri Mkuu

**LONDON, Uingereza**

UAMUZI uliochukuliwa na Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson kusitisha bunge ulikuwa kinyume na sheria, mahakama ya juu zaidi nchini humo imeamua.

Johnson alisitisha vikao vya bunge kwa wiki tano mwanzoni ma mwezi huu, lakini mahakama imesema ilikuwa ni makosa kuwasitisha wabunge kuendelea na majukumu yao kuelekea Brexit Oktoba 31.

Spika wa Bunge la wawakilishi, John Bercow, alisema wabunge watarudi kwenye vikao Jumatano baada ya uamuzi huo wa kihistoria.

Rais wa mahakama ya juu zaidi, Lady Hale alisema athari za msingi wa demokrasia zilivuka mpaka. Sehemu ya wabunge wanashinikiza Waziri Mkuu ajiuzulu

Johnson alitaka bunge lisitishe vikao kabla ya hotuba ya Malkia ili aweze kueleza bayana sera zake mpya za serikali.

Lakini wakosoaji wanasema alikuwa anajaribu kusitisha wabunge kuchambua mipango yake ya Brexit na hatua hiyo ya kusitisha vikao ilikuwa ndefu kusubiria hotuba ya Malkia.

Akisoma uamuzi huo rais wa mahakama hiyo ya juu zaidi, Lady Hale, amesema: "Uamuzi wa kumshauri Malkia kusitisha bunge ulikwenda kinyume na sheria kwa sababu iliweza kuchangia kutatiza au kusitisha uwezo wa bunge kuendelea na majukumu yake kikatiba bila ya kuwapo kwa sababu ya maana."

Hale alisema uamuzi huo wa pamoja wa majaji 11 unamaanisha kuwa bunge halijasitishwa- Uamuzi huo hauna athari yoyote.

Spika Bercow alisema wabunge wanahitaji kurudi kufuatia uamuzi huo na aliagiza maafisa wa bunge la wawakilishi kutayarisha .. kurudi kuendelea kwa vikao vya bunge kuanzia majira ya saa 11:30 BST siku yaJumatano.

Mahakama pia imeshutumu muda wa kusitishwa vikao hivyo, huku Hale akisema haiwezekani kusitishwa kutokana na ushahidi uliowasilishwa mahakamani, kwamba hakukuwa na sababu yoyote ya kumshauri Malkia kusitisha vikao vya bunge kwa wiki tano".

Akizungumza nje ya mahakama, Miller alisema uamuzi huo unatoa ujumbe mkubwa.

"Waziri mkuu huyu ni lazima afungue milango ya bunge kesho. NI lazima wabunge warudi na wawe wakakamavu katika kuiwajibisha serikali," alisema Miller.

Mwanachama wa SNP, Joanna Cherry, aliyeongoza kesi ya Uskotchi alimtaka Johnson ajiuzulu kufuatia uamuzi huu.

"Mahakama ya juu zaidi Uingereza imeamua kwa pamoja kuwa ushauri wake wa kusitisha bunge, ushauri wake kwa malkia, ni kinyume na sheria,"alisema Cherry.

*BBC*

# Agizo la Lugola kamata vibaka lazua hofu kubwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

AGIZO la Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola kwa Mkuu wa Polisi Wilaya ya Dodoma, kutokomeza vibaka katika mtaa wa Chang'ombe, limezua hofu kwa wakazi wa mtaa huo kushindwa kufanya shughuli zao.

Hofu hiyo inatokana na kamata kamata ya makundi ya vijana.

Mwishoni mwa wiki Lugola katika bonanza lililoandaliwa na Jumuiya ya Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) alimpa siku tatu OCD ahakikishe awe amempa mpango mkakati lini atatokomeza vibaka katika mtaa huo.

Akizungumzia na gazeti hili, Diwani wa kata hiyo, Samuel Fundikira, alisema karandinga la polisi limekuwa likizunguka na kukamata watu wanaodaiwa ni vibaka, na kuwa hali hiyo imezua hofu kwa wakazi wa eneo hilo.

Alisema kamata kamata hiyo imeathiri kwa kiasi kikubwa wakazi wa eneo hilo kutokana na kushindwa kufanya kazi kwa kuhofia kukamatwa na askari.

Alisema gari hilo limekuwa likisimama baadhi ya maeneo na kukamata makundi ya vijana na kuwaweka ndani, wakiwamo wasio wahalifu.

Alieleza kuwa msako unaofanywa ni mzuri, lakini ni vema wakatumia mbinu za kiaskari kuliko kuwakamata ovyo raia wa eneo hilo na kuwekwa ndani ilhali wengine sio vibaka.

"Naomba askari watafute mbinu za kuwakamata watu wanaowashuku ni vibaka kwa sababu taaluma hiyo wameisomea na wanajua jinsi ya kumbana kibaka au mhalifu," alisema Fundikira.

Aliongeza: "Wakiendelea na zoezi la kukamata makundi ya watu bila kutofautisha nani ni kibaka watachangia kuathiri maendeleo ya wakazi wa eneo hili, kwa sababu vijana wengi wanaogopa kutoka kuendesha shughuli zao za kila siku za kuwaingizia kipato hususani waendesha bodaboda kwa kuhofia kuwekwa ndani."

Diwani Fundikira alieleza kuwa katika bonanza hilo Waziri Lugola alipokea malalamiko ya kuwapo vibaka na baadhi ya askari wanaotuhumiwa kulichafua Jeshi la Polisi kutokana na kuhusishwa na kupokea rushwa.

Baadhi ya wakazi wa eneo la Chang'ombe, walisema ukamataji unaofanywa sio sahihi kwa sababu unawapa hofu na kushindwa kufanya shughuli zao.

"Ikifika saa mbili au saa tatu hapa hata kama unatoka dukani ukikutwa unatembea barabarani unakamatwa, kama wewe ni mfanyakazi kitakachokuokoa ni kitambulisho chako, lakini kama hujatembea nacho unapandishwa kwenye gari la polisi," alisema mmoja wa wakazi hao.

Hata hivyo, jitihada za kumtafuta Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Gilles Muroto, kuzungumzia suala hilo, aliombwa kutumiwa ujumbe mfupi wa simu (sms), lakini hadi gazeti hili linaenda mitamboni hakujibu na simu yake ilita bila majibu.



Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, Liberat Sabas (wa pili kushoto) na Ofisa Fedha Mkuu wa Benki ya NBC, Waziri Barnabas, wakibadilishana hati za makubaliano ya ulinzi wa askari wa jeshi hilo katika matawi yote NBC nchini. Hafla hiyo ilifanyika jijini Dar es Salaam jana. Wanaoshuhudia kutoka kushoto ni Mkuu wa Kitengo cha Sheria, Kamishna Mwandamizi wa Polisi, Gustavus Babile, Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa NBC, Doxa Mbapila na Ofisa Mwendeshaji Mkuu wa NBC, Alelio Lowassa. **MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aagiza kung'olewa milango kituo cha afya

**Na Josephine Majura, KONDOA**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Ashatu Kijaji, amemwagiza Kaimu Mhandisi wa Wilaya ya Kondoa, Felcitism Tesha, kung'oa milango yote katika Kituo cha Afya Busi kutokana na kutokuwa na viwango.

Dk. Kijaji alitoa agizo hilo jana alipofanya ziara ya kikazi katika Kijiji cha Busi wilayani Kondoa kukagua utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa vituo vya afya vinavyojengwa kwa fedha za serikali.

Kijaji ambaye ni Mbunge wa Kondoa Vijijini, alisema hajaridhishwa na milango iliyowekwa katika kituo hicho kwa kuwa ubora wake hauendani na thamani ya fedha iliyotolewa kwa ajili ya kazi hiyo.

Alisema fedha iliyotengwa kwa ajili ya milango hiyo ni kubwa zaidi ya milango inavyoonekana, hali inayosababisha kuhatarisha usalama wa wagonjwa na watumishi wa kituo hicho.

"Ninaagiza milango yote iliyowekwa ikiwa chini ya kiwango ibadilishwe kwa gharama za fundi aliyepewa tenda hiyo bila kutumia hata shilingi moja ya serikali. Milango haina hata mwaka imeanza kupasuka?" alihoji.

Pia aliutaka uongozi wa wilaya kwa kushirikiana na Kamati ya Ujenzi ya Kijiji hicho kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kikamilifu katika kusimamia miradi mbalimbali ya maendeleo inayofadhiliwa na serikali ili kubaini upungufu na kufanyia kazi mapema.

Naye Kaimu Mhandisi wa Wilaya, Tesha, alimwahidi Dk. Kijaji kwamba atatekeleza agizo hilo na kuhakikisha milango hiyo inabadilishwa haraka kabla ya kuleta madhara kwa wagonjwa na watu wengine katika kituo hicho.

# Elimu ya juu waelezwa dawa rushwa ya ngono

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

WANAFUNZI wa Taasisi za elimu ya juu nchini wametakiwa kutoa ushirikiano kukabiliana na changamoto ya rushwa ya ngono vyuoni kwa kukubali kutoa ushahidi wa vitendo hivyo kwa mamlaka mbalimbali.

Miongoni mwa mamlaka hizo ni za ushauri za wanafunzi au Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), na kwamba suala la usiri litazingatiwa katika ufuatiliaji bila kusababisha madhara yeyote ya kitaaluma.

Hayo yalielezwa na Msemaji wa chama cha washauri wa wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu nchini (TACOGA 1984), Nicholaus Ngowi, ambaye pia ni mshauri wa wanafunzi toka Chuo cha Mipango Mwanza, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, baada ya washauri hao kutoka Tanzania Bara na Visiwani, kukutana katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, mkoani Morogoro.

Alisema suala la rushwa ya ngono ni kosa la jinai ambalo kiutaratibu linashughulikiwa na mahakama, lakini wao kama washauri jukumu lao ni kutoa mafunzo juu ya madhara ya rushwa ya ngono kwa wanafunzi na kwa wafanyakazi wa taasisi ya elimu ya juu, lakini pia kutoa ushauri nasaha kwa wafanyakazi, washauri wa wanafunzi na wanafunzi wenyewe.

"Sisi wajibu wetu, kwanza tunakemea rushwa ya ngono, sio kwa washauri tu na wote wanaofanya kazi katika taasisi ya elimu ya juu, kwamba sisi ni walezi na tumekuwa tukiwakumbusha wanachama wetu na kuwaendeshea mafunzo, pia tumekuwa tukifanya kazi kwa karibu sana na Takukuru na tumewajengea uwezo viongozi wa Serikali za wanafunzi ili nao wawajulishe wanafunzi wengine ili ikitokea hali kama hiyo wawe tayari kuripoti na kutoa ushahidi kwenye mamlaka husika," alisisitiza Ngowi.

Aliongeza kuwa ofisi za washauri wa wanafunzi zimekuwa zikikutana na mambo mengi, hivyo kuwahakikishia Watanzania kuwa washauri wengi waliopo wana uwezo wa kutunza siri na kuripoti matukio katika mamlaka husika bila mwanafunzi kupata madhara yoyote ya kitaaluma.

Alisema taasisi zote za elimu ya juu pia zina mamlaka za rufani katika matokeo, hivyo anayedhani amefelishwa kwa sababu ya kuripoti matukio ya rushwa ya ngono, ana nafasi ya kukata rufani na mitihani yake itapitiwa na jopo la watu mbalimbali na haki ya mhusika itaweza kupatikana.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Prof. Lugano Kusiluka, alisema kwa muda mrefu eneo la ushauri nasaha na mwongozo bado halina wataalamu wengi kwa kuwa ni eneo jipya, lakini masuala yanayohitaji ushauri na mwongozo yanaongezeka kwa kasi kubwa sana ikilinganishwa na kasi ya kuzalisha wataalamu wa eneo hilo, hivyo washauri hao watambue jukumu na mzigo mkubwa ulio mbele yao.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA KADI

Anaitwa **SAID JUMA ISSA** Amepotelewa na kadi ya pikipiki aina ya HAOJUE yenye namba za usajili MC 611 BXH. Yenye chassis namba LC6PCJK26J0006005 na engine namba 156FMI5AD2F32758.

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi Taarifa : MOR/MOR/RB/327170/2019.

215431702

## MAGARI YANAUZWA

Kampuni ya PROSHARE CAPITAL LTD inauza magari yafuatayo: MASUMA MISAM FAZAL gari No.T 464 BUT VOLVO. NIYAGIRA M. RUSIBAMAYILA gari No.T 865 CZD TOYOTA VANGUARD. ABDALLAH SALIM AHMED gari No.T 822 DPT TRACTOR.

Kwa mawasiliano piga No. 0714 842935.

115431802

## KUPOTEA KWA PASIPOTI



**AMOS EPIMACK NYANDA**
Mtajwa hapo juu anatangaza kupotelewa na passport yenye namba **AB 809773** iliyotolewa na **PCO DAR ES SALAAM.** Imetolewa Tarehe 04 Jun 2016 na inaisha muda wake tarehe 03 Jun 2026.

Kwa yeyote atakae iona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kwa

**Kumb:MIS/RB/2325/2019.**

115431902

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA TARIME**

**MAOMBI NA. 36/2018**

**ELIAS MESHACK.........MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**MARWA MESHACK.........MJIBU MAOMBI**

Mdaiwa MARWA MESHACK popote ulipo,

Fahamu kwamba mleta maombi ELIAS MESHACK alileta maombi Na. 36/2018 dhidi yako na maombi kusikilizwa upande wa mleta maombi na kubaki upande wa mdaiwa kusikilizwa.

Hivyo basi kama unakusudia kutoa ushahidi wako unatakiwa uwepo Barazani wewe binafsi, wakili wako au mwakilishi anayekubalika kisheria tarehe 30/09/2019 siku ambayo shauri limepangwa kusikilizwa upande wa mjibu maombi.

Endapo hautatekeleza hayo shauri litaendelea kwa kutolewa amri sitahiki kama ipasavyo kisheria.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 04/09/2019.

115432002

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACQUELINE EZRON MAGORI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.0748/0002** kilichotolewa na KAWAWA SEKONDARI mwaka 2003.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **CD/RB/11187/2016.**

115430702


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*


## VYETI VIMEPOTEA



**JAMES A. MPONDA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P1081-0036** kilichotolewa na WAMO SEKONDARI mwaka 2004. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0310-0591** kilichotolewa na FOREST HILL SEKONDARI mwaka 2007. Cheti cha Ualimu Diploma chenye namba **E0506-0152** kilichotolewa na MARANGU TTC mwaka 2011.Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/KIJ/RB/284580/2019.**

115430502

**JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA
23/09/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya jumatano tarehe **25/09/2019** kampuni ya **Builders &Limeworks Co. Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **SAME** kuelekea **ARUSHA,** gari hilo lenye namba za usajili **T170BAP/ T515 ALG**

2. Gari hilo linavipimo vifuatavyo:

**Urefu...................17.0m**
**Upana...................3.5m**
**Kimo....................4.55m**

3. Njia itakayotumika: **SAME hadi ARUSHA** Kupitia KIA, gari litasafiri muda wa mchana tu *(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)*

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

115430602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI


**ALFRED AMNAWE MWAGENI** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari iliyokuwa na namba ya usajili T 963 CQL yenye chasis namba FE 315BD490618 na injini namba 4D32110045.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Taarifa ya Polisi: **IR/TR/RB/2506/2019.**

115431202

## KUPOTEA KWA CHETI



**Jofrey Laban Hosea** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4053/0065 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika Shule ya Sekondari Nyumba ya Mungu.

Yeyote atakekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **DAR/MB/RB/320063/2019**

215430902


**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Nipashe



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# EMERY: JUKUMU PENALTI ARSENAL LA AUBAMEYANG

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI Pierre-Emerick Aubameyang ataendelea kuwa chaguo la kwanza katika upigaji wa mikwaju wa penalti, kwenye kikosi cha Arsenal licha ya kutofanya hivyo wakati wa mchezo wa ligi dhidi ya Aston Villa, Jumapili.

Arsenal walipata ushindi wa mabao 3-2 na bao lao la kwanza lilifungwa kwa njia ya penalti na mshambuliaji kutoka nchini Ivory Coast, Nicolas Pepe.

Kocha wa 'Washika Bunduki' hao, Emery amesema maamuzi ya nani alipaswa apige penalti katika mchezo huo yalitolewa na Aubameyang, kwa kumkabidhi Pepe ambaye alifanikiwa kufunga bao la kusawazisha.

Alisema yeye kama kocha tayari ameshafanya maamuzi ya kumkabidhi jukumu Aubameyang la kuhakikisha anapiga mikwaju yote ya penalti inayotokea kwenye mchezo, na inapotokea jukumu hilo kapewa mtu mwingine hawezi kuingilia.

"Sijaona tatizo lolote kwa wachezaji wangu kukubaliana, Aubameyang ndiye mwenye jukumu la kupiga penalti, lakini kama aliridhia Pepe apige ni sawa.

"Nimeona hakuna kilichoharibika, na Pepe alipiga vizuri na tukafanikiwa kupata bao la kusawazisha.

"Kila mmoja kikosini anajua Aubameyang ndiye chaguo la kwanza, na hakuna ambaye atalidharau hilo," alisema kocha huyo kutoka nchini Hispania.

# UNITED YAWAONDOA HOFU MASHABIKI

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imewahakikishia mashabiki wake kwamba, klabu itaendelea "kupigania mataji kwa kiwango cha juu" na mafanikio uwanjani yatakuja huku wakitengeneza fedha.

United, ambayo ilipoteza kwa mabao 2-0 kutoka kwa West Ham Jumapili, ilishinda taji lake la 20 la Ligi Kuu mwaka 2013 na kwa kipindi cha misimu sita imekuwa ikishutumiwa kwa kukosa mafanikio.

Lakini jukwaa la mashabiki wa timu hiyo kupitia kwenye mitandao ya kijamii, mapema wiki hii limeonyesha kutorizishwa na mwenendo wa kikosi hicho, huku wakisema klabu hiyo inakwenda njia tofauti.

"Kila mmoja klabuni, kuanzia wamiliki, wamejikita katika kuhakikisha timu inashinda mataji," alisema msemaji wa United akinukuliwa na magazeti ya Uingereza wakati akilijibu jukwaa hilo la mashabiki damu wa 'Mashetani Wekundu hao.

"Kwa kufanya hivyo, tumewekeza vizuri zaidi kwa kikosi kinachocheza na tutaendelea kufanya hivyo.



"Wakati huo huo, wachezaji vijana na wenye vipaji wanaendelea kuja kutoka katika akademi yetu na hii itaongeza hamasa zaidi kwa timu yetu.

"Lazima ieleweke kwamba, wakati tukiendelea kutafuta mafanikio ya klabu uwanjani, lakini pia mapato yetu ya timu yanaimarika kutokana na uwekezaji tuliofanya."

Aidha, United imedokeza kwamba, bado inaendelea kutafuta mkurugenzi mpya wa soka ambaye ataendana na mahitaji ya klabu hiyo.

# UJUMBE WA SILVA KWENDA KWA MENDY WACHUNGUZWA

**LONDON, England**

UJUMBE kupitia mtandao wa Twitter uliotumwa na Bernardo Silva kwa mchezaji mwenzake wa timu ya Manchester City, Benjamin Mendy unachunguzwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), kwa kutuhumiwa kuwa wa kibaguzi.

Mchezaji huyo wa timu ya Taifa ya Ureno, Silva alimlinganisha Mendy na kibonzo cha rangi ya chokoleti kwenye pakiti ya pipi ya Conguitos - zinazopatikana nchini Hispania na Ureno.

Ujumbe huo uliwekwa Jumapili majira ya saa 8:45 mchana na ukafutwa saa moja baadaye.

Baada ya hapo Bernardo alituma ujumbe mwingine kwenye twitter akisema: "Huwezi hata kufanya mzaha siku hizi na rafiki yako."

Mashabiki walijibu kwa kutaka ujumbe huo ufutwe.

Mmoja aliandika, "Mshikaji, amekutusi kwa ubaguzi wa rangi." Mwingine aliandika:"Bernado Silva ameandika ujumbe gani?"



Mchezaji wa timu ya Taifa ya Ufaransa Mendy na Silva ni marafiki wa karibu na wameichezea Monaco kwa pamoja kabla ya wote kujiunga na Man City mwaka 2017.

Mendy alijibu ujumbe huo na hakuonekana kuhisi vibaya.

Hata hiyo, Man City imekataa kutoa tamko lolote kuhusu ujumbe huo.

FA litaukagua ujumbe huo na kwa nini uliandikwa hadharani kabla ya kutangaza hatua watakayochukua.

# VAN DIJK:

## HAPANA SIWEZI KUJILINGANISHA NA MESSI




**MILAN, Italia**

NYOTA wa Liverpool, Virgil van Dijk amesisitiza kwamba hawezi kujilinganisha na Lionel Messi, huku akikanusha taarifa kwamba amekatishwa tamaa kwa kushindwa kutwaa tuzo ya Fifa ya mchezaji bora wa mwaka.

Van Dijk alimaliza nafasi ya pili nyuma ya nyota wa Barcelona, Messi katika kuwania tuzo hiyo Jumatatu, huku mkali wa Juventus na Ureno, Cristiano Ronaldo akimaliza nafasi ya tatu.

Beki huyo wa kati amesema hakukuwa na namna ya yeye kujilinganisha na Messi, ambaye alifunga mabao 51 kwenye mashindano yote msimu wa 2018-19.

"Watu wanaopiga kura wamefanya maamuzi na unatakiwa kuyakubali," alisema Van Dijk akiwaambia waandishi wa habari.

"Hili ni kama kwa wachezaji, huwezi kunilinganisha mimi na Messi kwa sababu tuko tofauti. Najisikia fahari kuwa hapa."

Van Dijk aliisaidia Liverpool kushinda taji la Ligi ya Mabingwa msimu uliopita, huku wakishindwa na Manchester City kwa pointi moja kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya England.

Lakini Van Dijk ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Uholanzi, akiwa ametajwa kwenye kikosi bora cha FIFA, akaongeza kusema kwamba, hana tatizo kwa Messi kutwaa tuzo hiyo na wala hajakatishwa tamaa.

"Kukatishwa tamaa? Huwezi kuhuzunika kwa hili," alisema.

"Nina furaha kuwa hapa, kuwa kwenye kikosi bora cha mwaka, baada ya kazi nzuri na ngumu."

# Neymar: Kiwango PSG kinaimarika

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR anaamini kwamba, ushindi wa Jumapili wa bao 1-0 ugenini dhidi ya Lyon unaonyesha namna gani kiwango cha Paris Saint-Germain kinavyoendelea kuimarika.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil aliendelea kuwashawishi mashabiki wa klabu hiyo kwa kumfunga Anthony Lopes dakika ya 87 na kuifanya PSG kuondoka na ushindi.

Ulikuwa ni ushindi wa pili ndani ya wiki, na Neymar ameonyesha kuwa na hamasa kubwa kwa kiwango cha timu yake.

Ushindi huo wa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, umekuja ikiwa imetoka kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Ilikuwa mechi ngumu," alisema Neymar mara baada ya mchezo huo dhidi ya kikosi hicho cha kocha, Sylvinho.

"Lyon ni timu imara. Walijilinda vizuri na walicheza kwa hatari kubwa na kutengeneza mashambulizi ya hatari.

"Kila mchezo tumeonekana kuimarika. Kwa uhakika kabisa tulicheza vizuri."

Neymar sasa amefunga mabao mawili katika mechi mbili tangu aliporudi kwenye kikosi hicho cha kocha Thomas Tuchel baada ya kipindi cha uvumi mwingine kuhusu majaliwa yake.




# Mount apandisha 'mzuka' Chelsea

**LONDON, England**

MASON Mount amesisitiza Chelsea imebakia kuwa imara wakati wakijiandaa kutafuta ushindi kwenye mechi zinazokuja wiki hii dhidi ya Grimsby Town na Brighton and Hove Albion.

Kikosi hicho cha kocha, Frank Lampard kilichapwa mabao 2-1 na Liverpool Jumapili, na kufanya kuwa mchezo wa nne kuchezwa kwenye dimba la Stamford Bridge msimu huu bila ushindi.

Blues hao licha ya kupata bao la kufutia machozi kutoka kwa N'Golo Kante, lakini halikutosha kuwafanya waondoke na pointi tatu.

"Tunapitia kipindi kigumu na pale tunapofanya makosa tunaadhibiwa," alisema Mount. "Nafikiri mara zote tunatakiwa kubakia tumetulia.

"Akili yetu imetulia baada ya mchezo, tunachokiangalia sasa ni mechi zetu mbili zinazofuata nyumbani na tunatakiwa kushinda.

"Ni mechi ngumu, lakini nafikiri kama ukipata ushindi wa kwanza nyumbani na kuetengeneza kasi ile ile, tunaweza kushinda, na nina matumaini tunaweza kufanya hivyo.

"Nafikiri hata mashabiki walioangalia mpira waliona namna gani mchezo ulivyokuwa na kwa jinsi tuliyocheza kwa kujituma kuhakikisha tunapata matokeo.

"Pengine wanaweza kuelewa jinsi hali ya mchezo ulivyokuwa na naamini kuna kitu fulani tutafanya kwa ajili ya mechi zinazofuata."

# DON A SOKA
## MAGAZ A ULAYA




# MESSI APINGWA TUZO FIFA, VAN DIJK ATAJWA

**Kama kocha wake Klopp, ametwaa tuzo ya Kocha Bora wa Mwaka, inawezekanaje mchezaji wake asipate tuzo ya...**

**MILAN, Italia**

NYOTA wa Barcelona, Lionel Messi amewapiku beki wa Liverpool, Virgil van Dijk aliyeshika nafasi ya pili na mshambuliaji wa Juventus, Cristiano Ronaldo [nafasi ya tatu], hivyo kutwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia (Fifa) kwa mwaka 2019, lakini hata hivyo baadhi ya wachambulizi wa soka hawakuridhishwa na matokeo hayo.

Moja ya sifa kubwa iliyombebesha tuzo hiyo, mshambuliaji huyo wa Barcelona ni pamoja na kufunga mabao mengi zaidi kwenye ligi kuliko mchezaji yeyote Ulaya kwa msimu uliopita, akifumania nyavu mara 36 wakati akiisaidia timu yake kutwaa ubingwa wa La Liga na katika mashindano yote msimu wa 2018-19, akitupia mara 51.

Aidha, kwa upande wa wanawake Megan Rapinoe wa Marekani ametwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Fifa akimpiku mchezaji mwenza, Alex Morgan na nyota wa England, Lucy Bronze.

Wakati Van Dijk akigaragazwa na Messi, kocha wake Jurgen Klopp ametwaa tuzo ya Kocha Bora mwa Mwaka wa Fifa kwa upande wa wanaume akimbwaga Pep Guardiola wa Manchester City, huku pia kipa wa Liverpool, Alisson Becker akitwaa tuzo ya Kipa Bora wa Mwaka wa Fifa.

Mchambuzi wa soka England na mchezaji na kocha wa zamani, Paul Merson, yeye anaamini Van Dijk alipaswa kutwaa tuzo hiyo kwa upande wa wanaume.

Alifafanua: "Messi amefanya kile anachokifanya kila msimu, hajaweza kuifikisha Barcelona ngazi tofauti na kuweza kutwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. Unashinda kwa sababu ya kufanya kitu fulani cha kipekee, ambacho kwa Van Dijk alikifanya.

"Messi ameshinda tuzo hiyo kwa sababu walianza [tuzo] mwaka 2016, na kwa miaka miwili ya kwanza, Cristiano Ronaldo alishinda na mwaka jana, Luka Modric akashinda. Sasa lazima wampe Messi.

"Nini afanye Van Dijk? Ameipeleka Uholanzi fainali ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya na ameipeleka Liverpool ngazi tofauti. Kama kocha wake ametwaa tuzo ya Kocha Bora wa Mwaka, inawezekanaje mchezaji wake asipate tuzo ya Mchezaji Bora? Yote ni juu ya wakati huu na anapaswa kushinda. "

Tuzo hiyo ni mara ya sita kwa Messi mwenye umri wa miaka 32 kuitwaa, ambapo sasa inamfanya kumzidi mara moja mpinzani wake Ronaldo, kuitwaa.

Wawili hao wamepokezana tuzo hiyo tangu mwaka 2008, na utawala wao ulitibuliwa na Luka Modric mwaka jana.

Katika kinyang'anyiro hicho, Messi alimpigia kura Sadio Mane, Ronaldo na Frenkie de Jong wakati Van Dijk kura yake ilikwenda kwa Messi, Mohamed Salah na Mane, huku Ronaldo yeye akimpigia Matthijs de Ligt, Frenkie de Jong na Kylian Mbappe.

Alisson ambaye pia ametajwa katika kikosi Bora cha Fifa, mbali na kuibebesha Liverpool taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, aliiongoza Brazil kutwaa ubingwa wa Copa America.

Wengine wanaounda kikosi Bora cha Fifa kwa upande wa safu ya ulinzi ni Matthijs de Ligt (Uholanzi, Juventus), Sergio Ramos (Hispania, Real Madrid), Virgil van Dijk (Uholanzi, Liverpool) na Marcelo (Brazil, Real Madrid).

Viungo ni Luka Modric (Croatia, Real Madrid), Frenkie de Jong (Uholanzi, Ajax) na Eden Hazard (Ubelgiji, Real Madrid).

Wakati washambuliaji wakiwa ni Kylian Mbappe (Ufaransa, Paris Saint-Germain), Lionel Messi (Argentina, Barcelona) na Cristiano Ronaldo (Ureno, Juventus).

## KWA UFUPI

**STERLING AFUKUZIWA MADRID**

Real Madrid inafuatilia mustakabali wa baadaye wa mshambuliaji wa Manchester City na England, Raheem Sterling, 24, ambaye amefunga mabao saba katika mechi nane kwa klabu na nchi yake msimu huu. ***(El Mundo Deportivo - in Spanish)***

**POGBA, MAN UNITED KUTETA**

Manchester United imefungua meza ya mazungumzo na kiungo wake Paul Pogba kuhusu uwezekano wa kumpa mkataba mpya. Nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 26, amebakiza miaka miwili katika mkataba wake hapo Old Trafford. ***(Times)***

**MADDISON MTEGONI LIVERPOOL**

Liverpool inavutiwa kumsajili kiungo wa Leicester City na England, James Maddison, 22, katika dirisha la usajili la Januari. ***(Star)***

**RAPINOE AIVUTIA BARCELONA**

Barcelona inafikiria dili la kumsajili winga wa Reign FC, Megan Rapinoe, 34. Nyota huyo wa kimataifa wa timu ya Taifa ya Wanawake ya Marekani ametwaa tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa Fifa Milan juzi. ***(ESPN)***

**HAVERTZ AIKUNA ARSENAL**

KIUNGO wa Bayer Leverkusen, Mjerumani Kai Havertz, ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United, Arsenal na Chelsea, amekuwa akithaminishwa na pauni milioni 90. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, amefunga mabao 17 katika mechi 34 za Bundesliga alizocheza msimu uliopita. ***(Sun)***

**SOLSKJAER AONGOZA KUTIMULIWA**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, anapewa nafasi kubwa ya kuwa kocha wa pili Ligi Kuu England kutimuliwa msimu huunyuma ya yule wa Everton, Marco Silva. ***(Sun)***

**WILLIAN ANUKIA JUVENTUS**

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Mbrazil Willian, 31, amekuwa akimulikwa na Juventus, ambayo inataka kuanza mchakato wa kumsajili wakati mkataba wake utakapomalizika majira ya joto yajayo. ***(Tuttosport, via Sky Sports)***

**TOMORI KUFUNGWA CHELSEA**

CHELSEA inatumai beki wa England U-21, Fikayo Tomori, 21, atakubali dili la mkataba mpya ndani ya wiki chache zijazo. ***(La Gazzetta dello Sport)***

**MANDZUKIC KUTIMKIA EPL**

STRAIKA wa Juventus, Mcroatia Mario Mandzukic, 33, anatumai kukamilisha dili la kutua Ligi Kuu England katika dirisha la Januari. ***(Tuttosport - in Italian)***

**AURIER CHAGUO LA MILAN**

AC Milan imemweka beki wa Tottenham, Muivory Coast Serge Aurier, 26, kama kipaumbele chao kwa wanaowawinda kuwasajili. ***(Sport Mediaset, via Teamtalk)***

**LONGSTAFF, HAALAND KWA UNITED**

Manchester United inajiandaa kuwa 'bize' katika soko la usajili la Januari, na kiungo wa Newcastle na England, Sean Longstaff, 21, pamoja na mshambuliaji wa Red Bull Salzburg, Mnorway Erling Braut Haaland, 19, wakiwa ndio kipaumbele. ***(Manchester Evening News)***

**NIKE, LIVER KUWEKA REKODI**

LIVERPOOL inakaribia kukubali kuweka rekodi ya udhamini wa jezi kwa klabu hiyo na Nike utakaoanza msimu ujao. ***(Telegraph)***

## HABARI MICHEZO

# WADAU WAISHUKIA TFF NDAYIRAGIJE KUINOA STARS

**Na Faustine Feliciane**

KITENDO cha kocha wa timu ya Taifa 'Taifa Stars' kubeba majukumu mawili ya kukinoa kikosi hicho pamoja na klabu, kimepingwa vikali na wadau wa soka huku wakieleza kinachangia kushindwa kutekeleza jukumu hilo la kitaifa ipasavyo.

Hayo yamekuja kutokana na Kaimu Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije kubeba jukumu hilo huku akiendelea kuwa Kocha Mkuu wa Klabu ya Azam ambayo mbali na kushiriki Ligi Kuu Bara, pia ina kazi kubwa ya kuiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Mbali na Ndayiragije kuwa Kocha Mkuu wa Azam FC, lakini pia wasaidizi wake, Selemani Matola ni Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania ya Kilimanjaro, huku Juma Mgunda akiwa Kocha Mkuu wa Coastal Union ya Tanga zote zikishiriki Ligi Kuu Bara.

Henry Tandau akizungumza jana jijini Dar es Salaam, alisema haoni kama ni utaratibu mzuri kwa kuwa kila upande unaumia kuanzia kocha, klabu na timu ya taifa.

Tandau alisema Ndayiragije anakuwa hana muda wa kutosha kwenye klabu yake na hata timu ya taifa kutokana na majukumu kuingiliana.

"Kwangu naona si utaratibu mzuri sana, tazama Azam ilitangulia Zimbabwe bila kocha wake ambaye alikuwa na majukumu ya Taifa Stars, mimi nafikiri kocha anahitaji muda mrefu na timu, iwe Azam au timu ya taifa sasa kwa huu utaratibu naona kila mmoja anaumia na ndio maana unaona timu zote hazipata matokeo mazuri katika mechi za mwisho," alisema Tandau.

Aidha, alisema kama TFF imeamua kumpa kazi ni vyema wakakubaliana na Azam ili atulie sehemu moja na kupata muda mrefu na timu.

Hamadi Hassan, shabiki kindakindaki wa Taifa Stars, alisema timu yoyote iweze kupata matokeo mazuri kocha anatakiwa kuwa na timu kwa muda mwingi kuiandaa.

"Hata mifumo itakuwa inamvuruga kichwani mara afikirie klabu yake huku jukumu la timu ya taifa, TFF sasa inapaswa kutangaza kocha mkuu mapema sivyo pande zote zitaumia," alisema.

"Matokeo mabaya kwa Azam [dhidi ya Triangle] na hata Taifa Stars dhidi ya Sudan, hilo pia linaweza kuwa sababu kwa kuwa Ndayiragije hakupata muda wa kutosha kuchekecha kikosi chake."

Azam ambayo itashuka dimbani ugenini Zimbabwe Jumamosi kuivaa Triangle FC, inahitaji ushindi wa kuanzia mabao 2-0 ili kusonga mbele kufuatia mechi ya awali kwenye dimba la Chamazi kukubali kipigo cha bao 1-0, huku Oktoba 18, mwaka huu Taifa Stars nayo ikihitaji ushindi kama huo ugenini dhidi ya Sudan ili kuweza kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) kufuatia kupata matokeo mabaya kama hayo ya Azam katika mechi ya awali Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.



Mshambuliaji wa Tanzania U20, Andrew Simchimba (kulia), akipambana kuwania mpira na beki wa Kenya, Thomas Omenda katika mechi ya Kundi B ya kuwania ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Jinja, Uganda. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2. **MPIAGAPICHA WETU**

# Simchimba atupia Kenya ikiwashika

**Na Mwandishi Wetu**

MSHAMBULIAJI wa timu ya soka ya Taifa ya Vijana ya Tanzania Bara (U-20), Andrew Simchimba ameendelea kutisha mbele ya nyavu baada ya kuifungia tena timu hiyo wakati ikitoka sare ya mabao 2-2 na yosso wenzao kutoka Kenya katika mchezo wa Kundi B wa kuwania ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati (Cecafa U-20) uliochezwa jana mjini Jinja, Uganda.

Bao hilo la Simchimba limekuja akitoka kutupia hat-trick kwenye mechi ya awali dhidi ya Ethiopia wakati wakishinda kwa mabao 4-0 juzi.

**Kwa matokeo hayo, yosso hao wa Tanzania Bara wanaonolewa na Zuberi Katwila, wamefikisha pointi nne sawa na vinara wa Kundi B, Kenya ambao wana mabao mengi ya kufunga.**

Bao lingine la Tanzania katika mchezo huo wa jana lilifungwa na Abdul Suleiman wakati Otieno Odhiambo na Otieno Patrick waliifungia Kenya.

Tanzania itashuka tena uwanjani kesho kukamilisha hatua ya makundi kwa kuwavaa ndugu zao Zanzibar maarufu Karume Boys wakati Kenya yenyewe itamaliza hatua hiyo kwa kuwakaribisha Ethiopia.

Fainali za mashindano hayo yanayoshirikisha nchi 11 wanachama wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), zinatarajiwa kufanyika Oktoba 5, mwaka huu kwenye Uwanja wa Jinja.

# Azam sasa kamili kupindua matokeo

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya fungu la pili la wachezaji watano na kocha mkuu waliokuwa timu ya Taifa ya Tanzania 'Taifa Stars', kuwasili nchini Zimbabwe kwa ajili ya maandalizi ya kuivaa Triangle United, Azam FC imesema sasa kazi ni moja tu kupindua matokeo Jumamosi.

Kocha Mkuu wa Azam FC, Mrundi Etienne Ndayiragije anayekaimu nafasi ya Kocha Mkuu wa Taifa Stars, pamoja na wachezaji Frank Domayo, Mudathir Yahya, Shaaban Chilunda, Salum Abubakar 'Sure Boy' na winga Idd Seleman 'Nado', waliokuwa wakiitumikia Stars dhidi ya Sudan, Jumatatu waliungana na wenzao 18 wa klabu hiyo waliotangulia awali.

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Jafari Maganga, alisema kwa sasa jeshi la Azam FC limekamilika na tayari Ndayiragije amepokea jukumu hilo kutoka kwa msaidizi wake, Idd Cheche aliyekuwa ametangulia na fungu la kwanza.

"Tayari Ndayiragije amewasili nchini hapa [Zimbabwe] pamoja na wachezaji waliokuwa Stars na kuanza mara moja kukiandaa kikosi chake kuelekea mechi ya marudiano Jumamosi.

"Kuhusu hali ya hewa kwa sasa huku kuna joto kali na kuna jua sana mchana zaidi ya jijini Dar es Salaam, lakini hilo tunaamini wachezaji wameshaanza kuzoea," alisema Maganga. Aidha, Maganga alisema wachezaji wana ari kubwa ya kufanya vizuri katika mechi hiyo inayotarajiwa kuwa na ushindani mkubwa huku akieleza kinachotakiwa kwa sasa ni Watanzania kuendelea kuiombea.

Azam inahitaji ushindi kuanzia mabao 2-0 ili iweze kusonga mbele kwenye mechi hiyo ya Kombe la Shirikisho Afrika, kufuatia mechi ya awali kwenye dimba la Chamazi jijini Dar es Salaam kukubali kipigo cha bao 1-0.

## MIEMBENI YAANZA KWA KUIKWANYUA KIKWAJUNI

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Miembeni imeanza vema Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Kikwajuni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa Miembeni, Suleiman Jabir alisema siri ya ushindi huo ni wachezaji wake kucheza vizuri hususan katika kipindi cha pili.

Alisema walinzi na viungo walijituma na kuelewana vema, hivyo kuzitumia vizuri nafasi mbili walizozipata licha ya timu hiyo kuwa changa kutokana na kushuka daraja, jambo lililowafanya kusajili wachezaji wengi wapya kufuatia wazoefu kuondoka.

Jabir alisema matumaini yake ni kuona timu hiyo inafanya vizuri zaidi na hata kucheza Ligi Kuu msimu ujao japo ni mapema kusema hivyo.

Naye Kocha Msaidizi wa timu ya Kikwajuni, Robert Limo, alisema tatizo kubwa lililosababisha kupokea kichapo hicho ni wachezaji wake kutokuwa na mazoezi na maandalizi ya kutosha kuelekea mchezo huo.

Alisema hali hiyo inatokana na baadhi ya wachezaji kuwa watoro na kutega kuhudhuria mazoezi hali inayosababisha kuharibu programu ya kocha mazoezini.

# Michezo

Jumatano Septemba 25, 2019

Nipashe




## Messi apingwa tuzo Fifa, Van Dijk atajwa

HABARI UK 30

MWAKA WETU...



Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi akiwa na tuzo yake ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa Dunia, sambamba na winga wa timu ya wanawake ya Reign FC ya Marekani, Megan Rapinoe (kulia), aliyeshinda tuzo hiyo kwa upande wa wanawake, baada ya kukabidhiwa usiku wa kuamkia jana huko Milan, Italia. **HABARI UK. 30**

# YANGA NI USHINDI TU, ZESCO YAONYA

### Wachezaji walambishwa chao mapema kabla ya kutua Zambia kibabe, wenyeji watoa dozi huku...

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI Zesco United ikitoa onyo na kutuma salamu Yanga kwa kuibuka na mabao matano katika mechi mbili za Ligi Kuu Zambia ilizocheza Jumatano na Jumamosi ya wiki iliyopita, Yanga imetua salama Zambia, huku Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera akisema wamekwenda kupambana na kukamilisha vizuri kazi waliyoianza nchini wiki mbili zilizopita.

Huku Yanga ikisogezewa mbele mechi zake za Ligi Kuu Bara ili iweze kujiandaa vizuri na michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika, wenyeji wao Zesco, Jumatano iliyopita wakiwa ugenini waliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Nakambala Leopards kabla ya Jumamosi wakiwa nyumbani kushinda 2-1 dhidi ya Lumwana Radiants.

Kikosi cha Yanga kilichokuwa na wachezaji 10 pamoja na Zahera, kiliondoka nchini jana asubuhi na ndege ya Shirika la Ndege la Kenya (Kenya Airways), huku kundi la pili lilitarajia kupanda ndege hiyo jana usiku kungana na wenzao, kwa lengo la kuwakabili wenyeji wao Zesco FC hapo Jumamosi kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa.

Akizungumza na gazeti hili kabla ya kuondoka nchini jana, Zahera, alisema kuwa wachezaji wake wako tayari kupigana na "vita" iliyoko mbele yao ili waweze kusonga mbele katika mashindano hayo yanayofanyika kila mwaka barani Afrika.

Zahera alisema kila mchezaji wa Yanga anajua ugumu wa mchezo huo unaowakabili, lakini hawana hofu yoyote na wanaamini wataendelea kuwapa furaha mashabiki wao na kupeperusha bendera ya nchi vema.

Alisema wamejiandaa kukutana na changamoto mbalimbali za ugenini, huku wakijipanga kuongeza umakini katika mchezo huo wa marudiano.

"Tunakwenda Zambia katika mapambano, mnaweza kuita vita, ni mechi ambayo tunaitarajia haitakuwa nyepesi, wao wanahitaji kushinda na sisi Yanga tunahitaji kushinda, atakayepata ushindi, atasonga mbele, itakuwa ni mechi ya kupambana na kutumia nguvu," alisema Zahera.

Aliongeza kuwa anaamini wachezaji wake wakitumia vema nafasi watakazotengeneza kama wanavyofanya mazoezini, suala la ushindi katika mchezo huo litakuwa jepesi.

"Kwangu naamini kutengeneza nafasi za kufunga ndio kunaipa timu ushindi, ukienda tofauti, mambo yatakuwa magumu, ila tusubiri muda wa uwanjani tuone kile tutakachopata," Zahera alisema.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema kikosi chao kitakuwa katika mazingira tulivu na yatakayowafanya wachezaji wafikirie kupambana uwanjani.

"Tulianza kuweka mazingira mazuri huko huko nyumbani kwa kuwalipa mshahara wa mwezi wa nane, hilo ni moja ya eneo zuri litakalowafanya wakiwa huku (Zambia), wafikirie ushindi, ninaamini na mwalimu (Zahera), kwa upande wake atatimiza jukumu lake ili mwisho wa siku tutimize malengo yetu," alisema Mwakalebela.

Yanga inahitaji ushindi wa aina yoyote ili iweze kusonga mbele katika mashindano hayo baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 kwenye mchezo wa kwanza uliochezwa Septemba 14, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

# Aussems: Tunataka 3 za Kagera Sugar

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akionekana kuisuka zaidi safu yake ya ushambuliaji kupitia mastraika wake Mrundi Meddie Kagere, Mbrazil Wilker da Silva pamoja na muuaji hatari anayefanya makubwa akitokea benchi, Miraji Athumani, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems amesema wanakwenda kushinda dhidi ya Kagera Sugar.

Simba ambayo ilitarajiwa kuondoka leo asubuhi kuelekea Kagera tayari kwa mechi yao ya Ligi Kuu kesho katika Uwanja wa Kaitaba dhidi ya Kagera Sugar, itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu mbaya ya kupoteza nyumbani na ugenini dhidi ya wenyeji wao hao msimu uliopita.

Hata hivyo, Aussems jana alisema wanakwenda Kagera wakiwa na malengo ya kushinda na kwamba yaliyotokea msimu uliopita ni hamasa kwao kuweza kufanya vizuri katika mechi hiyo.

"Yaliyotokea msimu uliopita ni hamasa kwa wachezaji kufanya vizuri kwenye mchezo ujao na nimeshawaambia inabidi tuwaonyeshe kwamba sisi ni Simba. Tunakwenda na malengo ya kuhakikisha tunashinda," alisema Aussems ambaye huenda akamwanzisha Wilker katika mechi hiyo.

Tangu asajiliwe na Simba msimu huu, Wilker hajawahi kuichezea timu hiyo hapa nchini kutokana na kuumia wakati wakijiandaa na msimu mpya wakicheza mechi za kirafiki wakiwa kambini Afrika Kusini.

Katika mazoezi ya timu hiyo yaliyokuwa yakiendelea viwanja vya Gymkhana, kocha huyo amekuwa akionekana kujaribu kumuunganisha Wilker kwa nyakati tofauti na Kagere, Miraji pamoja Sharaf Eldin Shiboub na kwenye mechi ya kirafiki dhidi ya Azam B, Mbrazil huyo alitupia mabao mawili.

Msimu uliopita, Simba walishindwa kupata pointi Uwanja wa Kaitaba baada ya kuchapwa mabao 2-1 huku pia wakichapwa bao 1-0 Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >